Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI

**Kikao cha Tano – Tarehe 4 Februari, 2008**

*(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Naibu Spika (Mhe. Anne Makinda) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 58

### Kujenga Hospitali ya Wilaya ya Kigoma Vijijini

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Hospitali ya Mkoa wa Kigoma ndiyo inayohudumia wagonjwa kutoka Kigoma Vijijini na kwa kuwa msongamano mkubwa sana Hospitalini hapo hususani kwa wagonjwa wanaotakiwa kulazwa, na kwa kuwa kijiji cha Kalenge wilaya ya Kigoma vijijini kuna majengo yanayojengwa na mfadhili mmoja na yana nafasi kuweza kujenga Hospitali ya Wilaya:-

Je, Serikali haioni kuwa huu ni muda muafaka wa kuweza kuyachukua majengo hayo na kuyafanya yawe Hospitali ya Wilaya ya Kigoma Vijijini.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mbunge wa Viti maalumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati najibu swali namba 187 katika Mkutano wa Tisa wa Bunge lako Tukufu, nilieleza kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma Vijijini imeweka mkakati wa kujenga Hospitali ya Wilaya. Hatua za awali za kujadili na kupitisha uamuzi huu katika vikao vya Halmashauri zimefanyika. Aidha, kwa kuzingatia

makubaliano ya vikao vyote vilivyofanyika eneo la Kata ya Kandaga, kijiji cha Kalange limekubalika litumike kwa ujenzi wa Hospitali hiyo, hivyo, Halmashauri ya Kigoma Vijijini inaendelea kufanya mawasiliano na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ili waweze kupata kibali cha kujenga Hospitali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo yaliyoko katika Kijiji cha Kalange anayoyazungumzia Mheshimiwa Mbunge ni mali ya Kanisa Katoliki. Awali Halmashauri ilikuwa imekubaliana na mfadhili aliyejenga majengo hayo kuwa yatumike kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya.

Baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kuwasilisha ombi rasmi kwa mfadhili huyo ili majengo hayo yaweze kutumika kama Hospitali ya Wilaya, mfadhili huyu kupitia Askofu wa Jimbo katoliki la Kigoma ameeleza kuwa majengo hayo ni mali ya Jimbo na yatatumika kwa shughuli za Jimbo hilo. Hivyo siyo rahisi kwa Serikali kuyachukua majengo hayo bila kukubaliana na mmiliki wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa azma ya kuwa na Hospitali ya Wilaya inatumia, Halmashauri imeanza mkakati wa kujenga Hospitali ya Wilaya. Tayari wataalamu wa Ardhi na wasanifu Majengo wa Halmashauri hiyo wamefanya utafiti wa eneo, kuchora ramani na kuiwasilisha Wizara ya Ardhi Nyumba na Makazi. Kwa mwaka wa fedha 2008/2009 Halmashauri inategemea kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi huo.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza, kwa kuwa Wizara imesema kuwa kuna sehemu iliyotafutwa, tunaomba Mheshimiwa aweze kututajia ni sehemu gani kwani haijulikani

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, kama ifuatavyo:-

Nimesema kwamba katika jibu langu la msingi kwamba eneo ambalo limekubalika liko katika kata ya Kandanga Kijiji cha Kalange ambalo limekubalika na Mamlaka zote za Serikali za Mitaa ili ijengwe Hospitali ya Wilaya.

Na. 59

**Asasi za Kipesa Kutoa Mikopo Vijijini**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, awamu ya kwanza ya mikopo ya fedha za wajasiriamali zilitolewa na serikali kwa kila Mkoa hazikuwa motisha kwa wananchi wengi Vijijini, na kwa kuwa Serikali imeelekeza asasi za fedha kama Benki ya Posta, Pride, Scult n.k. kupeleka mikopo hiyo moja kwa moja vijijini na kwamba fedha hizo zingepaswa kuwafikia wananchi mwezi Disemba, 2007.

(a) Je, hadi kufikia tarehe 15 Januari, 2008 ni asasi kwa majina zitakuwa zimeanza kutoa mikopo hiyo?

(b)Je ni wajasiriamali wangapi kutoka Jimbo la Nyang'wale watakuwa wamepata mikopo kufikia kipindi hicho?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Philip Musalika lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Hadi kufikia tarehe 15 Januari 2008, Benki Kuu, kwa niaba ya Serikali ilikuwa imekamilisha kutiliana sahihi katika mikataba ya utekelezaji na makubaliano *(MOU)* baina yake na asasi za fedha 14, ambazo ni:-

*Akiba Commercial Bank Ltd,* Benki ya Posta, *Azania Bank Ltd, CRDB Bank Ltd, Dunduliza Cooperative Ltd, Kagera Farmers Cooperative Ltd, Kilimanjaro Cooperative Bank, Mbinga Community Bank Ltd, Mwanga Community Bank Ltd, Presidential Trust Fund (PTF), Pride (T), SCCULT 1992 Ltd, Uchumi Commercial Bank.*

Mheshimwa Naibu Spika, awamu ya pili ya mpango wa uwezeshaji ulizinduliwa rasmi tarehe 31, Disemba, 2007 katika Kijiji cha Msowelo Wilaya ya Kilosa. Akiba *COMMERCIAL Bank* walianza kutoa mikopo kwa wananchi wajasiriamali katika awamu hii ya pili, ambapo ilitoa mikopo ya kwanza kwa *SACCOS 3:* MMMK SACCOS ya Kilosa, Msowelo na Faraja Women *SACCOS* ya Gairo.

Benki na asasi zingine za fedha zilianza rasmi kutekeleza mpango huu tarehe 15.01.2008 baada ya kukamilisha maandalizi ikiwa ni pamoja na kusaini mkataba wa makubaliano.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu ya kwanza Wilaya ya Geita ambayo inajumuisha majimbo ya Nyang'hwale, Geita na Busanda ilitarajiwa kupata mikopo ya Tsh. 187, 500,000/- kiasi cha mikopo kilichotolewa na Benki ya *NMB* Tsh. 99,829,500/- na *CRDB* ni Tsh. 178,550,000/- kwa hiyo Wilaya ya Geita katika awamu ya kwanza walipata mikopo zaidi ya matarajio kwa Tshs. 90,879,500/-

Katika awamu ya pili ya mpango wa uwezeshaji Wilaya zimegawanyika kwenye sura tatu. Wilaya ambazo hazikupata mikopo kabisa katika awamu ya kwanza, Wilaya zilizopata mikopo pungufu ya matarajio na Wilaya zilizopata zaidi ya matarajio.

Katika awamu ya pili kipaumbele kimepewa Wilaya ambazo hazikupata kabisa mikopo na zile ambazo zilipata kidogo, kwa kuwa Wilaya ya Geita ilipata zaidi ya matarajio, haikujumuishwa kwenye awamu ya pili ya mpango huu.

Katika Jimbo la Nyang'hwale *SACCOS mbili (2)* ziliomba mikopo ya Tshs. 166,142,000/- na wananchi binafsi 126 waliomba mikopo ya Tshs. 280,780,490/-.

Wote hawa hawajapata mikopo waliyoomba, ingawa Wilaya ya Geita haipo kwenye awamu ya pili ya mpango huu wa uwezeshaji, utaratibu unafanyika ili wananchi wa jimbo la Nyang'hwale ambalo liko wilaya ya Geita waweze kupata mikopo kwenye awamu hii ya pili ya uwezeshaji na kukuza ajira. Utaratibu huu utahusisha pia majimbo mengine ambayo yatabainishwa kutokuwa yamepata mikopo katika awamu ya kwanza.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake ingawa hayakidhi haja. Amesema kwamba Geita haikuwemo katika awamu ya pili na kwa kuwa mikopo iliyotolewa tu kwa *SACCOS* anazosema ni mbili tu ya Katulu tu na Geita Mjini lakini wote wa Geita Vijijini wajasiriamali hawajapata kitu. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akahakikisha kwamba mikopo hiyo ambayo inahitajika sasa ili wajasiriamali wakanunue dawa ya kunyunyizia pamba na pembejeo itafika Nyang'wale tarehe ngapi mwaka huu?

Jambo la pili, Mheshimiwa Naibu Spika, inakuza sana suala hili kwamba hela ni nyingi sana za Mabilioni ya Kikwete, pesa za MKUKUTA wakati hazipo na hazitoshelezi. Je Serikali inaweza sasa iwe inatoa kimya kimya au ifute utaratibu huu.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza katika mpango huu wa pili tumegawa mikopo hii kwenye Wilaya ambazo kwanza hazikupata kabisa mikopo kwenye awamu ya kwanza na Wilaya hizi zimegawiwa Tshs milioni 200/- kila mmoja, halafu Wilaya ambazo zilipata kidogo kwenye awamu ya kwanza na zenyewe zimepewa Tshs milioni 100/- lakini katika Wilaya zote hizi kwenye sura zote hizi mbili vilevile Benki ya *CRDB* na *NMB* ambazo kwa makubaliano na Serikali, zitatoa mara tatu ya mikopo ambayo wamepewa na dhamana basi na zenyewe zitahusika kwenye Wilaya hizi .

Kwa Wilaya ya Geita kwa bahati mbaya ama nzuri kuna majimbo matatu ya Uchaguzi, Busanda, Geita, na Nyang'wale yenyewe, sasa katika kupanga mikopo hii haikupangwa kwa Majimbo lakini tunachosema sasa kwa sababu tumebaini kwamba kuna hali hiyo sasa Serikali inachosema ni kwamba baada ya kutoa mgawo kwa Wilaya bado kuna fedha ambazo zimebakizwa kwa makusudi ili yale majimbo na sehemu za nchi ambazo wananchi hawajaweza kufikiwa basi wafikiwe na ninaomba nimwahidi Mheshimiwa Musalika kwamba Serikali ilivyosema kwamba itakwenda Nyang'wale itafanya hivyo. (*Makofi*)

Lakini la pili ni kuhusu kiasi cha fedha, shilingi Bilioni 21 zinaweza kuonekana ni chache lakini kwa vyovyote vile ni nyingi mpaka sasa hivi ndani ya mwaka mmoja chini

ya mpango huu mikopo zaidi ya shilingi bilioni 32 imetolewa kwa wananchi 34,000 ambao kwa hali ya kawaida wasingeweza kufikiwa na mikopo kwa sababu hawana uwezo wa kwenda kukopa. Kwa hiyo, Serikali imefanya ilichosema kwamba kila mkoa utapewa shilingi bilioni moja alivyokuwa ametangaza Waziri Mkuu kwamba mikopo hii itakuwa ya masharti nafuu na kwamba itafuata taratibu za kibenki, kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Mbunge aende na sisi awahamasishe wananchi wa Jimbo lake la Nyang'wale na sisi kama Serikali na Wizara tutakwenda naye kwenda kushirikiana katika jambo hili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri amejibu vizuri kirefu sasa tuendelee, lakini kiongozi wa Kambi ya Upinzani amesimama.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED**: Ahsante sana Naibu Spika nina swali dogo la nyongeza:-

Kwa kuwa fedha hizi zinatokana na bajeti ya Serikali, katika wamu hii ya kwanza je, Serikali inaweza kutueleza ni tathmini gani ya kiuchumi iliyofanikiwa kutokana na awamu ya kwanza ya mkopo huu?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA MHE. JEREMIAH S. SUMARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini inafanyika na sisi tunaridhika, kwamba wananchi zaidi ya 34,000 wamepata mikopo hii ambayo wametumia kwenye shughuli zao za uzalishaji basi lazima kuna thamani iliyoongezaka kwenye uchumi wao wenyewe lakini vilevile kwenye uchumi wa nchi kwa ujumla . vilevile kuna fedha zingine ambazo zimetokana na hili mfano benki ya CRDB mikopo yake yote ambayo inazidi bilioni 16/- imetolewa kwenye vyama vya akiba na mikopo na hata hapa vilevile kuna thamani inayoongezeka kwenye uchumi, kwa sababu kwanza wananchi wamejifunza jinsi ya kuweka akiba na wameelekeza ile mikopo kwenye shughuli za uzalishaji. Kwa hiyo tunaamini ingawaje hakuna *empirical evidence* mpaka sasa kwa sababu mpango wenyewe una mwaka mmoja tu toka uanze lakini tunaamini kwamba hapo mbele ya safari tutakapofanya hivyo na kupata takwimu tutaweza kutoa taarifa yenye uhakika zaidi. (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika**,** kwanza napenda kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana, lakini tunachoona ni kwamba tumekopesha watu 34,000 bado hao ni wachache sana, tulifikiri bilioni 21 zingeweza kutosha lakini imeonekana hazitoshi kwa hiyo tunafikiria kuangalia utaratibu kwenye bajeti ijayo, tuweze kutenga fedha nyingi zaidi ili tuweze kuwafikia watu wengi zaidi. (*Makofi*)

Na. 60

**Leseni za Utafiti wa Madini**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, maeneo mengi ya Wilaya ya Chunya yamepewa leseni za utafiti wa madini *(PL)* kwa kampuni mbalimbali

(a) Je, ni kampuni zipi zilizopewa leseni za kutafuta madini kwenye maeneo ya Tarafa ya Kwanja?

(b) Je, leseni hizo zilitolewa lini kwa mara ya kwanza na zimehuishwa mara ngapi kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 1998?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu**:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni 20 zilipewa leseni za utafutaji mkubwa wa madini katika Tarafa ya Kiwanja kuanzia mwaka 1998 hadi 2007. Kampuni hizo ni John S. Mwapili (Leseni Moja) iliyotolewa mwaka 1998, kampuni ya *Borsa Company Limited* (Leseni Moja iliyotolewa mwaka 2000), kampuni ya *Impala Mining Limited* (Leseni Moja), *Afrigold Limited* (Leseni Moja), *Jambo Mining Limited* (Leseni Moja), *Jubilee Resources Limited* (Leseni Moja, *Sun Mining Limited* (Leseni Moja) na *Afrigola Limited* (Leseni Moja) zilizotolewa mwaka 2001; Kampuni za *Teamco Limited* (Leseni Mbili), *Afro Mining and Exploration Company Limited* (Leseni Mbili), *Oxford Development Limited* (leseni Mbili) *Shield Resources Limited* (Leseni Moja) na *Acrow Group of Companies Limited* (Leseni Mbili) zilizotolewa mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni nyingine ni Sun Mining Ltd (Leseni Mbili, *Lola Exploration Ltd* (Leseni moja), *Afro Mining and Exploration* (Leseni moja) na *Amazon Trading Co.* (Leseni moja) zilizotolewa mwaka 2005, Kampuni ya *Shield Resources Ltd* yenye leseni kumi na tatu (13); leseni sita zilitolewa mwaka 2005; leseni moja ilitolewa mwaka 2006 na leseni sita zilizotolewa mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni nyingine ni *SDS Gems* (leseni moja) na *National Gold Exchange* (Leseni moja) zilizotolewa mwaka 2006 na *Judy Gold Mines Ltd* (Leseni moja) ilitolewa mwaka 2007.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, leseni zilizotolewa kati ya mwaka 1998 na 2000 zimeishakwisha muda wake wa kipindi cha miaka 7 baada ya kuhuishwa mara mbili kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 1998. Leseni zilizotolewa mwaka 2001 zilitolewa mwezi Januari na zimekwisha Januari 2008 baada ya kuhusishwa mara mbili. Aidha, leseni zilizotolewa mwaka 2002 zitakwisha muda wake wa miaka saba mwaka 2009 baada ya kuhusishwa kwa vipindi viwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, leseni zilizotolewa kati ya mwaka 2005 hadi 2007 bado hazijamaliza kipindi cha awali cha miaka mitatu (3) na hivyo hazijawahi kuhuishwa.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuweza kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa inaeleweka wazi kwamba hayo makampuni 20 ndiyo yamehodhi ardhi yote ya uchimbaji katika Tarafa ya Kiwanja na karibu Wilayani Chunya na kwa kuwa hayo makampuni Mheshimiwa Naibu Waziri amesema karibu nusu yake yamehuisha leseni zake mara mbili au mara tatu na muda wake umekwisha. Je, Serikali itarudisha hizi leseni kwa wachimbaji wadogowadogo ili wao wawe na sehemu za kuchimba na kuondoa umaskini?

Swali langu la pili ni kwa kuwa Serikali kwa miaka mitano imetoa mtambo wa kusaga mawe katika Kijiji cha Matundasi kwa gharama kubwa sana na mtambo huo umekaa haufanyi kazi kwa sababu hauna vitendea kazi ambavyo ni magari na hauna pampu za maji, na kwa kuwa Serikali mwaka jana iliahidi kwamba ingebadilisha umiliki wa mtambo huu kwa mmiliki mwingine na kuweka vifaa vya magari na pampu za maji mwezi wa kumi mpaka sasa hivi hawajafanya je, Naibu Waziri anasemaje katika hilo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba nijibu maswali mawili kutoka kwa Mheshimiwa Mwambalaswa kama ifuatavyo:-

Kuhusu swali la kwanza la nyongeza la urejeshaji wa maeneo haya muda wake umeisha na haujahuishwa kwa wachimbaji wadogo naomba kulitaarifu Bunge lako na wananchi kwa ujumla kwamba zoezi la kuratibu maeneo ambayo yanafaa kwa wachimbaji wadogo linaendelea na tunachofanya ni kutathmini kuona kwanza kama kuna mashapo ya kutosha ambayo yanawezesha wachimbaji wadogo waweze kuchimba kwa kuzingatia pia teknolojia ambayo inatumika kwa kiwango cha uchimbaji mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli tunakubaliana na wazo la Mheshimiwa Mbunge kwamba ingekuwa vyema wachimbaji wadogo nao wakafikiriwa lakini niseme tu kwamba sasa hivi tunaendelea na zoezi kujiridhisha kwanza kama maeneo haya ambayo yameachwa hayajahuishwa na hawa waombaji waliokuwa nayo yanafaa kwa wachimbaji wadogo hilo tunaendelea kulifanyia kazi na tunamwomba Mheshimiwa Mbunge tunamwomba tuzidi kushirikiana na tutampatia maendeleo kwa jinsi ambavyo muda unakwenda. Kuhusu swali la pili la nyongeza, naomba nikubaliane naye kwamba ni kweli mwaka jana tulitoa taarifa kwamba kile kituo cha Matundasi Serikali ilikuwa imedhamiria kukikodisha kwa mwendeshaji mwingine ama pia Wizara yenyewe ilikuwa inaangalia uwezekano wenyewe wa kukiendasha; na mtiririko wa matukio ulikuwa kama ifuatavyo:-

Tarehe 31 mwezi wa nane tulipata taarifa kutoka kwa aliyekuwa akikiendesha Bwana Masule ya kuiomba Serikali akatishe mkataba kwa sababu ya alizoziona yeye kwamba asingeendelea kukiendesha kile kituo. Lakini tarehe 16 Mei, 2007 sisi kama Serikali tulikubaliana naye kwa sababu alikuwa anaendesha kwa mujibu wa Mkataba tuliokuwa nao na baada ya yeye kuachia hicho kituo Wizara ilitoa tangazo mwezi wa sita tarehe moja mwaka jana kwa ajili ya ukaribisho wa waombaji wengine; na kwa kweli

tangazo hili lilielekea kwa wananchi wa Mbeya ambao walikuwa na uwezo na hasa wachimbaji wadogo. Kwa bahati nzuri tulipata waombaji takribani wawili lakini bahati mbaya sana hawakuwa na sifa za kuweza kukidhi kukiendesha hicho kituo.

Kwa hiyo, zoezi la kutangaza mara ya pili likaendelea na tangazo la pili tulilitoa tarehe 21 Julai, 2007 na tuliweka siku ya ukomo wa maombi ni tarehe 21 Agosti, 2007. Tukapata waombaji lakini pia hatukujiridhisha kwamba wanafaa kwenye hilo zoezi na hatimaye tarehe 6 Novemba, 2007 tukawa tumetoa fursa nyingine kwa waombaji wengine na zoezi hilo la maombi lilikoma tarehe 20 Desemba, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoendelea sasa hivi nikupitia hayo maombi ambayo yalikuwa yameletwa ofisini kwetu tuone ni wapi waombaji wenye sifa zinazofaa hivyo kwamba tuweze kuwapa na kwa kweli lengo letu ni kumkodisha mwendeshaji wa kiwango cha uchimbaji mdogo.

Na. 61

**Utafiti wa Madini – Kahama**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kampuni ya Utafiti wa Madini ya Dhahabu ya *TWIGG-GOLD* ilianza utafiti kwenye eneo la Mwambomba, Kata ya Idahina Wilaya ya Kahama tangu mwaka 2000; na kwa kuwa, kabla ya utafiti eneo hilo lilikuwa likitumiwa na wachimbaji wadogo wadogo pia kwa kilimo cha ufugaji, lakini baada ya shughuli za utafiti kwenye eneo hilo waliahidi kusaidia baadhi ya miradi ya maendeleo ya kijiji hicho:-

(a)Je, kwa nini Serikali imetoa kibali cha kuendelea na utafiti zaidi ya muda uliowekwa?

(b)Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya unyanyasaji unaofanywa na watumishi wa Kampuni ya *TWIGG-GOLD* kwa wananchi wanaokutwa wakichunga ndani ya eneo la utafiti, au kuokota kuni bila kuathiri shughuli za utafiti;

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Mwabomba lililoko katika Kata ya Idahina Wilayani Kahama lilikuwa chini ya leseni ya utafutaji wa madini namba PL 1755/2001 iliyotolewa kwa Kampuni ya *Geotang Mining and Water Engineering* tarehe 7/8/2001. Baada ya kipindi cha awali cha miaka mitatu cha leseni hiyo kumalizika tarehe 6/8/2004 Kampuni hiyo haikuomba kuhuishwa kwa leseni hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya leseni ya Kampuni ya *Geotang Mining and Water Engineering* kumaliza kipindi cha awali na kutohuishwa, mwaka 2004 Kampuni ya *TWIGG-GOLD* kwa nyakati tofauti iliomba leseni mbili katika eneo la Mwabomba. Leseni ya kwanza ya utafutaji madini yenye namba PL 2752/2004 ilitolewa kwa Kampuni ya *TWIGG-GOLD* tarehe 8/10/2004. Leseni hiyo ilimaliza kipindi cha miaka mitatu ya awali tarehe 7 Oktoba, 2007 na Kampuni haikuomba kuihuisha leseni 6 Agosti, 2007 na haijamaliza kipindi chake cha awali cha miaka mitatu ambacho kinakwisha tarehe 5 Agosti, 2010.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali haina taarifa ya unyanyasaji unaofanywa na watumishi wa Kampuni ya *TWIGG-GOLD* kwa wananchi wanaokutwa wakichunga mifugo yao au kuokota kuni ndani ya eneo la leseni ya utafutaji wa madini.

Iwapo kuna unyanyasaji wowote unaofanywa na watumishi hao, tunawashauri wananchi washirikiane na viongozi wa Serikali za Vijiji, Kata, Wilaya na ofisi yetu ya madini iliyopo Wilayani Kahama ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wahusika.

Kwa mantiki hii Wizara yetu inamkaribisha Mheshimiwa Mbunge atuletee maelezo ya kina kuhusu tuhuma za unyanyasaji ili tuifanyie kazi.Mheshimiwa Naibu Spika, mmiliki wa leseni ya kutafuta madini hana mamlaka ya kuzuia shughuli nyingine ambazo hufanyika juu ya ardhi ya eneo la leseni iwapo shughuli hizo haziingiliani na utafutaji madini.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa sehemu ya eneo la Mwabomba iliyokuwa chini ya leseni PL 2752/2004 ambayo ilikwisha muda wake wa kipindi cha awali na haikuhuishwa, imeombwa na Kampuni ya *Kiokote Exploration Ltd.* tarehe 8 Oktoba, 2007. Ombi hilo bado linashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyofafanua kwenye jibu la sehemu (a), sehemu nyingine ya eneo la Mwabomba iko chini ya leseni ya utafutaji madini *PL 2752/2004 ya TWIGG-GOLD* iliyotolewa tarehe 6/10/2007. Leseni hii itamaliza kipindi chake cha awali cha miaka mitatu tarehe 5/10/2010 na itaruhusiwa kuhuishwa kwa miaka mingine miwili kwa masharti ya kuachia kiasi kisichopungua nusu ya eneo la leseni hiyo kwa sasa.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuuliza mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a)Kwa kuwa tatizo hapa ni unyanyasaji na wananchi wa Kata ya Idahina nimefanya mikutano zaidi ya mara tatu na wamenithibishia hali hiyo na mimi mwenyewe nimeona kwa macho yangu. Ninaomba Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu na wananchi wa Kata ya Idahina kwa nini wananyanyaswa katika maeneo yao ya asili na watu ambao hata siyo raia wa nchi hii? (*Makofi*)

(b)Kwa kuwa Naibu Waziri mwenyewe amekiri kwamba kampuni *TWIGG-Gold* muda wa leseni yao imekwisha. Hadi hii leo ninavyozungumza hapa Bungeni ma-*tent* ya kifahari ya watafiti hawa yako pale Idahina. Je, Serikali inaweza kuwaelekeza watu hawa waondoshe ma-*tent* yao pale iwezekanavyo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali ya Mheshimiwa Lembeli, kama ifuatavyo:-

La kwanza, tunampongeza kwanza kufanya mikutano na kusikia kero za wananchi. Lakini kama tulivyojibu kwenye suala la msingi tunaomba Mheshimiwa Mbunge, tushirikiane kwa pamoja atuletee maelekezo. Kwa kweli tungependa hata baada ya hiki kipindi hiki cha maswali na majibu kama inawezekana Mheshimiwa Mbunge, atupe maelezo sisi tulichukulie hatua mara moja kwa sababu hatuoni sababu ya wananchi kuendelea kunyanyaswa. (*Makofi*)

Lakini la pili, ni kwamba kampuni ya *TWIGG- Gold* muda wake umekwisha kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ile kampuni ilikuwa na leseni nilizoomba awali moja wake umeisha na haijahuisha na haijahuisha. Lakini ya pili inaisha mwaka 2010 imani yetu na ndivyo uelewa wetu ni kwamba ma-*tent* inayoonekana kule sasa hivi ni kwa maeneo ambayo kwa sehemu ambao leseni inaelendelea mpaka 2010. Lakini kama kuna kasoro ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, tushirikiane na ofisi yetu tuweze kuitatua hiyo kasoro. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la utafiti katika maeneo yetu hususan katika eneo la Bukombe, imekuwa ni shida sana na hasa kuna watafiti ambao wameendelea kukaa muda mrefu toka mwaka 1992 na kwa kuwa watafiti hawa wamechukua eneo kubwa sana naamini hata muda wa kuisha unapofika hawaachi eneo na kama wakiachia wanabadilisha jina. Je, Serikali itawasaidiaje wananchi wa Bukombe ambao wakipata maeneo yana dhahabu hasa katika maeneo ya Nyakasaluma na mengine Serikali inaingia pale na watafiti wanasema kwamba ninyi siyo eneo. Serikali inasema nini kwa wananchi wale? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili lilishawahi kujitokeza mwaka jana siwezi kukumbuka sana najua Mheshimiwa Mbunge, alishaliuliza na tukalitolea ufafanuzi. Ambacho naweza kusema ni kwamba kinachoendelea pale na tumekuwa tukijiridhisha mara kwa mara sisi kama Wizara kwa kushirikiana na ofisi zetu na viongozi wa ngazi mbalimbali kule, Wilayani wanaoendesha shughuli pale kwa makampuni ambayo yana leseni wanaendesha kwa mujibu wa Sheria na kanuni za nchi yetu.

Kwa sasa hivi hakuna leseni ambayo muda wake umekwisha lakini wakaendelea kufanya kazi zao ambazo walikuwa wamepewa awali kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo nilikuwa napenda tumthibitishie Mheshimiwa Mbunge, lakini pia kwa neema iliyoko katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge na Wilaya ya Bukombe, kwa ujumla kwa kweli kuna kampuni nyingi ambazo zinaomba za nje na

ndani ya nchi ya Tanzania, tulipotoa ufafanuzi mwaka tulielezea na nitamkaribisha Mheshimiwa Mbunge, tumpe taarifa ya wenye leseni, walioko pale siyo wote wageni, wako wengine wazalendo wa nchi hii.

Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge, tuzidi kushirikiana.

Kuhusu kuwawezesha wananchi wa Bukombe kama tulivyojibu kwenye swali la msingi kwamba bado tunaangalia kwa sababu kama eneo la sasa hivi la mtu si rahisi kulifanya liwe la wachimbaji wadogo lakini utaratibu huo unaendelea, zoezi hili linaendelea na kama ambavyo huwa tukisema kwamba kuna maeneo mengi ambayo sasa hivi tumeshatenga kwa mujibu wa taratibu zetu kuwa maeneo ya wachimbaji wadogo, lakini zoezi linaendelea.

Kwa hiyo, tutazidi kuwasiliana na Mheshimiwa Mbunge. Ahsante. (*Makofi*)

Na. 62

**Hifadhi za Taifa Wilaya ya Serengeti**

**MHE. MGANA I. MSINDAI (K.n.y. MHE. DR. JAMES MNANKA WANYANCHA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, asilimia 94 ya eneo la Wilaya ya Serengeti, imetengwa kwa ajili ya hifadhi ya Wanyamapori hivyo kusababisha hoteli nyingi za kitalii kujengwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, lakini hata hivyo hoteli hizo hazilipi ushuru wowote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, hali ambayo imesababisha kushuka kwa mapato ya Halmashauri hivyo kuleta umaskini mkubwa kwa wananchi wa Wilaya hivyo.

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu suala hilo?

(b)Je, ni lini itaruhusu Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti kutoza ushuru hoteli zilizo ndani na nje ya Hifadhi ya Serengeti kama ilivyokuwa hapo zamani kabla hoteli hizo kumilikiwa na watu binafsi?

(c)Je, Serikali inapendekeza kiasi gani cha fedha zitozwe ushuru kwa siku kwa kila mtalii anayetembelea na kulala kwenye hoteli hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, napenda kutoa maelezo ya msingi kama ifuatavyo:-

Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*) limepewa mamlaka ya kusimamia Hifadhi ya Taifa nchini. Hivi sasa, Hifadhi za Taifa zimeongezeka kutoka Hifadhi 12 za awali hadi kufikia Hifadhi 15 ikijumuisha Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.

Kuanzia mwaka wa fedha 1987/88 *TANAPA* iliruhusiwa kukusanya na kutumia mapato yote yanayotokana na Hifadhi za Taifa kujiendesha, kwa ajili ya uhifadhi, kuendeleza utalii, miundombinu hifadhini na kuanzisha Hifadhi mpya. Baada ya uamuzi huu kufanyika, Serikali ilisitisha kutoa ruzuku kwa ajili ya kuendesha Hifadhi za Taifa hapa nchini. Badala yake *TANPA* inalipa kodi ya mashirika.

Katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 *TANAPA* imelipa sh.3,571,833,548 bilioni kama *Coorporate Tax*, na mwaka 2006/2007 wamelipa karibu sh. Bilioni 7.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi uliofanyika Novemba, 2005 unaonyesha kwamba, Hifadhi ya Serengeti ina hoteli 22 na maeneo 59 ya kujenga mabanda ya kulala watalii ya muda mfupi. Hoteli saba (7) kati ya hizo ziko nje ya hifadhi na hoteli 15 ziko kwenye maeneo ya hifadhi. Hoteli zote zilizo ndani na nje ya Hifadhi hulipia leseni za biashara kwenye Halmashauri ikiwa ni kianzio cha mapato cha Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANAPA* inathamini mchango wa wananchi katika kutunza hifadhi zetu. Hivyo, kwa kupitia Idara ya ujirani mwema kila Hifadhiya Taifa hutenga asilimia 7 ya bajeti ya matumizi ya kawaida ya mwaka kwa ajili ya miradi ya ujirani mwema. Miradi inayohusika kwenye utaratibu huu ni ujenzi wa miundombinu ya kijamii kama vile, shule, nyumba za walimu, miradi ya maji na kadhalika. Pamoja na shughuli nyingine zinazolenga uboreshaji wa shughuli za uhifahdhi. Kati ya mwaka 2003/2004 na 2006/2007 Hifadhi ya Serengeti ilitoa takriban sh. 395,635,889 kwa miradi mbalimbali katika Wilaya ya Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu a, b na c kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Katika maboresho ya mfumo wa kodi za Serikali za Mitaa, mwaka 2004 Serikali ilifuta kodi kadhaa zilizoonekana kuwa kero ili kuboresha mazingira ya kibiashara na hatimaye kuongeza ukusanyaji wa mapato. Hivyo basi katika marekebisho namba 9 ya mwaka 1982 katika *schedule* kifungu cha 4 (d) imeainishwa kuwa Hoteli za Kitalii na mabanda ya kulala watalii zisitozwe ushuru wa Halmashauri. Wakati huo huo Serikali Kuu imekuwa ikiziongezea ruzuku Halmashauri ili kufanikisha uendeshaji wa Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imekuwa ikifanya jitihada kubwa kutangaza utalii ili kuvutia watalii wengi zaidi kutembelea nchi yetu. Aidha, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kuvutia wawekezaji kuwekeza kwenye huduma za malazi nje na ndani ya hifadhi. Ni imani ya Wizara kuwa zikijengwa hoteli nyingi nje ya Hifadhi zitasaidia kutoa ajira, kuongeza kipato cha wakulima, wafugaji na wavuvi.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa asilimia 7 inayotolewana *TANAPA* kwenda kwenye Halmashauri zinazozunguka Serengeti imepitwa na wakati.

(a) Je, Serikali iko tayari kuongeza ifikie hata asilimia 10?

(b)Kwa vile ruzuku inayotolewa na Serikali Kuu kwenda kwenye Halmashauri imekuwa ndogo kulinganisha na idadi ya watu wanaoongezeka na mambo yanayofanyika kule Wilayani. Je, Serikali Kuu, itakuwa tayari sasa kupitia upya asilimia ya ruzuku inayopelekwa kwenye Halmashauri ili iendane na wakati? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mgana Msindai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Msindai naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba viwango vinavyowekwa vya kutoa misaada kwa vijiji na kata ambazo zinazunguka hifadhi ni vidogo. Lakini pia gharama za uhifadhi na gharama mbalimbali za kuendesha hifadhi hizi zinazidi kupanda kila siku. Ninachopenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwa swali lake la kwanza na la pili, ni kwamba Serikali inachukua mapendekezo haya na itayafanyia kazi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea wengine nimewaona lakini wapo kwenye uchangiaji wa hoja inayokuja. Kwa muweke maswali mtachangia.

Na. 63

**Kuwalinda Wananchi Kando ya Hifadhi za Kimisi na Burigi**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa, Hifadhi za Taifa za Kimisi na Burigi zina wanyama wakali sana kama vile Tembo ambao wamezaliana kwa wingi na wamekuwa wakishambulia wananchi wa Karagwe na mali zao; na kwa kuwa, Wilaya ya Karagwe, haina watumishi na nyenzo za kujihami na wanyama hao:-

(a)Je, Serikali ina mikakati gani ya kudumu ya kuwalinda wananchi wa Karagwe na mali zao dhidi ya wanyama hao?

(b)Je, Serikali inajua uharibifu wa mali na vifo uliotokea jimboni Karagwe na ni fidia kiasi gani imetolewa?

(c)Je, kwanini Serikali haijengi ofisi za wanyamapori ndani ya hifadhi ya Kimisi pamoja na kuajiri maofisa wanyamapori Wilayani Karagwe ili kudhibiti Tembo hao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mikakati iliyopo ya kukabiliana na tatizo la wanyama waharibifu ni pamoja na ifuatayo:-

1. Kutenga Bajeti kila mwaka kwa ajili ya doria na msako wa kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu.

2. Kulinda na kuwafukuza wanyama wakali na waharibifu kutoka katika maeneo ya vijiji kwa kuwarudisha hifadhini na kuwaua pale inapotokea kuhatarisha mali na maisha ya wananchi.

3. Kuwapatia wananchi elimu ya uhifadhi, faida zake na athari zitokanazo na wanyamapori.

4. Kufanya utafiti zaidi ili kubaini njia nyingine za kudhibiti wanyama wakali na waharibifu.

5. Kuongeza idadi ya wanyamapori wakali na waharibifu kwenye *quota* ya wanyama wanaowinda kwa matumizi mbalimbali.

6. Kuwashauri wananchi kulima mazao mbadala ambayo hayapendwi na wanyamapori wanaopatikana katika eneo husika.

7. Wizara itaishauri Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, kuajiri watumishi wa kutosha kwenye taaluma ya wanyamapori kwa ajili ya ulinzi wa maisha na mali za wananchi dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inafuatilia matukio yanayotokea katika maeneo mengi yanayoathirika kutokana na wanyama pori wakali na waharibifu.

Katika kipindi cha mwaka 2001 hadi 2007 jumla ya watu 20 waliuawa na 7 kujeruhiwa na wanyama pori wakali na waharibifu katika maeneo ya wilaya ya Karagwe. Wizara hutoa kifuta machozi baada ya kupata taarifa sahihi kutoka kwa uongozi wa Wilaya husika kuhusu familia ya marehemu. Kati ya watu 20 waliouawa familia ya moja ya aliyeuawa na tembo mwaka 2006 ilipewa kifuta machozi kiasi cha 50,000/=. Familia za marehemu ambazo hazijalipwa kifuta machozi ni zile ambazo idara haipata taarifa rasmi toka Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe. Kuanzia mwaka 2007/2008 kifuta machozi kimeongezwa hadi shilingi 200,000/=.

Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, 2006/2007 na 2007/2008 jumla ya ekari 63.7 za migomba, 11 za mihogo, 41 za maharage, 19 za mahindi, 4 za viazi vitamu na ekari 4 za miti ya matunda ya aina mbalimbali ziliharibiwa katika Wilaya ya Karagwe. Katika kipindi hicho simba na fisi waliua ng'ombe 16 na mbuzi 20. Kufuatia matukio hayo wanyapori waharibifu wa aina mbalimbali 77 waliuawa. Tembo 415 na nyani 220 walidhibitiwa kwa kurudishwa ndani ya mapori ya Burigi, Biharamulo, Kimisi. (*Makofi*)

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inakamilisha ujenzi wa kituo kidogo cha doria *(Game Post)* katika Eneo la Rusumo, karibu na Pori la Akiba Kimisi. Kukamilika kwa kituo hicho kutaimarisha usimamizi wa pori ikiwa ni pamoja na udhibiti wa wanyama wakali na waharibifu kwa kushirikiana na Halmashauri husika. Aidha, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge, kuwa Wizara yangu imekuwa ikiajiri watumishi wenye taaluma ya wanyamapori kila mwaka kulingana na kibali kinachotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007 na 2007/2008 watumishi 125 waliajiriwa na kati ya hao 6 walipangiwa Kituo cha Burigi/Biharamulo/Kimisi. Kuhusu ajira za watumishi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe hili ni jukumu la Halmashauri ya Wilaya.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Niombe kutoa masikitiko yangu kwa majibu ambayo nimepewa na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba sijaridhika kwa sababu hapa katika majibu yake ya msingi amezungumzia kwamba Serikali imejenga kituo kidogo cha doria *Game Post* katika eneo la Rusumo ambayo iko katika Wilaya ya Ngara. Tatizo kubwa sana ni kwamba wanyapori hawa wako katika Wilaya ya Karagwe katika Kata za Kianga, Kata ya Nyakakika pamoja na kata ya Nyakasimbi. Kwa kuwa tatizo hili linaendelea kujitokeza mpaka sasa hivi ninapozungumza tembo wako kwenye vijiji vya watu.

(a)Je, Serikali kwa nini isifanye juhudi za haraka sana na ikafanya dharura kwenda kuwaokoa wananchi na hao wanyama wakali?

(b)Sikumbuki ni mara ngapi nimekuwa nikiomba hapa Bungeni, ninamwomba Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Waziri wafike wakajionee majanga ambayo yamewasibu wananchi wa Karagwe ambao wameshapoteza wananchi zaidi ya 20 na kuharibiwa mali zao, nilitaka nifahamu je, ni lini Mheshimiwa Waziri au Naibu wake wataweza kufika Karagwe haraka sana na kuokoa tatizo hili? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Blandes, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatuma askari wa uhifadhi katika Wilaya hiyo leo hii nikitoka hapa kwenye kipindi hiki cha maswali na majibu. (*Makofi*)

Pili, baada ya Bunge hili Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Mbunge watakwenda kuyakagua maeneo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Watakwenda tu sasa nyie vipi! (*Kicheko*)

Na. 64

**Dawa Zilizoisha Muda wa Kutumika**

**MHE. MARIA I. HEWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika usambazaji wa dawa za binadamu zinazotumika hospitalini hueleweka ni lini hizo zimetengenezwa na lina zitaisha nguvu:-

(a)Je, ni nani anayehusika kukusanya dawa hizo ili zisiendelee kutumika pindi linapotokea tatizo la ufundi juu ya ubora wa dawa hizo ambazo tayari zinakuwa vijijini?

(b)Je, kiasi gani cha dawa aina ya M.E.S (dawa ya kikohozi) ambayo ilitangazwa kuisha nguvu muda mrefu kugunduliwa na kuzuiwa au kuharibiwa ili isiendelee kutumika?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa Mbunge wa Viti Maalum kwana naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Kwa mujibu wa Sheria za udhibiti wa dawa, kila dawa inayotengenezwa, mtengenezaji analazimika kuweka katika lebo ya dawa tarehe ya kutengenezwa kwa dawa na tarehe ya mwisho ya matumizi ya dawa hiyo. Utaratibu wa uwekaji wa muda wa matumizi ya dawa hufanywa baada ya kufanyiwa majaribio ya kisayansi kwa kuzingatia vigezo vya kitaalam vya utengenezaji wa dawa. Baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika hospitali na vituo vya afya vya Serikali kitengo kinachohusika na dawa ni cha famasi na kinasimamiwa na Mfamasia au Fundi Sanifu Dawa au Muuguzi anayekabidhiwa kusimamia kazi za kitengo cha dawa. Wakati wa utoaji wa dawa, mtoa dawa anatakiwa kuangalia muda wa matumizi wa dawa kabla ya kumpatia mgonjwa. Aidha, mtoa dawa anatakiwa kuzingatia kanuni ya *First Expiring First Out (FEFO)* – maana yake dawa inayokaribiwa kuisha muda wa matumizi ndio inayotolewa kwanza. Dawa ikiisha muda wake wa matumizi huondolewa na kuhifadhiwa katika sehemu tofauti na huwekewa alama ya kuonyesha kuwa haifai tena kwa matumizi.

Utaratibu unaofuata ni kwa Mkuu wa Hospitali au Kituo cha Afya kumfahamisha Mhakiki Mali ya Serikali kuwepo kwa dawa zilizokwisha muda wa matumizi na yeye huiagiza Bodi ya Uhakiki mali kufanya tathimini ili kutoa kibali zifutwe kwenye vitabu vya mali ya Serikali. Baada ya hapo Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*) hufahamishwa ili kuelekeza utaratibu utakaotumika kutekeleza dawa hizo, chini ya usimamizi wa Afisa afya, Afisa Mazingira, Afisa Usalama na Mkaguzi wa Dawa. Hati ya

uteketezaji hutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi namba 1 ya mwaka 2003.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, dawa ya kikohozi aina ya MES ambayo ilitangazwa kutokidhi kwa kiwango chake cha ubora ni ile iliyokuwa ikitengenezwa na Kiwanda cha Afya *Laboratories* na tayari ilikwisha ondolewa kwenye soko. Mamlaka ya chakula na dawa ilitoa tangazo kwa umma, wauzaji na wasambazaji wote wa dawa zilizotengenezwa na kiwanda hicho kurudisha walikonunua dawa hiyo. Hadi sasa jumla ya chupa 18,480 za MES zimeondolewa sokoni. Ufuatiliaji unaonyesha kuwa hivi sasa dawa hiyo haipo tena katika soko. Aidha, Kiwanda cha Afya *laboratories* kilifungwa tangu Desemba 2005 baada ya kudhihirika kuwa kilikuwa hakijatimiza viwango vya ubora wa kutengeneza dawa.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hisia yangu ni hasa kwa kuhurumia vitengo au makundi mawili hapa nchini, moja ni lile la watoto wadogo na akina mama ambao ni nguvu kazi kubwa sana katika taifa letu ndiyo watumiaji wakubwa wa madawa haya. Nasema hivyo kwa sababu ndiyo wanayanunua. Je, Serikali kama yenyewe inakiri mimi mwenyewe kwa kusoma gazeti mwaka 2007 pindi wao wenyewe waliweza kugundua 2005 ndiyo wakafunga mpaka 2007 ndiyo wanakuja kututangazia hili. Je, hawaoni kwamba kitengo walichonacho ni dhaifu na kwamba wanapaswa sasa kuwa makini na watuambie watakuwa na operesheni mara ngapi kwa mwaka kwa kufuatilia utekelezaji wa madawa haya? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria I. Hewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokuwa nimezungumza katika jibu langu la msingi, nimesema kwamba zile zilipofahamika mwaka 2005 mamlaka ya Chakula ya Dawa ilitoa tangazo kwa umma, kwa maana hiyo waliagizwa wale wauzaji na wazambaji zote wa dawa walizotengeneza kuzirudisha katika kile kiwanda. Mimi sidhani kama kuna upungufu katika utendaji wa Serikali kwa sababu kawaida huwa kila mwaka na kila wakati inapobidi mamlaka ya chakula na dawa ikishirikiana na Halmashauri husika huwa zinafanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maduka. Kwa hiyo, inaweza kuona zile dawa ambazo hazifai. Kwa maana hiyo, napenda nichukue nafasi hii kwa Waheshimiwa Wabunge, kuwahakikishia kwamba mamlaka ya Dawa na Serikali kwa ujumla inatekeleza hilo. Napenda niwakumbushe tena wale wote wanaohusika katika Halmashauri wafamasia na watu wa *TFDA* waendelee kufanya ukaguzi wa hapa na pale kila inabidi ili tatizo hili lisijitokeze.

Na. 65

**Mikakati ya Kudhibiti Ugonjwa wa Malaria**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa ugonjwa wa malaria ni kati ya magonjwa hatari na sugu unaosababisha vifo vingi na kuathiri nguvu kazi Wilaya Liwale na nchini kote kwa ujumla:-

(a) Je, ni kweli kwamba malaria inaongoza kwa kusababisha vifo vingi nchini ikilinganishwa na magonjwa mengine kama vile UKIMWI n.k. na kuna takwimu kiasi gani za vifo kwa hivyo miaka ya karibuni?

(b) Kwa kuwa kinga ni bora zaidi kuliko tiba kwa nini Serikali haina kasi ya kuweka mikakati ya kutekeleza mazalia ya mbu sambamba na matumizi ya vyandarua vyenye dawa?

(c) Kwa kuwa hakuna tiba inayotokomeza kabisa ugonjwa malaria je, kuendelea kutumia dawa hizo mkila wakati hakuleti madhara yatokanayo na dawa hizo na kama yapo ni yapi hayo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) na (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Malaria ni ugonjwa unaoongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi na vifo vingi hapa nchini Tanzania. Karibu kila mwananchi ana uwezekano mkubwa wa kupata ugonjwa huo. Tafiti zinaonyesha kuwa makundi ya watoto chini ya miaka 5 na wanawake wajawazito ndio wako katika hatari kubwa zaidi ya kuugua malaria. Inakadiriwa kuwa watu milioni 16 hadi 18 huugua ugonjwa wa malaria na watu 100,000 hufariki ambapo kati yao 70,000 ni watoto kila mwaka.

Hali hii ni kubwa sana ukilinganisha na ugonjwa kama UKIMWI ambao mpaka sasa unakadiriwa kuwapata wagonjwa wapatao 400,000.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kuwa kinga ni bora kuliko tiba Wizara yangu imeamua kuanzisha mpango wa uwiano wa kudhibiti mbu waenezao Malaria kwa kutumia njia mbalimbali ambazo ni kama zifuatavyo:-

- Kutumia vyandarua vilivyowekwa dawa ya viuatilifu.
- Kupulizia dawa majumbani.
- Kuboresha mazingira na kuondoa mazalia kwa kuishirikisha jamii.
- Kupuliza dawa za kuua viluwiluwi kwenye madimbwi.

(c) Dawa zote zinazotumika zina madhara iwapo zitatumika bila ya kufuata maelekezo yatolewayo na watalaam. Hata hivyo dawa za tiba zinazotumika kwa sasa zimefanyiwa utatifi wa kina na kuonekana ni salama kwa matumizi. (*Makofi*)

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri. Kutokana na takwimu ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri kazitaja inadhihirisha kabisa kwamba malaria ni hatari kwa Watanzania na ndiyo inayoongoza kwa kuua Watanzania wengi.

(a) Kwa nini sasa Serikali isitangaze sasa kuwa janga la taifa? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa katika jibu lake namba amesema taratibu zimeshaanza kukinga kwa kuharibu mazalia ya mbu lakini siyo kweli kwa kuwa ninachokielewa mimi taratibu zilizoanza kutumia vyandarua vyenye dawa hapo inaonyesha kwamba hatuna *time frame* ya utekelezaji wa utaratibu wa kuzuia mazalia ya mbu. Kwa nini basi tusifuate utaratibu ambao unatumika hivi sasa huko Zanzibar ambao kusema kweli unaelekea kutokomeza ugonjwa huo na wanafanikiwa kwa kiasi kikubwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maswali ya Mheshimiwa Kigwalilo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ugonjwa wa malaria kwa sasa hivi Serikali bado haijaamua kuita kama ni janga kwa sababu kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi njia mbali mbali zinawezekana na kama elimu itatolewa malaria inaweza kuzuilika. Kwa hiyo, hakuna sababu ya kuitangazia kwamba ni janga la kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la pili la kuharibu mazingira ya viluilui, naomba tu nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, katika afua *interventions* ambazo tumezitumia ni kwamba moja ya mambo ambayo tumeyafanya ni pamoja na kuua vimelea. Lakini ni kwamba si vyandarua peke yake. Kwa mfano Muleba sasa hivi tunafanya umwagiliaji *(spraying)* ili kuweza kuwaua wale mbu lakini vilevile Halmashauri kwa kushirikiana na Mabwana Afya huwa wanatakiwa kupita katika maeneo husika. Lakini vilevile Serikali imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuweka mazingira safi ikiwemo kufunika madimbwi na kutoa vile vitu ambavyo vinaweza kusababisha kutuama maji na mbu kuzaliana. Kwa hiyo, si kweli kwamba Serikali haijachukua *interventions* zozote, Serikali inachukua na kuendelea na *interventions.*

Na. 66

**Uimarishaji wa Vyuo vya Elimu ya Juu Nchini**

**MHE. PINDI H. CHANA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 imeahidi kuendelea kuimarisha Vyuo vya Elimu ya Juu nchini lakini bajeti zake hazikidhi mahitaji kama Chuo Kikuu cha Mkwawa, Mzumbe na vinginevyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuliangalia tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Chana Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoelezwa wakati wa kusoma Bajeti ya Wizara yangu ya mwaka 2007/2008 na kwa kuzingatia mafanikio makubwa yanayotokana na mpango wa maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES), Wizara yangu inaandaa mpango wa maendeleo ya juu na ufundi yaani MMEJU ambao unalenga kupanua Elimu ya Juu. Ndani ya mpango huu mkakati wa kuviwezesha Vyuo Vikuu kupata fedha zaidi utazingatiwa. Ni matumaini ya Wizara kuwa bajeti inayotengwa na Serikali kwa ajili ya Vyuo Vikuu pia itakuwa inaongezeka mwaka hadi mwaka. Aidha, Wizara imeandaa Mradi wa *Quick Win* ambao utafadhiliwa na Benki ya Dunia ili kuboresha mazingira ya Vyuo Vikuu na Vyuo vya Ufundi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupatiwa ruzuku kutoka Serikalini, Vyuo Vikuu pia huhimizwa kuzalisha mapato ya ndani ili kuziba pengo hili. Hata hivyo, ili kuweza kuzalisha zaidi vitendea kazi na mazingira ya kufanyia kazi yanahitaji kuboreshwa.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa kuwa suala la elimu katika nchi yoyote na nchi zinazoendelea ni la msingi sana na hasa elimu ya juu, nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara kwa mpango huu wa MMEJU na mpango huu wa *QUICK WIN*:-

(a) Ningependa kufahamu ni lini miradi hii itaanza ili tuweze kujiandaa?

(b) Ningeomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kwamba huwa tunapitisha bajeti kwa ajili ya kila chuo na wakati mwingine bajeti tunazozipitisha hapa hazifiki kama vile tunavyozipitisha zinafika pungufu. Ningependa kujua kama hilo ni kweli na ni sababu zipi zinazopelekea bajeti zinazopitishwa zipelekwe katika Taasisi husika zikiwa pungufu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mipango hii itaanza lini, mpango wa MMEJU ndiyo sasa tunaumalizia na utakapokuwa umekwisha tutaupeleka Serikalini ili tuweze kuombea pesa lakini pia tutaomba Wafadhili ili waupitie mpango huu na tuweze kupata pesa. Kwa hiyo, utakapokuwa tayari tutaarifiwa.

Kuhusu *Quick Win*, hizi pesa sasa hivi zinakaribia kwenda vyuoni kwa ajili ya kuboresha miundombinu. Kwa sababu muundo hasa wa bajeti ya mwaka 2007/2008 ni kuendeleza rasilimali watu. Ikiwemo kuongeza udahili lakini kabla ya kuongeza udahili lazima tuboreshe miundombinu, kwa hiyo, hizi pesa za *quick win* ziko katika mchakato wa kwenda vyuoni ili kuboresha miundombinu. Pesa ambazo hazifiki vyuoni hizi ni

taratibu zinazotumika kwa sababu tunapomaliza bajeti haina maana kwamba pesa tayari ziko kule Wizarani au ziko Hazina. Inabidi hizi pesa zigawanywe na pia zitoke kwa awamu. Na tunajua zinatoka kwa awamu ya miezi mitatu mitatu yaani kwa *quorters*. Sasa kufuatia jinsi *quorter* inavyotoka na sisi ndiyo tunavyopeleka pesa katika vyuo na mara nyingi vyuo vingi vinapata pesa yote lakini mara chache ni kweli pesa haiendi yote kutokana na kiasi cha pesa iliyotolewa na Hazina.

Na. 67

**Mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya wanafunzi wa elimu ya juu walioko nje ya Mkoa wa Dar es Salaam wanapata matatizo wanapoomba mikopo ama kwa fomu zao kuchelewa kufika chuoni au kutofika kabisa:-

(a) Je, Serikali ina mipango gani ya kuandaa mazingira muafaka ya mikopo ili kuishi nje ya Dar es Salaam kusiwe ni sababu ya kukosa mikopo hiyo?

(b) Je, ni vigezo gani vinavyotumika kwa jamii kwa sasa kuchagua wanafunzi watakaoingia chuoni?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka utaratibu ambapo waombaji wa mikopo wanaoishi nje ya Dar es Salaam, wanapata fomu za maombi ya mikopo toka sehemu zifuatazo:-

(i) Kwa waombaji wapya, fomu hizo zinapatikana katika kaunta yoyote ya Shirika la Posta (Tanzania) ambazo ziko katika kila Wilaya nchini kote;
(ii) Kwa waombaji wanaoendelea na masomo, fomu hizo zinapatikana katika Ofisi za Washauri wa wanafunzi wa vyuo vyote vya elimu ya juu nchini;

(iii) Aidha, fomu pia hupatikana katika tovuti ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

(iv) Katika Ofisi za Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu Dar es Salaam.

Kwa wale waombaji wapya, fomu za maombi ya mikopo zilizojazwa ipasavyo na nyaraka husika kuambatishwa na kupelekwa katika kaunta yoyote ya shirika la Posta iliyo karibu na mwombaji ambayo husafirisha fomu hizo za maombi kwenda Bodi ya

Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa gharama za Bodi. Kwa wale waombaji wanaoendelea na masomo huchukua fomu hizo kutoka kwa Washauri wa Wanafunzi *(Deans of Students),* huzijaza na kisha kuziwasilisha katika Ofisi za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, kupitia vyuo vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha ili kuhakikisha kuwa kila mwombaji wa mikopo mwenye sifa anazipata fomu hizo mapema, fomu za maombi ya mikopo kwa mwaka wa masomo wa 2008/2009 zimekwishasambazwa katika shule za sekondari zenye kidato cha sita na vyuo vinavyotoa stashahada ili wahitimu watarajiwa wazijaze na kisha taarifa zao kuhakikiwa na Wakuu wa Shule kabla ya kujazwa na Wazazi/Walezi na Ofisi za Serikali za Mitaa na baadaye kutumwa katika Bodi ya Mikopo. Utaratibu huo utaiwezesha Bodi kupata taarifa ambazo ni sahihi zaidi, na kutoa muda wa kutosha wa kufuatilia usahihi wa taarifa za waombaji na kisha kutoa mikopo mapema kabla ya vyuo kufunguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba utaratibu huo unaotumiwa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu unawawezesha waombaji walio nje ya Dar es Salaam kuwasilisha maombi yao ya mikopo ndani ya muda unaotakiwa na hivyo kuondoa uchelewashwaji wa kupatiwa mikopo, endapo wanakidhi vigezo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu huwekwa na vyuo husika na kutangazwa kila mwaka katika vyombo vya habari hususan magazeti.

Utaratibu huo unahitaji kila mwombaji kujaza na kuwasilisha fomu za maombi katika chuo unachohitaji kujiunga nacho huku akiambatanisha vivuli vya vyeti vyake vya kitaaluma. Mbali na fomu za maombi, waombaji pia hutakiwa kufanya mitihani ya kujiunga na chuo *(matriculation exams)* kwa baadhi ya vyuo. Kupitia utaratibu huu wa kutuma maombi ya kujiunga na chuo na kufanya mitihani ya kujiunga na chuo, watahiniwa wenye sifa za juu za kitaaluma na waliofaulu vema mitihani hiyo ndiyo hupewa nafasi za kujiunga na vyuo baada ya kuhakikiwa na Kamisheni ya Vyuo Vikuu *(TCU)* na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE).*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Sera ya Serikali ni kuwakopesha wanafunzi wenye uwezo (*qualified),* asilimia 60 ya gharama za masomo; na kwa kuwa asilimia 60 inatolewa katika vyuo binafsi, kwa mfano, Tumaini ni kubwa mara dufu kuliko inayotolewa kwa shule au kwa vyuo vya Serikali; je, Serikali haioni kuwa Sera hii iliyoasisiwa na *World Bank* na *IMF* nchini inavipendelea vyuo binafsi na inadhoofisha vyuo vya Serikali? Na kama hivyo sivyo kwa nini Serikali haiweki *flat rate,* ada iliyo sawa kwa vyuo vyote bila kuangalia asilimia? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa Bodi ya Mikopo hutoa mikopo kwa wanafunzi waliofaulu daraja la kwanza kwa wanaume hadi daraja la kwanza na la pili kwa wanawake; na kwa kuwa wengi wenye viwango hivyo vya kufaulu ni wale ambao wanatoka katika vyuo vya

binafsi;  vyuo ambavyo familia zao zina uwezo; Serikali haioni kuwa inajenga tabaka la wenye uwezo na wasio na uwezo?  Na kama hali hii ikiachiwa kuendelea je, Serikali haioni kwamba vijana wetu watakosa uzalendo wa kupenda taifa lao na kwa hiyo, Wizara inachukua hatua gani  ili hali hii isitokee?  *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hayo ni maswali mangapi?  *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri jibu tena kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 60 *flat rate* ilitolewa mwaka jana kipindi cha 2006/2007.  Kwa mwaka huu wa masomo 2007/2008 tumeongeza vigezo na tumepanua wigo wa kutoa mikopo kulingana na uwezo wa mwombaji.  Kwa hiyo, kuna waliopewa asilimia 20, 40, 60, 80 na 100 kulingana na jinsi walivyotueleza, wana uwezo gani na walezi wao wana uwezo gani wa kulipia gharama za elimu ya juu.  Kwa hiyo, hatuna tena *flat rate.*

Kuhusiana na vyuo binafsi kwenda chuo binafsi ni matashi ya kila mwanafunzi anayehitaji kwenda katika chuo binafsi na unapoamua kwenda chuo binafsi ina maana umeamua utalipa gharama ya chuo binafsi kwa sababu kabla ya kwenda unaletewa *joining instructions.*  Kwa hiyo, sidhani kama hii inahitaji upendeleo kama nilivyomwelewa Mheshimiwa Mbunge.

*Division One and Two* tumesema mara nyingi kwamba kila mwaka tunaongeza nani tumpe mkopo.  Mwaka jana tuliwakopesha wasichana *Division One and Two* na wavulana *Division One.*  Kulingana na hali halisi ya fedha iliyokuwepo, kwa mwaka huu wa masomo tumeongeza ukopeshaji kwa *Division One and Two* wavulana pamoja na wale wa *Division One and Two* wasichana. Kwa hiyo, kadri pesa inavyoongezeka tunatumaini kwamba tutaendelea kuongeza wigo wa kuwakopesha wanafunzi wetu.  Na kwa masomo ya Ualimu, na zile fani ambazo ni mahususi za Sayansi, Udaktari, *Engeneering,* tumekopesha hadi *Division Three,* mradi mwanafunzi amedahiliwa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajitahidi kupanua wigo wa kuwakopesha wanafunzi na hatuhitaji kupendelea wala kuonea mwanafunzi yoyote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Mgeni Kadika, nina matatizo ya swali, takwimu ni nyingi sana.  Mheshimiwa uliza kwa kutumia kadi.  Waheshimiwa mjifunze kama tulivyojifunza kuweka kadi.

Na. 68

**Kesi za Unyanyasaji wa Wanawake**

**MHE. MGENI J. KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inapiga vita unyanyasaji dhidi ya wanawake vikiwemo vitendo vya kubakwa, kukeketwa, kupigwa na waume zao, kunyimwa urithi, kuolewa umri mdogo na kadhalika; na kwa kuwa mikoa inayoongoza kwa ukeketezaji ni pamoja na Mikoa ya Arusha, Dodoma na Mara; je, kesi ngapi zimefikishwa Mahakamani katika mikoa hiyo hiyo na kutolewa hukumu na ngapi zinazongoja kutolewa hukumu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, kama ifuatavyo:-

Takwimu ambazo zimetolewa ni kutoka Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mikoa kwa Mikoa ambayo imetajwa kwa kipindi cha mwaka 2006/2007.

Mkoa wa Dodoma kesi za ubakaji zilifunguliwa kesi 133, zimesikilizwa 79 na zinazoendelea kusikilizwa 54. Kesi za ukeketaji zimefunguliwa 6 na zote zimesikilizwa. Kesi za kupigwa imefunguliwa 1 na imekwishasikilizwa. Kesi za miradhi imefunguliwa na imekwishasikilizwa 1. Kuolewa umri mdogo zilifunguliwa 9 na zote zimesikilizwa.

Mkoa wa Arusha kesi za ubakaji zilizofunguliwa 154, zimesikilizwa 95 na zinazoendelea kusikilizwa 59.

Mkoa wa Manyara kesi za ubakaji zilizofunguliwa ni 52, zilizosikilizwa 8 na zinazoendelea kusikilizwa ni 44.

Mkoa wa Mara – Mahakama ya Wilaya ya Musoma, ubakaji kesi zilizofunguliwa ni 418, zimesikilizwa 263 na zinazoendelea kusikilizwa 153. Ukeketaji zimefunguliwa 13 na zimesikilizwa zote. Kupigwa zimefunguliwa 6 na zote zimesikilizwa. Mirathi zimefunguliwa 5 na zote zimesikilizwa. Kuolewa umri mdogo zilizofunguliwa 4 na zote zimesikilizwa. Kwa kuzingatia takwimu nilizokupa, hakuna mashauri yaliyofunguliwa katika Mikoa ya Arusha na Manyara kuhusu ukeketaji, kupigwa na waume, mirathi na kuolewa katika umri mdogo.

**MHE. MGENI J. KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kuna mtindo wa kukeketa watoto wachanga na baadhi yao hufa kwa kutoka damu nyingi na hayo husababishwa zaidi na wazazi wao; je, katika kesi hizo zilizotolewa hukumu na wazazi wamo? Na kama wamo ni hukumu gani walizopewa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashindwa kumhakikishia kama katika kesi hizo wapo wazazi ama walezi. Sina uhakika na hilo kwa hiyo, siwezi kumdanganya ila sina uhakika. Inawezekana wapo. *(Makofi)*

Na. 69

**Kuboresha huduma za simu za mikononi**

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH (k.n.y. MHE. LAUS O. MHINA)** aliuliza:-

Kwa kuwa huduma ya simu za mikononi ni muhimu sana hususan kwa mawasiliano kati ya maeneo ya mjini na vijijini:-

(a) Je, ni lini huduma hiyo itaboreshwa katika Kata ya Bungu hasa ikizingatiwa kuwa maombi ya wananchi wa eneo hilo ni ya siku nyingi?

(b) Je, kuna uwezekano gani wa kuweka mnara katika eneo la mji wa Mashewa kwani mawasiliano katika eneo hili si mazuri?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINI (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Eng.* Laus Omar Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Celtel* imekwishajenga mnara katika eneo la Magoma na kufikisha huduma ya mawasiliano katika eneo hilo na maeneo ya jirani. Kwa sasa mnara huo huwezesha kutoa mawasiliano kwenye vijiji vilivyopo maeneo ya jirani na Bungu, Mashewa na Kararani.

Aidha, Kampuni hiyo ina mpango wa kujenga minara miwili Wilayani Korogwe ambayo itafikisha mawasiliano Wilayani humo katika maeneo ya Bungu, Mahsewa na Kararani na vijiji jirani. Mpango huu wa kufikisha mawasiliano katika eneo la Mashewa Julai 2008, na Kararani ifikapo Septemba, 2008 na Bungu ifikapo Januari, 2009. Ujenzi wa minara hiyo utawezesha kupatiwa mawasiliano vijiji vyote vilivyopo kati ya Magoma na Mashewa, na pia vijiji vilivyopo maeneo ya Bungu pamoja na maeneo ya karibu na kijiji cha Kararani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya simu ya *Zantel* inatekeleza kwa awamu mipango yake ya utoaji wa huduma ya simu za mikononi ambapo awamu ya kwanza ni kutoa huduma katika makao makuu ya mikoa yote na sehemu za karibu na maeneo hayo. Awamu ya pili ni kutoa huduma katika makao makuu ya wilaya zote na maeneo ya karibu na awamu ya tatu ni kutoa huduma vijijini. Upimaji wa maeneo itakapowekwa minara ya *Zantel* katika maeneo ya awamu ya kwanza na ya pili umekamilika. Aidha, utekelezaji wa awamu ya tatu utaanza mwezi Novemba mwaka huu ambapo kijiji cha Bungu kinahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya simu ya *TTCL* ipo kwenye mikakati kabambe ya kusambaza na kuboresha huduma ya simu za mikononi kwa kutumia teknolojia ya *CDMA (Code Division Mutltiple Access)* katika maeneo mbalimbali nchini. Mradi huu unatekelezwa kwa awamu ambapo maeneo ya Bungu na Mashewa ni

mojawapo ya maeneo ambayo *TTCL* itayaangalia kwa ukaribu ili kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi.

Aidha, kampuni ya simu ya *Tigo* inalifanyia uchunguzi wa awali eneo la Bungu kwa ajili ya kuliweka katika mipango yake ijayo. Eneo la Mashewa tayari liko katika mpango mkuu wa ujenzi wa mnara unaotegemewa kuanza katikati ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni ya simu ya *Vodacom* imekwishabaini maeneo ya Bungu na Mashewa pamoja na maeneo mengine yaliyo jirani. Wataalamu wa Kampuni hiyo wako kwenye mchakato wa kubaini maeneo muafaka kwa ajili ya kujenga mitambo ya mawasiliano. Wataalamu hao pia wanaendelea kufanya tathmini za awali katika maeneo mengine ya jirani kama vile Mahezangulu.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri na yenye matumaini kwa wananchi wa Mashewa, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa katika eneo la Mashewa ni kijiji ambacho kwamba kina harakati nyingi za wafanyabiashara na vilevile wachimbaji wadogo wadogo wanaotoka katika maeneo ya Kalalani. Ni sababu zipi mpaka sasa hivi Serikali isiunganishe nguvu za pamoja katika makampuni haya ili wakaweka mnara mmoja na wote wakautumia katika shughuli za mawasiliano ili kupunguza gharama?

La pili, mfano huu unafanana vilevile katika maeneo ya upande wa Pangani, tatizo ni hilo hilo. Kwa nini mashirika haya hawaungani wakafanya hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINI (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema kuunganisha nguvu kwa kampuni hizi kwa kutumia minara kungeweza kuwapunguzia gharama lakini vilevile kupunguza gharama kwa watumiaji. Serikali kupitia *TICLA* inaendelea kuyashauri makampuni haya yafanye hivyo, ingawaje kwa kweli jambo hili bado liko katika sera zao za kibiashara. Lakini tunaendelea kuwahimiza itumie fursa hii kutoa tena wito wa Serikali kwa makampuni haya kukaa pamoja na kuangalia uwezekano wa kuunganisha nguvu kwa kutumia mnara mmoja mmoja badala ya kila kujenga wa kwake.

Na. 70

**Barabara ya Kahama – Geita Kupitia Bulyanhulu**

**MHE. JAMES D. LEMBELI (k.n.y. MHE. EZEKIEL M. MAIGE)** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Kahama – Geita kupita mgodi wa Bulyanhulu (k.m. 76) ni ya vumbi na wananchi wamekuwa wakilalamikia juu ya hiyo (vumbi) tangu mwaka 2000 bila ufumbuzi kupatikana hadi sasa; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais alikwishatoa agizo kwa Wizara husika ikae na wawekezaji wa *Bulyanhulu Gold Mine* na *Geita Gold* pamoja na wadau wengine ili kujadili na kuamua nini cha kufanya katika barabara hiyo:-

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani katika utekelezaji wa agizo hilo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

(b) Kwa kuwa wamiliki wa mgodi wa *Barrick* wamekuwa wakitoa dola milioni saba kama kodi kwa Serikali na dola 200,000/- kama kodi kwa Halmashauri ya Kahama kila mwaka; je, Serikali inaonaje kutumia mapato hayo pamoja na mengine katika ufumbuzi wa tatizo la barabara hiyo kuliko ahadi hewa za Serikali?

(c) Je, Serikali ipo tayari kufanya tathmini ya madhara ya kiafya na kimazingira yanayoweza kutokea kwa wananchi na mazingira yao kutokana na kutimuliwa na vumbi hilo kila wakati?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINI (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Jimbo la Msalala, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Agizo la Mheshimiwa Rais limetekelezwa. Serikali imekubaliana na Wamiliki wa mgodi wa Bulyanhulu na Geita kufanya ukarabati na matengenezo ya barabara ya Kahama hadi Geita ambayo ina urefu wa kilomita 131, kati ya hizo kilomita 79 ni za barabara ya Mkoa na 57 ni za Wilaya. Wamiliki wa migodi hiyo wamekuwa wakitekeleza makubaliano hayo kulingana na mipango yao na kutekeleza kazi hizo kila inapohitajika kufanya hivyo. Hata hivyo, mpaka sasa siyo Serikali wala wawekezaji hao waliopata uwezo wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hutumia mapato yake kutokana na vyanzo mbalimbali vya fedha kutekeleza kazi mbalimbali zinazoletwa katika Bajeti ya Serikali na kupitishwa na Bunge lako Tukufu. Mapendekezo anayotoa Mheshimiwa Bunge yuko nje ya utaratibu wa utendeji wa Serikali. Aidha, kwa kodi inayolipwa Halmashauri ya Kahama, Baraza la Halmashauri ndilo lenye uwezo wa kuidhinisha matumizi ya fedha kwa kazi wanayoiona inafaa kulingana na taratibu zilizopo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haioni sababu ya kufanya tathmini ya madhara ya vumbi kwa binadamu na mazingira. Kwa uzoefu wa maeneo mengine na tafiti zilizokwishafanyika, madhara haya yanaeleweka na njia za kuzuia zinajulikana pia, ni uwezo mdogo kiuchumi wa Serikali ndio unafanya urekebishaji wa miundombinu uende pole pole. Mheshimiwa Mbunge akumbuke kuwa zaidi ya asilimia 80 ya mtandao wa barabara nchi nzima bado ni wa udongo/changarawe. Hivyo tatizo si la barabara ya Kahama – Geita pekee bali ni tatizo la nchi nzima.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri ambayo kimsingi hayalengi katika kuleta suluhu na maelewano ya kudumu baina ya Uongozi wa Mgodi na wananchi hususan Wakakola na Bugalama, nina swali lifuatalo:-

Kwa kuwa moja ya kero kubwa ya wananchi wanaozunguka mgodi wa Bulyanhulu, ni vumbi linalotimuliwa na malori makubwa ya mgodi huu kiasi kwamba mapema mwaka huu kulitokea hali ya kuvunjika kwa amani baada ya wananchi kufunga barabara inayoelekea kwenye mgodi huo; je, na baada ya Serikali kusema kwamba haina uwezo?

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali bwana, umesema je, tena baada inaanzaje? *(Kicheko)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Je, Serikali inaweza kufafanulia wananchi kipi chenye tija kwao, afya zao, au mgodi ambao unazalisha mabilioni ya pesa kila mwaka bila kujali maslahi ya wananchi wanaozunguka mgodi huo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINI (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili kwa kweli lilikwishashughulikiwa na Serikali ngazi ya Wilaya na wawekezaji walishauriwa namna nzuri ya kuhakikisha kwamba barabara ile haitoi vumbi jingi kama ambavyo wananchi wamekuwa wakilalamika. Naendelea kusisitiza kwamba Serikali, hasa ngazi ya Wilaya, iendelee kukaa na wawekezaji hawa ili tatizo hili lisiwe kubwa sana wakati ambapo Serikali yenyewe haijawa na uwezo mkubwa wa kujenga barabara ile kwa kiwango cha lami.

Na. 71

**Kupanda Kwa Bei za Bidhaa**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza**:-**

Kwa Kuwa, kwa kiasi kikubwa bei za bidhaa zimepanda sana na hasa maeneo ya vijijini ambapo vitu kama chumvi, sementi, bati, na kadhalika, vinauzwa bei ghali; na kwa kuwa Serikali imekuwa ikichukua hatua kadhaa kurekebisha hali hiyo:-

(a) Je! bei ya bati, sementi, sukari, chumvi, imeanza kupungua (kushuka) kulingana na viwango halali?

(b) Kama ndivyo, bei hiyo ikoje katika mji wa Peramiho, Songea, Mbinga, Namtumbo na Tunduru ikilinganishwa na bei za zamani?

(c) Je! ni njia ipi inayotumiwa kuwapa taarifa wananchi kutambua bei hizo mpya hasa wale wa vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba bei za bidhaa mbalimbali hapa nchini zimeendelea kupanda.

Baadhi ya sababu za kupanda kwa bei ya bidhaa hizo ni pamoja na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na malighafi zikiwemo za mafuta, vipuri, umeme na nishati nyinginezo. Vilevile, kupanda kwa gharama za uchukuzi na umbali kutoka mahali bidhaa zinapozalishwa hadi kumfikia mlaji huchangia kuongezeka kwa bei za bidhaa husika. Sababu nyingine ni kuadimika kwa bidhaa kunakotokana na ongezeko la mahitaji kama ilivyotokea kwenye saruji hivi karibuni, ambalo pia huchangia kupanda kwa bei pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu hutumia mwanya wa mfumo wa soko huru unaoruhusu viwango vya bei za bidhaa kupangwa na nguvu ya soko lenyewe, kupandisha bei za bidhaa hizo kiholela kwa kiwango kikubwa zaidi ili kujilimbikizia faida kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hayo yote bei za bati, saruji, sukari na chumvi katika miji ya Songea, Peramiho, Mbinga, Namtumbo na Tunduru pamoja na maeneo mengine hapa nchini, zimeendelea kupanda.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, wastani wa bei za bati, saruji, sukari na chumvi katika miji ya Mkoa wa Ruvuma kati ya mwezi Julai, 2007, na Januari, 2008 ni kama ifuatavyo:-

Bati la geji 30 aina ya Kiboko, katika miji ya Songea, Peramiho na Mbinga imepanda kutoka shilingi 9,500 mwezi Julai, 2007 hadi 12,500 mwezi Januari, 2008. Katika Mji wa Namtumbo na Tunduru bati hilo limepanda kutoka shilingi 10,000 hadi 14,000 katika kipindi hicho. Bei ya chumvi laini gramu 500 katika miji ya Songea, Peramiho, na Mbinga ilipanda kutoka shilingi 150 hadi 200 wakati katika mji wa Tunduru bei ya chumvi hiyo ilipanda kutoka shilingi 300 hadi 500 ambapo Namtumbo bei ilibakia kuwa ya shilingi 200 wakati wote.

Bei ya sukari katika miji ya Songea, Peramiho na Mbinga ilipanda kutoka shilingi 900 kwa kilo hadi 1,200. Kwa miji ya Namtumbo na Tunduru bei ya sukari ilipanda kutoka shilingi 1,000 hadi 1,300. Na mfuko wa kilo 50 katika miji ya Songea, Peramiho na Mbinga ilipanda toka shilingi 14,000 hadi 16,000. Namtumbo bei ya saruji ilipanda kutoka shilingi 15,000 hadi 20,000 na Tunduru bei ya saruji ilipanda kutoka shilingi 18,000 hadi 22,000.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, bei za bidhaa hutangazwa na makampuni na mawakala wao kupitia vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na magazeti, radio na luninga. Njia nyingine ni kupitia maonesho yanayofanyika mara kwa mara ambayo huwapa fursa wananchi wanaotembelea maonesho hayo kujua bei za bidhaa husika.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa bidhaa hizo zilizotajwa katika swali langu la msingi na bidhaa nyingine zimekuwa ni kigezo kikubwa cha kuleta maendeleo katika maeneo yetu na hasa vijijini; na kwa kuwa mpaka sasa upandaji huo holela wa bei hizo umekuwa ni kikwazo na kero kubwa sana kwa wananchi wetu na hasa katika maeneo hayo ya vijijini, na kwa vile Serikali imekiri na kutambua hilo:-

(a) Je, Sasa ni nini kauli ya Serikali katika mfumo huo wa soko huria ambao ni holela kwa sasa kuweza kuwasaidia wananchi wetu kuondokana na adha ya kupanda kwa bei bila utaratibu kila siku?

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ziko Mamlaka za Serikali zinazoshughulikia suala zima la upandaji wa bei, lakini Mamlaka hizo zimejikita katika maeneo maalumu tu. Lakini katika bidhaa hizi muhimu zinazoshughulikia maendeleo ya wananchi bado hatuna utaratibu wa kuangalia mfumuko huo wa bei. Je, Serikali inawaambia nini wananchi katika kurekebisha tatizo hilo?

**MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda…!

**NAIBU SPIKA:** Naomba ujibu kwa kifupi, kwa niaba ya Serikali! Haya!

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna tatizo la bei kupanda. Lakini pia ni kweli kwamba mfumuko wa bei unachangiwa zaidi na bei ya chakula, hivyo ni jambo muhimu kwa wananchi wote kuongeza uzalishaji wa chakula ili mazao ya chakula ambayo yanachangia katika mfumuko wa bei yawe nafuu zaidi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine kwa ujumla washirikiane na Serikali katika kuhimiza uzalishaji wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usimamizi wa upandaji wa bei, napenda kusema kwamba kwa vile tumeingia katika mfumo wa uchumi wa soko, suala la usimamizi wa bei halipo tena. Kitu kinachoweza kufanyika ni pale tu katika huduma fulani ya baadhi ya huduma ambazo kuna ukiritimba ambao unasababisha bei hizi kupanda. Hapo ndipo Serikali itaweza kuchukua hatua za kudhibiti upandaji wa bei. Mfano ni katika shirika la *EWURA* ama *TICRA* mambo haya yanasimamiwa lakini hatuwezi tena kurudi kule tulikoanza tulikokuwa tuna Tume ya Bei ikisimamia upandaji wa bei. Jambo hili haliwezekani kwa sababu mfumo huu unaruhusu ushindani wa soko.

Na.72

**Soko la Mazao Mkoani Kagera**

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina mikakati mizuri kwa wananchi wake wote wakiwemo wakulima, wafugaji, wafanyabiashara ili waondokane na dimbwi la umasikini; na kwa kuwa katika Wilaya ya Biharamulo, Ngara, na Karagwe kuna wakulima wazuri wa karanga, kahawa, maharage, mihogo, viazi, ndizi na matunda ya kila aina, lakini tatizo kubwa ni ukosefu wa soko la uhakika:-

(a) Je! Serikali haioni kuwa huu ni wakati muafaka kwa mkoa wa Kagera kuwa na soko ili wananchi waweze kuuza mazao hayo hapa nchini kuliko mazao yao kuuza nchi jirani?

(b) Je! ni lini zao la kahawa litapatiwa soko la uhakika kuliko ilivyo sasa ambapo zao hilo linauzwa nchini Uganda?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO (HEZEKIAH N. CHIBULUNJE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inao mkakati wa kuendeleza masoko ya mazao ya kilimo chini ya mpango wa kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini, *ASDP,* ambapo Halmashauri za Wilaya zinatakiwa kubuni na kuanzisha miradi ya ujenzi wa masoko ya kisasa katika Wilaya zao.

Kupitia mipango ya kilimo ya Wilaya (*District Agricultural Plan* (*BADPS)),* uteuzi wa maeneo ya ujenzi wa masoko unatakiwa kufanywa na Halmashauri husika ili kuhakikisha kuwa masoko yatakayojengwa yanazingatia mahitaji ya eneo hilo. Kwa mfano, ujenzi wa masoko katika mikoa ya mipakani kama Kagera unatakiwa kuzingatia mahitaji ya kuuza mazao hayo katika nchi jirani. Pia kwa vile kuna baadhi ya mazao yana soko zuri katika nchi hizo jirani. Kinachotakiwa ni kuhakikisha kuwa mazao hayo yanauzwa kupitia mfumo rasmi kwenye masoko na sio kupitia njia za panya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa wito kwa Halmashauri za Wilaya kutumia fursa hiyo ya Mpango wa Kilimo wa Wilaya kubuni miradi ya masoko na kuainisha maeneo ya ujenzi wa masoko ya kisasa na Serikali itatoa ushirikiano kwa Halmashauri hizo kwa kuwapa utaalamu unaotakiwa kwa ajili ya ujenzi wa masoko hayo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, soko la kahawa Mkoani Kagera linaendeshwa kwa utaratibu wa ushindani kupitia kwenye soko rasmi kama ilivyo katika maeneo mengine

yanayozalisha zao hilo. Chini ya utaratibu huo Mkulima yupo huru kuuza kahawa kwa wanunuzi binafsi au kupitia chama cha Ushirika.

Jumla ya makampuni binafsi kumi na moja yamepewa leseni za kununua kahawa mkoani Kagera msimu huu. Aidha, wazalishaji wa kahawa maalumu huruhusiwa kuuza kahawa yao moja kwa moja nje ya nchi kwa kufuata taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hairuhusu uuzaji wa kahawa mbichi. Na ili kulinda ubora wa zao hilo na kudhibiti biashara ya magendo ya kahawa mkoani Kagera, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeanzisha mitambo ya kukaushia kahawa ili kutatua tatizo la hali ya hewa linalosababisha uuzaji wa kahawa mbichi. Pamoja na kutoa elimu kwa wakulima mipakani juu ya athari na hasara za uuzaji wa kahawa mbichi, Serikali inatoa mwito kwa wakulima wa kahawa kuuza kahawa yao kupitia kwenye mfumo rasmi uliowekwa.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika. Maswali ya Mheshimiwa Naibu Waziri, hayakidhi kwa wale wakulima kuridhika na masuala yake anayoyajibu au Serikali. Kwa sababu zao la kahawa, kwa kuwa wanauza mbichi ni kwa sababu wale wa vyama vya ushirika hawawaridhishi kwa bei yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba Serikali au Mheshimiwa Naibu Waziri, anijibu kwa nini wasiwaruhusu wakauza huko huko Uganda wanakotoa bei nzuri ya kuwaridhisha wananchi? Ni umasikini kuuza kahawa mbichi, sio kusema wanapenda. Suala la pili. Kwenye suala langu nimeulizia kuhusu maharage, mahindi na karanga. Kwa kweli naomba Serikali inijibu.

Hawa watu wa Karagwe, Muleba, Biharamulo, mazao yao wanakaa nayo na huku wana umasikini mkubwa sana. Kwa sababu kama kipindi hiki sasa hivi wanawaambia kuchangia shule, watatoa wapi pesa na hivi mazao yao yanawaharibikia ndani? Wawaruhusu wauze nje. Naomba anijibu Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Swala ni moja tu, wauze nje? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, napenda kujibu maswali yote ya Mheshimiwa Mwijage, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza hapa kwamba katika mfumo wa soko huru, uuzaji wa mazao haya wauzaji wako huru kuuza kwa vyama vyao au kwa wanunuzi binafsi. Na nikataja hapa kwamba kuna wanunuzi binafsi ambao tayari wamekwishateuliwa. Lakini suala ambalo Serikali inasisitiza kwamba lisifanyike ni kuuza kupitia njia za panya ambazo zinaanzisha utaratibu wa kuuza kahawa mbichi na hivyo kushusha ubora wa kahawa yetu. Lakini kimsingi kuuza mazao nje ilimradi tunafuata utaratibu inaruhusiwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha lakini tumezidisha dakika tano. Kwanza nawatambulisha wageni. Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zitakuwepo kwenye *pigeon holes* zenu, zitakuwepo huko. Sasa naomba sana zitakapotokea mjitahidi kusoma kusudi tufuate utaratibu wa kuendesha Bunge kwa kufuata Kanuni. Zitakuweko kule na msome vizuri.

La pili, wanasema kwamba zile *pigeon holes* zenu, hamchukui makabrasha yanayowekwa mle. Matokeo yake wanashindwa kuweka nyingine kwa sababu yanakuwa yamejaa. Kwa hiyo, mjitahidi wale ambao wanasahu kutoa wachukue.

Sasa wageni tulionao leo, kwanza ni vijana 21 kutoka Asasi ya Vijana ya *Tanzania Youth Alliance, TAYOA*, tafadhali msimame wote. Asante, karibuni sana. Lakini pia tuna wajumbe 20 wa Chama cha Huduma za walemavu Tanzania, naomba nao wasimame, 20. Naona hawakuja, watakuja kesho.

Nina mgeni wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Wassira, anaitwa Julius Gamba. Hakusema ni nani katika Jimbo lake au vitu kama hivyo. Manake Kanuni inasema lazima useme ni nani katika Jimbo lako. Kwa hiyo, tunaendelea.

Kuhusu matangazo ya vikao: Mheshimiwa Mohamed Misanga, Mwenyekiti Kamati ya Miundombinu, anaomba kuwatangazia wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 4 Februari, kutakuwa na kikao cha Kamati saa 7 mchana katika ukumbi namba 231. Saa saba mchana ukumbi namba 231.

Mheshimiwa Hassan Khatib, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, yeye anaomba wajumbe wa Kamati yake leo tarehe 4 Februari, saa 5.30 asubuhi hii kukutana kuwa na kikao katika ukumbi 428. Ni asubuhi hii saa 5.30.

Halafu kuna tangazo la Mheshimiwa Dokta Haji Mwita Haji, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii. Yeye anaomba wajumbe wa Kamati hiyo kukutana katika kikao cha Kamati yao leo tarehe 4 saa 5, katika ukumbi 219 saa 5.00.

Tangazo la mwisho, nimeagizwa na Mheshimiwa Spika, kuwa niwaeleze kuwa aliwahi kutangaza kuwa hatakuwepo katika Bunge hili kuanzia tarehe ya leo nadhani mpaka tarehe 9. Sasa nasema amesitisha safari hiyo na ameagiza kwamba atarejea kesho tarehe 5 Februari. Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kazi. Katibu! *(Makofi).*

## Muswada wa Sheria ya Utalii wa Mwaka 2007
## *(The Tourism Bill, 2007)*

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunayo orodha nzuri tu ya kujadili lakini naamini karibu wote mtapata nafasi kwa sababu tutajadili siku yote ya leo na kesho

asubuhi, tutaanza na azimio halafu tutaanza na Muswada ule mungine. Kwahiyo orodha yenu ni kubwa lakini mutapata nafasi. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa James Lembeli, atafuatiwa na Mheshimiwa Aloyce Kimaro na Mheshimiwa Michael Laizer, jiandae!

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa kuchangia Muswada huu siku hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda niipongeze Serikali kwa kuleta Muswada huu ndani ya Bunge lako Tukufu katika kipindi hiki. Muswada huu umekuja katika wakati muafaka ambapo Tanzania ni miongoni mwa nchi za Kiafrika ambazo hivi sasa zinavutia watalii wengi kutoka sehemu mbalimbali za Dunia. katika mazingira haya ambapo Tanzania inakuwa ni miongoni mwa nchi zinazopokea watalii wengi, sheria hii au Muswada huu wa sheria utasaidia sana katika kuhakikisha kwamba biashara ya utalii nchini inafanyika kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za kimataifa za utalii. Lakini sheria hii pia itakuwa inatambua umuhimu wa utalii na wajibu wake katika kuchangia uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu shabaha yake nyingine ni kuhakikisha kwamba Tanzania inapata mapato yake yanayostahili kutokana na biashara ya utalii. Wakati huo huo sheria hii ambayo naamini kabisa Bunge lako Tukufu litaipitisha, itatoa nafasi na fursa kubwa kwa watanzania kushiriki kikamilifu katika biashara hii, biashara ambayo inaweza kutoa fursa na nafasi nyingi za kazi kuliko sekta nyingine yoyote hapa nchini. Hali ilivyo hivi sasa biashara ya utalii ambayo kimsingi ni ina faida (*lucrative)* inafanywa na wageni. Na watanzania hawapati fursa sawa, lakini Muswada huu unalenga kutoa fursa kwa baadhi ya shughuli za utalii kufanywa na watanzania pekee. Muswada huu pia unazingatia suala zima la usalama wa Taifa na usalama wa wawatalii wanapokuja hapa nchini. Muswada huu umeweka pia kipengele kinachomtaka kila mtalii anayeingia hapa nchini kujiandikisha lakini pia kila mwenye biashara ya utalii anaandikishwa na anapata leseni sambamba na kuweka daftari la kusajili wageni wote anaowahudumia. Jambo hili ni zuri kwa sababu pia litaisaidia Serikali kuhakikisha inapata mapato yake sahihi kuliko ilivyo sasa ambapo wafanyabiashara wengi wa biashara hii, na hasa wale wa nje, wanadanganya Serikali na hivyo kutokulipa kodi zinazostahili. Kwa heshima kabisa napenda kumpongeza Waziri Maghembe, kwa kuleta katika Muswada huu kipengele kinachotambua kada ya waongoza watalii (*Tour Guides). (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapingana na baadhi ya Wabunge wenzangu ambao wamependekeza kwamba kada hii isiingie katika sheria mama bali iwekwe katika Kanuni. Hapa kinachotaka kufanyika ni kwamba baadhi ya wafanyabiashara (*tour operators)* wengine wako hapa waki-*lobby* Wabunge kwamba kada hii isiingie katika Sheria lakini iwekwe kwenye Kanuni. Lengo hapa Mheshimiwa Naibu Spika, ni *tour operators* kuendelea kuwanyonya, kuwakandamiza *tour guides* ambao kwa kweli ndio wanastahili sifa kwa maendeleo ya utalii wa nchi yetu hivi leo. Kada ya *Tour Guides* Mheshimiwa Naibu Spika, ndio sura ya utalii hapa nchini. *Tour guides* wa Tanzania ndio wanaoifahamu Tanzania, ndio wanayafahamu maeneo ambayo wazungu na wageni watalii wanaokuja hapa nchini. Na inasikitisha na kushangaza kuwa baadhi ya watanzania wanasema kwamba wazungu ndio wanaweza kuifanya kazi hiyo. Mimi

sikubaliani na ningependa kipengele hiki kiwemo katika sheria ili tuweze kuilinda kada hii, *(Makofi).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uzoefu wangu mdogo nilionao, kuendelea kuwaruhusu wageni kuwaongoza watalii wanapokuja nchini tunahatarisha utamaduni wetu. Lakini pia yapo madhara makubwa, kwa mfano, katika ajali asilimia 90 ya ajali zinazotokea Mlima Kilimanjaro, Mtalii kaanguka, kaporomoka, kafa, ukifuatilia kwa makini *guide* sio Mtanzania ni mzungu. Nimempongeza Mheshimiwa Maghembe, kwa kusimamia hili na Watanzania wamekuwa wakifanya hii kazi, mfano, *tour guides* wanaoongoza wageni wa kitaifa wanapokuja nchini katika hifadhi zetu ni watanzania. Mimi mwenyewe nimewahi kumwongoza mama Clinton. Alikuja hapa wakati nikifanya kazi *Tanzania National Parks.* Na tumeifanya kazi hiyo kwa umahiri mkubwa kiasi kwamba yule mama aliporudi kwao alimwandikia Waziri Meghji kumshukuru kwa kazi nzuri inayofanywa na Watanzania katika kuwaongoza watalii wanapokuwa katika Hifadhi za Taifa. Leo hii tunapozungumza, hifadhi za Taifa Ngorongoro, Idara ya Wanyama Pori, wameunda Idara Maalumu katika taasisi hizi (*tour guides).* Na wapo vijana ambao wamesoma, wana digrii, sasa kwa kuruhusu watu wengine kuifanya kazi hii, hii kada tutaipeleka wapi? Hii azima ya kutoa ajira 1,000,000 katika kipindi cha miaka mitano itatoka wapi? Kwahiyo namshukuru Mheshimiwa Maghembe kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kabisa Muswada huu, pia katika kipengele kinachotenga baadhi ya maeneo ya biashara ya utalii kufanywa na watanzania peke yao. Taifa linapoteza mabilioni ya pesa kwa kutegemea *tour operators* wa nje. Na hapa naipongeza Serikali kwa kupendekeza kwamba biashara kama ya kupandisha watalii milima ifanywe na watanzania peke yao. Biashara ya *rental cars*, mawakala wa tiketi za ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano mmoja. Kule Marekani, *America* ya Kaskazini ziara ya siku sita ya kupanda Mlima Kilimanjro inauzwa dola 3.500. Hii ilikuwa mwaka 2005 na kama kuna mtu anabisha naweza nikampa data hizi. Lakini pesa iliyokuwa inaingia kwenye *coffer* za Serikali ni chini ya dola 600. Hapa katikati hawa mawakala wa utalii wa nje wanapoleta wageni wanauza hizo safari kwa mawakala wa Kitanzania kwa dola 1,200. Zaidi ya dola 2,000 zinabaki Marekani. Sasa kwa Muswada huu nina hakika kwamba tutaweza kupata halali yetu. Najua wapo Watanzania wenye uwezo wa kuifanya biashara hii ya kupandisha mlima, Arusha, Moshi wapo. Makampuni ya kigeni yanayofanya biashara hiyo hivi sasa yanapiga vita Muswada huu. Lakini mimi nasema na naomba sana Bunge lako Tukufu lisikubali kabisa kuhalalisha biashara ya aina hii. Tutaendelea kunyonywa mpaka siku ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijagongewa kengele napenda kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. *(Makofi).*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana sasa….! Nilifikiri unasema umeunga tayari mkono. Haya! Endelea!

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na Muswada huu sasa naiomba Serikali pia iwe makini katika kuhakikisha kwamba kile kinachowavutia watalii wengi kuja nchini kinahifadhiwa na kinalindwa kwa hali na mali. Isije tukawa tunawahamasisha wageni kuja wakati tunaharibu yale mazingira ambapo watalii wanapenda kwenda. Kwa asilimia zaidi ya 80 wageni wanaokuja nchini wanatembelea hifadhi zetu, mbuga zetu. Sasa kitu ambacho ninataka kukisema ni *trend* ya Serikali kushinikiza baadhi ya mambo yafanyike katika hifadhi zetu na katika *game reserves,* kama ujenzi wa mahoteli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi nasikitika sana ninaposikia viongozi na baadhi ya watu wanatolea mfano wa Masai Mara kama mfano wa kuigwa. Masai Mara si kitu, imekwisha. Wakenya wenyewe wanatushangaa wakitusikia sisi tunasema kwamba Masai Mara wana vitanda 4,000 sisi tuna vitanda 1,000. Wazungu hao hao waliokuwa wanakwenda Masai Mara ndio wanaokuja Tanzania kwenda Serengeti. Mimi nimefika Masai Mara sio chini ya mara tano. Wakenya badala ya kusema njoo Masai Mara, wanakwambia njoo Masai Mara ufike Serengeti kwa urahisi. Sisi tunasema jenga mahoteli tujaze kule. Tutaharibu Serengeti na pengine katika kipindi cha miaka 10 ijayo Serengeti nayo ikawa si kitu, ikawa si kama Masai Mara. Ningeiomba sana Serikali, sambamba na Muswada huu iyalinde maeneo ambayo kwa kweli yanatuletea utalii mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa mahoteli katika hoteli zetu mimi sikatai kwa Serengeti ni wazo zuri. Lakini sio ufanyike kwa matakwa ya mtu, anataka hapo basi apewe. Zipo *General Management Plans* zifuatwe. Lakini unaposhinikiza madhara yake ni makubwa. Sopa *Lodge* ilipojengwa Serengeti, wataalamu wa hifadhi walikataa katakata isijengewe, hapo Serikali ikashinikiza, madhara yake leo yako pale. *Spring* iliyokuwa inapitisha wanyama pale imekauka na wageni ambao walikuwa wanatumia dakika 10 kuona wanyama sasa wana *drive* kilomita 20 kwenda *central* Serengeti kuona wanyama. Sasa mimi nilikuwa natoa angalizo *(Makofi).*

Mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Muswada huu tukiujadili, tumesikia ujio wa Rais Bush. Lakini sijasikia jitihada za Wizara kutumia nafasi hii ya ujio wa Rais Bush kuitangaza nchi yetu.

*(Hapa kengele ililia)*

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ya kwanza au ya pili?

**NAIBU SPIKA:** Ya pili.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kwamba mimi nafanya biashara za utalii na nina hoteli ya utalii. Naomba nimpongeze Waziri wa Maliasili na Utalii, niwapongeze wafanyakazi wa Wizara hiyo walioandaa Muswada huu na pia niwapongeze Kamati ya Maliasili na Mazingira kwa kukubali Muswada huu na kuuleta hapa. M mi nilikuwa nafuatilia sana Muswada huu. Pamoja na kwamba si mjumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira nilikuwa nahudhuria vikao hivyo ili kutoa mchango wangu kuona kwamba kila kilichojadiliwa kinakwenda

sawasawa. Naipongeza Kamati kwa kunikaribisha na kuleta Muswada huu hapa. Ninayozungumza hapa ni kwa maslahi ya Tanzania na Watanzania wote sio kwa maslahi ya mtu mmoja mmoja. Nawapongeza sana walioleta Muswada huu tukielewa kwamba pato la asilimia 17.5 linatokana na utalii. Biashara hii ya utalii ingeweza kuongezeka na pato la taifa kutoka Wizara hii likafikia mpaka asilimia 40 kama tungeleta Muswada mwingine wa wanyama pori. Tukaleta Muswada wa kulinda misitu yetu ambayo inavunwa kiholela na wageni wa China, Korea wamejaa kwenye misitu yetu, kila leo tunasikia magogo yamekamatwa, lakini matokeo yake yanaishia wapi wala hatupati hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwenye Muswada niende kifungu cha 7 ambacho kinasema waongoza watalii wote (*tour guides)* lazima wawe ni Watanzania na watapata leseni kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii. Hiki ni kitendo cha ujasiri. *Tour guides* wamekuwa wanadhulumiwa na *tour operators*, hivi leo tu kwenye *balcony* wako *tour operators* wamekuja ku-*lobby* kwa Bunge kifungu hiki kisipitishwe ili waendelee kuwanyonya.

Nashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia na kusisitiza kwamba hawa *tour guides* wapate leseni na wasimamiwe na Wizara. Nikiendelea kutangaza maslahi niliyonayo, pia mimi ni Mwenyekiti wa Kilimanjaro *Guards Association*. Hawa vijana wanapata leseni kutoka Kilimanjaro *National Park*, mwaka jana tarehe 30 Oktoba, idadi yao ilikuwa 884 wenye leseni. Kwa hiyo, hawa vijana (*tour guides)* wapo, inashangaza *tour guides* anatoka Kenya, anatoka Uingereza, *South Africa* na sisi tunamruhusu anapaleka wageni mlima Kilimanjaro, Mlima Meru, Mlima Oldonyolongai. Niishukuru Wizara kwa kuliona hili, kinachotakiwa sasa hawa *tour guides* tuwapange kwenye kanuni tuhakikishe kwamba wanakuwepo *tour guides* wa mlima (*mountain guards),* wanakuwepo *tour guides,* safari *guards* wa kupeleka wazungu kwenye Mbunga za Wanyama, wanakuwepo *marine guards,* wanakuwepo *city guards* wa kutembeza wageni kwenye miji yetu na wawe *graded.* Kunaweza kuwa na *guards* ambao ni *route guards* tuwatumbue . Mlima Oldonyolengai kama sio Mmasai ambaye yuko pale anayejua zile njia wewe mtalii au *tour guide* unayetoka Marekani wewe njia utaifahamuje? Mlima Kilimanjaro, Meru, Udzungwa, wanaofahamu zile njia ni *guards* ambao wametoka pale pale. (*Makofi*)

Pia kuwe na *interpretation guards* ambao wanaweza kueleza wageni bionuwai ya sehemu zile wanazopita kwamba haya ni maua, ua hili linachukua miaka miwili kukua, huyu ni simba, huyu anachukua miaka mingapi mpaka aweze kufika umri wa kuzaliana, huyu ni chui, huyu ni pundamilia, wawepo wale ambao wanaweza ku-*interprete*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe pia tuanzishe shule za kufundisha hawa *guards* kwa sababu wewe unatoa leseni, wote wana *qualification* na kwa kiwango gani. Kwa hiyo, kuna shule kama Mweka tupeleke pesa Mweka ili hawa vijana *tour guides* waweze kufundishwa pale na watambulike kimataifa. Vilevile pale Kilimanjaro *National Park* kuna Chuo cha Ujasiriamali ambacho kimetelekezwa na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Sasa naiomba Wizara ikichukue kile Chuo wawe wanawa-*train*

*mountain climbers* ndiyo tutapata viongozi wazuri wa kuongoza watalii mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipato cha mlima Kilimanjaro mwaka 2004/2005/2006 wamezalisha shilingi bilioni 44 kutoka mlima Kilimanjaro tu. Kwa miaka mitatu waliozalisha hizi pesa ni hawa *guards* na *potters,* kwa hiyo, hii Sheria ni vizuri ikawalinda na kwenye kanuni tuweke kanuni ya kulinda mishahara yao kwamba kuwe na *minimum salaries* za *guards and potters.* Na kwa kuwa hawa *guards* tunawapa leseni, tunaweza kuwabana wale ambao hawalipi sawa sawa, tunawanyang'anya leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hizo pesa ambazo zinazalishwa mlima Kilimanjaro ili uweze kulindwa vizuri, kuna Halmashauri tano, Halmashauri ya Rombo, Moshi Vijijini, Halmashauri ya Hai, Siha na Longido. Hizo shilingi bilioni 44 ingepaswa 10% ibaki kwenye Halmashauri hizo maana ndiyo wanatunza huo mlima. Hapa kuna kiini macho. Wanasema 7% itabaki kwenye lile eneo lililo la *National Park*, hawasemi 7% ya pato la *National Park*, wanasema *7%* ya bajeti ya *National Park.* Kwa hiyo, unakuta *National Park* ambayo ni mpya, bajeti yake ni kubwa kuliko *National Park* ambayo imeshabuniwa kama Kilimanjaro. Kwa hiyo, unakuta *National Park* ambazo zinaanza leo wanapata bajeti ya pesa nyingi. Ukigawa utakuta wale ambao ndio wageni ndio wanapata pesa nyingi kuliko wanaozalisha. Kwa hiyo, tubadilishe hiki kipengele tuseme ni 7% ya kipato cha *National Park* hiyo, hivyo ni 7% ya shilingi bilioni 44 *for the three years* ndio ziende Halmashauri kwa sababu ndiyo wanaolinda huo mlima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nisogee mbele niende kwenye Sura ya 9, Ibara ya 58. Naipongeza pia Wizara kwa kusema kwamba leseni zote za *tour operators* ambao wanapandisha mlima Kilimanjaro, Lengai, Meru, Uduzungwa zitatolewa kwa Watanzania tu sio kwa wageni. Tumekuwa tunapoteza fedha nyingi, zinabaki Uingereza Marekani kwa kuwapa leseni watu ambao wanakaa Marekani. Wanatuma wageni wanawaambia *tour guide* kwa sababu nimekuajiri nenda Kilimanjaro *Airport* saa mbili usiku watakuja wageni uwapandishe mlimani ukishamaliza kuwapandisha warudishe *airport* warudi Marekani, pesa zinabaki Marekani. Hapa *tour operator* au *tour guide* analipwa kiasi kidogo tu. Sasa kwa sababu hii imekuwa kwa ajili ya Watanzania tu bei zitapangwa vizuri. Fedha zitakuja Tanzania, *tour operator* atapata pesa yake sawa sawa, *tour guide* atapata pesa yake sawa sawa na wale wengine *potters* nao watapata kipato chao sawa sawa. Yule anayekwenda kinyume tutamchukulia hatua, tutamnyang'anya leseni. Na hii sio tu hata kuingia ubia hairuhusiwi, Mtanzania kuingia ubia na mtu mwingine yeyote ambaye si Mtanzania katika kupandisha mlima. Kwa hiyo, wale wote ambao wameingia ubia na matajiri wao wanabaki Uingereza, Marekani, baada ya kupitisha Muswada huu leseni zao sasa zitafutwa, hivyo atakayepandisha mlima ni Mtanzania peke yake, naipongeza sana Wizara. (*Makofi*)

Pia hili alilokuwa anazungumza Mbunge Lembeli kwamba hatujatumia vizuri hii fursa ya ujio wa Rais Bush, leo ungekuta Marekani kule New York kuna eneo linaitwa *time square,* ndiyo matangazo ya Tanzania yanapita pale, unaonyesha Serengeti, Mlima Kilimanjaro, Manyara, vitu vyote vya Tanzania halafu na kusema na Rais wao anakuja. Kwa hiyo, ndiyo time ya kuwaambia wa Marekani kwamba Tanzania ipo na mnaiyona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tutaendelea kwa utaratibu huu wa kuleta Muswada mzuri hapa Bungeni yale maisha bora kwa Watanzania yatapatikana na sisi tunao uwezo. Watanzania wana uwezo wa kufanya kazi hizo na nashukuru huu Muswada umekuja, Mungu aibariki Tanzania, Mungu awabariki Watanzania, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. MICHALE L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushurkuru kunipa nafasi ili na mimi nichangie Muswada huu wa Utalii. Lakini kuipongeza Wizara kwa kuleta Muswad huu ili tuangalie na kupitisha sheria hizi za utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi mojawapo iliyojaliwa kuwa na vivutio vingi sana ambavyo haviko katika maeneo mengine. Tusipotumia fursa hii tutabaki kuwa maskini. Naipongeza sana Wizara kwa ajili ya kuongeza *National Park* zingine na baadaye watalii watakwenda maeneo hayo na nadhani pato la taifa litakwenda juu zaidi. (*Makofi*)

Lakini ningependa kusema kwamba bado vivutio ni vingi sana katika nchi yetu. Yaani kila wakati tunazidi kuvumbua vingine vipya na watalii kuanza kwenda katika maeneo hayo. Lakini kikubwa sana ni ushirikishwaji wa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo. Ningependa kusema kwamba ushirikishwaji wa wananchi bado ni mdogo na wananchi wakishirikishwa maeneo mengine mengi yatajulikana. Nitoe tu mfano, kwenye *block* za *hunting blocks* hawa watu wa *hunting blocks* wanadhani kwamba maeneo hayo yamekuwa ya kwao moja kwa moja. Kuna *camp sites* wanazoweka katika hizo *hunting blocks*, zinawekwa kwenye ardhi ya vijiji, wale wawindaji, wanyama tu ndiyo wa kwao lakini ardhi siyo ya kwao. Kwa hiyo, kwenye hizo *camp sites,* wananchi wangelipwa hizo fedha za *camp sites* za eneo, wananchi ndiyo wangepewa walipwe hilo eneo. Hata wageni wanaokwenda pale, wanaolala kwenye hizo *camp sites*, wananchi wapate *fees* kwa ajili ya wageni wanaolala pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuipongeza Wizara ni kukubaliana na Kamati kwamba watakwenda kasi kuongeza *Wildlife Management Areas.* Kwa kweli tunawashukuru sana kwa sababu wako na Kamati na wananchi wanataka maeneo hayo yawe *WMA.* Serikali, Wizara wanakubaliana na sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba mrekebishe kidogo katika maeneo ya *WMAs* 16 zilizoanzishwa nchini, lakini bado utaratibu wa hizo *WMAs* kufaidika, bado kuna utata, kwa sababu ukisema fedha zote zipelekwe kwanza sijui Hazina au Wizarani ndipo zirudi vijijini itakuwa ni kero kubwa sana. Tunaomba muangalie utaratibu huo kwa sababu bado kuna utata mkubwa sana kati ya hayo maeneo waliyopata *WMA,* bado hawajapata faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ambayo ningependa kuizungumzia ni vivutio vilivyopo katika maeneo yetu. Namshukuru sana Mheshimiwa Kimaro amezungumzia Mlima Kilimanjaro. Mlima Kilimanjaro ni hifadhi mojawapo ambayo ndiyo iinaingiza fedha Serikalini kuliko zote. Nakubaliana naye kwamba Halmashauri

zinazozunguka Mlima Kilimanjaro, na nashukuru mmetaja na Longido, kwa sababu ni Halmashauri mojawapo tunasema kwamba tunaomba ile asilimia iongezwe. Hatusemi hatupati, tunapata, *National Park* ya Kilimanjaro inatusaidia, kila mwaka tunapata miradi kwa ajili ya *National Park* ya Kilimanjaro, lakini tunaomba iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo ningependa kulizungumza ambalo kidogo linaniuma hasa kuhusu jamii ya Kimasai. Mlima Kilimanjaro ni kivutio na Serengeti ni kivutio, Ngorongoro ni kivutio, Oldonyolengai ni kivutio, wanyama walioko nchini ni kivutio. Sasa jamii ya Kimasai imewekwa kama ni kivutio mojawapo.

Wote mnaona katika picha, matangazo ya utalii, unaona Morani wanawekwa, akina mama wa Kimasai wanawekwa. Lakini sioni faida inayopata jamii hiyo. Ukifanya nembo ya utangazaji hata kwa wacheza mpira wanalipwa. Sisi mnatuweka kwenye kundi la wanyama, ambao hawalipwi! Mlima Kilimanjaro ambao haulipwi, mnatutangaza tuwe kivutio cha kutangazwa, cha kuwaleta watalii, lakini hatuoni faida yoyote jamii hiyo itakayopewa. Hivi kama Mlima Kilimanjaro hauwezi kudai, sisi tunadai na mimi naona kama Mbunge ninayetoka katika jamii hiyo, naona kwamba huo ni unyanyasaji. Hatuwezi kuwa vivutio vya utalii lakini hakuna chochote jamii hiyo inachofaidika. *(Makofi/Kicheko)*

Watu wanaozunguka Serengeti wanafaidika, hata kwenye tiketi za *Precision Air* unaona akina mama wa Kimasai wamebandikwa pale. Uende Tanzania uwaone Wamasai. Uende Serengeti uwaone wanyama, uende Ngorongoro uone wanyama na Wamasai. Kwa hiyo, mimi napenda kusema kwamba mtafute asilimia ya pato jamii hiyo inayopata, kama hamtafuti, msitumie tena katika utangazaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni Mlima Lengai. Mlima Lengai upo jimboni kwangu. Ningependa kusema kwamba bado kabisa hatujatangaza Mlima Lengai. Mlima wa ajabu kidogo, ni tofauti na milima mingine, ndiyo maana tafsiri ya Lengai ni jina la Kimasai wanasema ni Mlima wa Mungu. Wamesema hivyo kutokana na maajabu ya huo mlima. Huo Mlima unabadilika siku hadi siku. Ukiangalia asubuhi mlima huo ni mweusi kabisa. Kesho unakuta mlima ule ule ni mweupe moja kwa moja. Kwa hiyo, unabadilika.

Hakuna mlima mwingine unaobadili sura kama huo? Ni Mlima Lengai peke yake. Siku hizi watalii wanakuja kwa wingi sana kuangalia Mlima Lengai, wanatoka Kenya wanapitia Longido, magari mengi sana hasa wakati huu unapotoa *volcano* unakuta magari mengi sana yako pale, wanapiga mlima picha. Siku hizi hawawezi kupanda kwa sababu ya *Volcano*. Ningeomba sasa tuanze kutangaza Lengai ujulikane na nchi zingine kwa sababu kitakuwa ni kivutio kimojawapo ambacho watalii watakuja kuangalia na kuongezea pato nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mlima Lengai uko karibu sana na *lake* Natron, ni kama kilomita kumi kutoka Mlima Lengai kwenda *lake Natron*. Kwa hiyo, unakuta kwamba kuna vivutio viwili vya ajabu, Mlima Lengai na *Lake Natron* ambao tuna flamingo wote duniani wanakuja kuzalia pale. Kuna maji ya moto kabisa ambayo yanatoka tu ardhini,

ukiyachota na kuweka majani unakunywa chai, hakuna tena cha kusema uchemshe. Ni vitu ambavyo vinaweza vikatangazwa na wageni kuja kuviangalia kwa sababu havipatikani, si rahisi kupatikana katika maeneo mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na naipongeza Wizara na naunga mkono Muswada huu. (*Makofi*)

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie kwenye huu Muswada wa Utalii. Niseme tu Muswada huu umechelewa kuletwa, ulitakiwa uwe umeletwa miaka mingi iliyopita na vilevile ulitakiwa uletwe pamoja na Muswada wa Sheria ya Wanyamapori kwa sababu vyote vinaendana. Kwa hiyo, kwa nafasi hii nimwombe tu Mheshimiwa Waziri ajitahidi na ule Muswada wa Wanyamapori uje mapema. Huu ni mwaka wa tano tunaambiwa unakuja mpaka leo haujaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tunasifika kwa kuwa na vivutio vingi na vivutio ambavyo vinajulikana ni vichache na muda mrefu vilikuwa vinatumiwa na majirani zetu. Mheshimiwa Waziri juzi ametaja mapato ambayo yamepatikana kwa miaka kama miwili/mitatu mfululizo. Mimi nimwambie kwamba hayo mapato bado yapo chini kwa sababu bado hatujatangaza vivutio tulivyonavyo. Bado hapa ndani hatujaenda kwenye maeneo mengi yenye vivutio vizuri ambavyo vinaweza kuvutia wageni kutoka nje. Bado tuko Kaskazini, bado kidogo tuko Zanzibar. Ukanda wa Kati una vivutio vya ajabu sana. Ukienda mimi nilikotoka kuna ngoma za asili, miaka mingi, ni kubwa watu wawili/watatu hawawezi kuzibeba na mpaka leo hawawezi kuzibeba na zipo *intact*.

**NAIBU SPIKA:** Ulikotoka wapi?

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Iramba Mashariki ndiyo vivutio hivi vipo. Kuna mawe ambayo watu walikanyaga na mpaka leo nyayo zao zipo. Kuna alama ambazo walikuwa wanakaa mpaka leo makalio yanaonekana. Hiyo siyo Iramba Mashariki tu, nenda Tabora, Rukwa, Mtwara, bado tuna vivutio vingi, tunaomba Serikali sasa itoe fedha kwa ajili ya kupanua utalii wetu. (*Makofi*)

Niseme juu ya kujenga mahoteli. Mahoteli mengi yanajengwa hapa kwetu kwa sababu za kisiasa, hatufuati utalaamu. Tuna *buffer zones*, nikianzia na Serengeti kuna hifadhi ya Gurumenti, Hifadhi ya Maswa, kuna makao *open* ambayo mahoteli yakijengwa kule wageni wataingia kirahisi zaidi ndani ya Serengeti, ndani ya Ngorongoro, Manyara na hifadhi zingine. Lakini tunakwenda kujenga katikati ya hifadhi zetu, matokeo yake tunaharibu maeneo ambayo wanyama wanazaliana, tunaingilia njia ambazo wanyama wanapita, tunakausha chemichemi za maji na hivyo kuchakaza maeneo yetu ya utalii. Mimi ningeomba tuwaachie watalaamu wafanye hizo kazi, tusitake kujaza hoteli katika Serengeti au katika Ngorongoro au Mikumi au hifadhi zingine zote tutakuwa kama wenzetu wa Kenya.

Mheshimiwa Lembeli amesema Masai Mara ilikuwa inajulikana sana, na sasa hivi umekwishakuwa Mji. Kwa hiyo, naomba tuwe waangalifu sana na hii sheria iangalie.

Tunazungumzia asilimia ya watu wanaopakana na hizi hoteli. *TANAPA* sasa hivi wana uwezo mkubwa sana, wana uwezo mkubwa kuliko Idara ya wanyamapori. Kama Idara ya Wanyamapori inalipa asilimia 25 *TANAPA*, kwa nini inashindwa kulipa hiyo? Mapato ya *TANAPA* yamekuwa makubwa mara kumi ya Idara ya Wanyamapori. Sasa ningeomba Mheshimiwa Waziri, mkakae mkafikirie upya hata kama hutafika asilimia 25 lakini iwe asilimia 10 au zaidi ili wananchi wapate faida ya wanyama wanaowatunza. Ukienda Ikoma, Ngurumeti, wananchi kila siku wanakamatwa kwa sababu ya kuwinda. Sasa walikwishaacha, wanawatunza hawa wanyama. Kwa hiyo, wapate ile asilimia kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, umefika wakati sasa wa Serikali kusimama imara isiendeshwe na hawa *tour operators* au hawa *professional hunters*. Wakati wa makisio mwaka huu zilikuja bei za wanyama hapa na Bunge hili likapitisha lakini mpaka sasa hawalipi, wamelipa wachache na wengine hawajaanza kulipa mpaka leo, wanavurugwa na *TAHOA.* Kwa hiyo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kwamba suala hilo lilishakuja Bungeni, Bunge likaidhinisha basi kusiwe na mchezo tena kule wa kubadili kienyeji kama kuna tatizo liletwe hapa Bungeni, tunapoteza fedha nyingi sana za kigeni kwa ajili ya hawa watu ambao hawaitakii mema Tanzania. Utalii ndio sekta pekee ambayo unaweza kujipangia bei unayotaka wewe na wasipokuja kuwinda wanyama wetu wanazidi kuzaana na kuongezeka na watakuja tu lakini leo hatufanyi hivyo!

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna mtindo umezuka, *hunting blocks* mwisho wake ni mwaka ujao lakini watu wanaruhusiwa kusema au kujenga *semi permanent camps,* kwa nini ifanyike hivyo? Kama *hunting blocks* kipindi chake kinaisha mwakani kwa nini leo waendelee kujenga? Utalii wetu unaingiliwa sana na kama wenzangu walivyosema, sasa Watanzania ndio wawe waendeshaji, wageni wakija waingie ubia na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tuangalie sana na ni lazima tuwathamini watu wanaoishi karibu na maeneo ya hizi mbuga zetu. Bahati nzuri mimi nimekuwa katika Wizara hii miaka mingi, nenda Hifadhi ya Lubondo kuna visiwa vinavyozunguka pale vya Mwaisome na vinginevyo, kuna visiwa ambavyo havitumiki lakini wananchi wanaambiwa wasijenge kwa sababu ni *buffer zone,* inaweza ikachukuliwa wakati wowote wakati wananchi wale wamekulia kule. Kuna sehemu zingine ambazo hazitumiki kama hifadhi ni lazima wananchi wapewe kwa sababu ndio unaleta mahusiano mazuri, hawataingia kuvua kwenye hifadhi, hawataingia kuvuruga wanyama walioko kwenye hifadhi kwa sababu wana eneo lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwamba umefika wakati ambapo ni lazima tuwathamini wananchi wetu kwa kuwapa maeneo na lazima tuwathamini wananchi wetu kwa kuwapa asilimia inayotosheleza kujiendeleza wao. Nasema Muswada huu umechelewa na wenzetu majirani, Waziri hakutaja, wanafaidika zaidi kiuchumi kuliko sisi, sasa hivi ni lazima tujirudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine niseme uchaguzi wa hizi bodi kwenye maeneo kama haya, tusichaguane kisiasa, tusichaguane kindugu, hapa wanatakiwa wataalam. Hizi

bodi siyo ajira ni miaka mitatu unaleta wengine wa kukusaidia. Sasa hivi kuna bodi huku huku Maliasili, wajumbe wa bodi wamekuwa kama watendaji na hiyo ndio inayoturudisha nyuma. Ni lazima Mheshimiwa Waziri ukae ufikirie kuna watu wako pale kwa sababu ni ndugu yangu mimi Mgana Msindai, ninamweka pale lakini hajui lolote, yeye ni kuhudhuria vikao na kupata posho, basi. Tunataka watu ambao watachangia maendeleo katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi lengo letu ni kukuza utalii, bilioni saba ni hela ndogo sana. Kama tungesimamia sawasawa na tujenge vyuo vya kufundisha watu wetu, watu wetu wengi hawajasoma ndio maana wanakuja watu kutoka nje lakini tungekuwa na vyuo, tuwafundishe, tungewapeleka nje wakasome wakirudi hali yetu isingekuwa kama hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kabisa tungekuwa tunapata zaidi ya bilioni 40 kwenye utalii na uwindaji wa wanyama pori. *Logs* watu wameshahodhi kama mali yao, hatuna Askari wa kusindikiza wawindaji, wanaachwa kambini, wawindaji wanaenda peke yao, akiwinda nyati mdogo akikutana na mwingine anawinda, ushahidi upo. Ninasema hivi kwa sababu nimekuwa kwenye Wizara hii kwa miaka 28, ninafahamu. Tutumieni tuwasaidie na lengo letu ni kuhifadhi hawa wanyamapori, kuhifadhi hii milima ili tupate pesa nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa nitamwita Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Riziki Lulida ajiandae na Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi ajiandae ni kuweka tu kadi kama tulivyoagizwa.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kupata nafasi ili niweze kuchangia katika Muswada huu. Kwanza kabla ya yote, ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri mambo machache, kwanza niishukuru Wizara, mwaka jana nilipokuwa nikichangia katika bajeti nilishauri mambo kadhaa na ninashukuru kwamba mengine yamefanyiwa kazi. Nimepata faraja sana kwamba Wizara ni sikivu kwa sababu niliyosema warekebishe, wamerekebisha basi waendelee kulinda heshima hiyo. Ninashukuru sana sina haja ya kuyataja lakini wanafahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie machache kwenye Muswada huu. Ninaomba wazingatie sana matumizi ya ardhi na ile Sheria ya Ardhi isipanguliwe kwa ajili ya uwekezaji. Wananchi wameshajua matumizi ya ardhi kupitia Sheria ya Ardhi, Na.5, jinsi vijiji wanavyoweza kumiliki ardhi na matumizi yake na hifadhi zake. Sasa nitaomba sana kama Sheria hii itazingatia sana uwindaji, ujenzi wa mahoteli, fukwe za bahari kwa sababu wanaojenga hoteli Dar es Salaam wanahodhi mpaka fukwe bila kujali kwamba katika Sheria na Kikatiba, inaruhusu mita 60 iwe wazi kwa wananchi

kuweza kuitumia. Lakini kutokana na kuwapa nafasi za kujenga hoteli namna hiyo basi wanaweka uzio kiasi ambacho mwananchi wa kawaida anashindwa kufika kwenye fukwe zile kwa sababu pamehodhiwa na mtu mwingine. Ninaomba sana waone jinsi gani wanaweza kuwashauri kutokana na Sheria hii ili wanapojenga wajue kwamba maeneo hayo ni maeneo pia ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine napenda kushauri katika vijiji wawahusishe wananchi. Tutumie TAMISEMI kama nilivyosema kuhusu umiliki wa ardhi. Wananchi wanajua kabisa kwamba eneo hili mwenye sauti ni Serikali ya Kijiji na wananchi wenyewe kwa hiyo tunapoenda kuweka miradi yeyote ile wananchi wanaokaa katika maeneo hayo, wafahamu eneo lao kumeletwa kitu gani badala ya ku-*impose* mradi halafu wananchi wanashangaa nani kaingia hapa, anafanya nini? Hawajui kinachofanyika pale au gema linalofanyika pale kama ni kwa manufaa yao kiuchumi, kimaendeleo, hawafahamu ni watu ambao wametengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba wafanye uwekezaji shirikishi hata kama wananchi hawawezi kushiriki kikamilifu katika kunyanyua uchumi pengine ili kuona kama mradi ule ni wao angalau wafahamu nini kinatendeka. Mara nyingi wawekezaji wakienda pale wanamkuta Mwenyekiti wa Serikali hajui chochote, anaona tu Wazungu wanaeleaelea au Wahindi au mtu yeyote, anaeleaelea, mtu ambaye si mwenyeji wa eneo lile, akiulizwa anasema mimi nimezungumza na watu wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, namna hii inaleta unyanyasaji kwa wale wenye ardhi. Ni dhahiri ardhi ni mali ya wananchi hata kama uwekezaji ni kwa faida ya Taifa lakini pia na wenyewe wanaokaa pale waufahamu mradi ule, wauenzi na wawe walinzi wa mradi ule. Mtaweka uwekezaji kama wananchi wa pale hawaufahamu na kama hawaupendi watakuwa wahujumu wa mradi ule. Sasa kwa nini tuwe na matabaka? Uwekezaji tunaukubali lakini wananchi wawe na heshima yao katika eneo ambalo limewekewa huo uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kuna utaratibu wa Serikali kuweka Maofisa Waandamizi katika Balozi, ulikuwepo na ulifanya kazi nzuri kwa mfano Ofisi ya Ujerumani kulikuwa na Maofisa Waambata wa Utalii, walisaidia sana katika Balozi hizi angalau kuzungumzia mambo ya utalii. Sasa naona ni vema tukautazama utaratibu huu kama utakuwa unaleta faida, nafikiri utaleta faida kwa sababu kama uliweza wakati ule kwa nini kipindi hiki cha utalii, ambapo mwamko umekuwa mkubwa usiweze kufanikiwa? Jaribuni kutazama, wataalam tunao na nina uhakika uwezo tunao, tunaweza tukaweka Watendaji wa Ubalozi lakini na huyu akawa mmoja wa Watendaji wa Ubalozi akashughulikia zaidi utalii ili nchi yetu iweze kufaidika. Huu ni ubunifu mzuri Serikali iliutumia na ninaomba uendelezwe kama itawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu ninaomba Sheria hii mpya, sehemu ya uendeshaji, ipo kwenye sehemu ya tano, Kifungu cha 24, kuhusu madaraka ya bodi ya kuweza kuona uendeshaji wa utalii kama anayemiliki uendeshaji huo ana sifa au hana sifa na kama ana makosa waweze kumsimamisha. Lakini nafikiri ingeenda sambamba na Sheria ya Uwekezaji hapa nchini *TIC*, kwa sababu mkitazama tu ni dhahiri mwekezaji

huyu ameingia lakini anaweza akawa na matatizo mbalimbali na mnataka kumsitisha lakini ameingia pia kupitia Sheria hii ya Uwekezaji. Sasa isije kuwa Sheria mbili zikagongana huyu wamempa nafasi kupitia *TIC* na utalii pia nao wamepewa nafasi lakini anapoondolewa tusimshirikishe *TIC*. Nafikiri hatutakuwa tumeitendea haki Sheria ya Uwekezaji. Naomba washiriki pamoja ili kusitokee hitilafu, wakagongana wenyewe kwa wenyewe kwa sababu Serikali ni moja na utendaji ni wetu wote kwa ajili ya ufanisi wa utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba tu mambo ya kuhodhi ardhi nayo pia niyazungumzie. Mwindaji au mwenye hoteli, kama wenzangu walivyozungumza, anapewa eneo kubwa kweli kiasi ambacho wananchi wanaweza wakaondoka isiwasaidie wananchi waliopo pembezoni pale lakini huyu mmoja anaweza asilifanyie kazi vizuri akahodhi, ana vyeti vyote akakaa miaka miwili, mitatu hakuna faida ambayo inaonekana. Sasa ni vema wapewe kiasi ili kwanza tuwe na wawekezaji wengi lakini pia kuweza kudhibiti maeneo hayo na kuyafanyia kazi vizuri maeneo yale. Kwa kweli kwa kumpa mtu mmoja inaonekana kwamba inaleta hisia mbovu kwa Serikali. Wale wawekezaji, wengi wana maeneo ya uwindaji, wana maeneo ya utalii lakini kwa kweli faida inakuwa ni ndogo kwa sababu kazi haiendi kwa kasi na kwa ufanisi kama vile angepewa eneo la kuweza kulimiliki mwenyewe na kuliendesha vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana mfanye utafiti huo na mfanye mawasiliano mazuri na hao wawekezaji. Tunajua wengine wana uwezo wa kumiliki maeneo makubwa lakini baadaye anasema kwamba ili mradi nimemiliki lile eneo kubwa basi nitafanya wakati wowote muafaka kwangu lakini inakuwa ni hasara kwetu sisi, ni hasara kwa hawa wananchi ambao wako pale kwa sababu wameondolewa katika eneo lao ambalo walikuwa wanalipenda lakini wakati huo huo hawaoni faida kwa manufaa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ninaomba uwekezaji huu uangalie na mazingira. Kwa kweli nchi yetu inaharibu mazingira. Kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja kazungumza kuhusu *North* Mara**,** tuwekeze lakini tuangalie sana mazingira yetu. Sasa hivi wananchi tunawatoa katika maeneo yao ambayo wanalima tunawaambia hapana msitu unaharibika lakini hawa tunawapa nafasi katika sehemu ambazo tungeweza kuhifadhi mazingira yetu, sasa tutazame fedha na kuharibu mazingira, fedha fedheha mazingira haya tunayahitaji kwa vizazi vijavyo. Sasa ikiwa tutakuwa tunawapa wanaharibu mazingira kwa sababu ya fedha ambayo tunaitaka kwa mara moja lakini ardhi ile inakaa na kudumu vizazi na vizazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba sana suala la uhifadhi wa mazingira liwe na nafasi yake. Wanapopewa maeneo haya, wananchi wanalalamika sana wakiona kwamba wao wakazi wa pale wanaondolewa kwamba wanaharibu vyanzo vya maji, wanaharibu misitu na kusababisha mvua hazinyeshi, maji hayaonekani na kupelekwa katika maeneo ambapo hata mito haina maji kwa sababu ya uwekezaji. Sasa hawa wenyeji tunawaambia waboreshe hayo mazingira lakini wawekezaji tunawapa eneo lote bila kujali kwamba watadhibiti namna gani mazingira yale ili yawe mazuri ili ardhi yetu ibaki kuwa nzuri na tupate vyanzo vya maji ili wananchi wasihadhirike na uhaba wa maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo tu ya kusaidia. Naomba katika majumuisho yao wayaangalie na kutoa majibu ya kuweza kuwaridhisha wananchi wetu pamoja na uwekezaji ambao tunaunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Riziki Lulida na Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninapenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hoja hii ni faraja sana hasa kwa Mikoa ya Kusini ambayo kwa muda mrefu miundombinu ilikuwa mibaya, barabara zilikuwa mbaya lakini sasa hivi tunategemea mambo yatakuwa mazuri kwa sababu barabara ya Dar es Salaam kwenda Mtwara inapitika mpaka Mozambique na Afrika Kusini. Kwa kweli suala la utalii litaleta mvuto mkubwa katika Mikoa ya Kusini kutokana na kwamba ni wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa juhudi kubwa inayofanya katika kutangaza utalii hasa kwa kupitia *CNN*. Sasa hivi ni wakati muafaka Wizara itangaze kupitia *Al-Jazeera*, mtandao ambao una ukweli na unaangaliwa na watu wengi, utaleta ufanisi wa aina yake. Utalii utangazwe katika mashirika kama Sauti ya Ujerumani, Uingereza *BBC* na mashirika mengine ya utangazaji ili tupate watalii wengi ambao wataweza kuja katika nchi yetu na kuona vivutio vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuchangia upande wa fukwe za bahari ambazo sasa hivi wimbi kubwa la wageni hupita kwa siri na kunyatia hizo fukwe na matokeo yake tutajikuta zile fukwe wanakaa wageni sisi tunaenda kukaa juu ya milima na zinakuwa hazina manufaa kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ninazungumza hivyo? Sasa hivi Kilwa, Lindi, Mikindani, Mtwara kwa kweli tuna fukwe nzuri sana na wenzetu wamezijua kama zile ni fukwe nzuri wanazinyemelea kwa kupitia wanakijiji na wale wanakijiji hawana elimu ya kutosha kujua nini maana ya fukwe zao na pia wanavyozichukua hawashirikishi wanakijiji kujiona kama wao wana ardhi yao inabidi wawekezaji waje wawekeze kwa wanakijiji, wanawarubuni na wananunua fukwe zile kwa bei za chini matokeo yake baada ya miaka michache itakuwa kama nchi ya jirani utashindwa hata kwenda kuvua katika fukwe kwa vile zimezuiwa na wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali iangalie kwa makini suala la ubora wa fukwe zetu wasiangalie sana Ngorongoro kwa sababu kule kumeshafika mahali pazuri. *Beach* hizi zinaachwa ovyoovyo, hazina maendeleo, matokeo yake watu wanazigawa kirahisi tu kutokana na hela ndogo ambazo wanadanganywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kumejitokeza tatizo la Viwanja vya Ndege kutokuwa na ulinzi wa kutosha. Nina uzoefu kuwa ukipanda *Precision Air* utakaguliwa, ukipanda *Air Tanzania* utakaguliwa lakini hizi ndege za kukodi sijaona wale wanaochukua ndege za kukodi wakikaguliwa, hii inaleta ubabaishaji na njia za panya za kutoresha baadhi ya rasilimali zetu. Ndege inafika haikaguliwi, matokeo yake wanaweza wakachukua nyara zetu bila sisi wenyewe kujua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna *tendency* ya kuwa na imani kuwa wenzetu Wazungu waaminifu lakini kuna wababaishaji ndani yake. Hivyo tuwe tayari kuhakikisha kuna ulinzi katika viwanja vyetu vidogo vidogo kama vile vya Kilwa, Mtwara, Masasi, Nachingwea na wakaguliwe kama wanavyokaguliwa abiria wengine ili wajue ndani ya mizigo yao kuna nini ili kuleta usalama katika Viwanja vyetu vya Ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia upande wa uwekezaji katika mahoteli. Baadhi ya wawekezaji wanahodhi hizi hoteli lakini hazina ubora wa kutosha. Inasikitisha kuona mtu anahodhi hoteli kwa bei kubwa, shuka imepasuka, taulo limepasuka, ni uwekezaji wa aina gani huu ambao unaudhalilisha nchi. Anapangisha bei kubwa anachoangalia zaidi ni mapato yake lakini haangalii ubora wa ile hoteli na wanaokuja kuzikalia zile hoteli ni watu wanaotoka nchi mbalimbali wanategemea kupata ubora mkubwa wa lakini kuna hoteli zingine zinasikitisha. Ningeomba Wizara iziangalie hizo hoteli na kuzifanyia ukaguzi wa kila mara ili aibu hii ituondoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuja kwenye suala la *tour guides*. Kwa kweli imefikia wakati muafaka sasa tuwe na uzalendo na tuangalie hawa ma-*tour guides* wetu kwa kazi nzito wanayofanya ya kubeba mizigo. Leo huwezi kumpeleka mtu Kilwa, Njinjo ukasema unataka *tour guides* atoke Uingereza au atoke China! Wamatumbi wana uzoefu, anajua nikitoka hapa ninatokea mpaka Ulanga kwa kupitia njia zetu za asili lakini hao wengine wanakuja hapa kwa ajili ya faida zao binafsi. Tutumie nafasi hii muafaka kuhakikisha kwamba *tour guides* inaendeshwa na wazawa ili nao wapate ajira na hii itatuondolea umaskini kwa Watanzania ambao wamekaa muda mrefu vijijini hawana kazi za kufanya lakini kazi za kuwasindikiza wageni wanaziweza kwenda katika mapori kwa shughuli za uwindaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni masikitiko makubwa kuona anatoka mtu China kuja kufanya *tour guides* Dar es Salaam au anaenda kukaa Lindi kuwapeleka watalii porini, hii haiwezekani kabisa tutafute njia muafaka kuhakikisha kwamba hawa watu wanawaachia wenyewe wazawa wafanye kazi hizi ili wapate ajira isiwe sasa hivi inakuwa ni soko la wageni kuja kupata ajira Tanzania kwa sababu na sisi vile vile tukienda kwao hatuwezi kupewa nafasi kama hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru sana kama suala hili litaangaliwa na ninashukuru hii *Bill* imekuja kwa wakati muafaka na naomba ikubalike ili na Watanzania wafaidike kwa kushirikishwa katika rasilimali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ninashukuru sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Muswada huu. Mimi pia siko mbali na wenzangu ambao wameipongeza Wizara kwa kuleta Muswada huu. Ninaipongeza na pia umefika wakati muafaka, ambao sisi wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara tuko kwenye harakati hizo na isitoshe tuna utalii wa nchi kavu pamoja na wa baharini. Hivyo vyote sisi wa Mkoa wa Lindi na Wilaya zake, vinatuhusu haswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wameshazungumza ya kutosha lakini mimi nitazungumzia masuala machache tu. Kwanza, ninapenda kuomba Wizara iweke mfuko maalum ambao utasaidia wananchi wazalendo ili na wenyewe waingie kwenye biashara hii ya utalii. Wananchi hawa wengi hawapati mikopo kwenye maeneo mengine, mfano benki utaratibu wake mgumu, lakini kukiwepo na mfuko maalum kwenye eneo hili, utawasaidia na wenyewe kuingia kwenye biashara hiyo badala ya biashara hii kuendelezwa pengine na wawekezaji kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ninasoma Muswada huu sikuona kipengele ambacho kinawalinda wananchi wale ambao wananyanyaswa kwenye maeneo yao. Nitachukulia mfano wa kwenye hoteli. Wale waliojenga hoteli kwenye fukwe wanafikiria pia bahari ni ya kwao, mvuvi anapoenda kuvua kwenye eneo lile ambalo linatazama hoteli yake anamwagiwa samaki au anawekewa vizingiti mbalimbali ili asivue kwenye eneo lile wakati eneo lile ni la wananchi, bahari siyo ya mwekezaji mwekezaji ana hoteli tu. Ninaomba kipengele hicho kiwekwe kwenye Muswada huu kwa sababu sikukiona kipengele ambacho kinawalinda wananchi kwenye maeneo yao ambayo wanafanya shughuli za kujiongezea kipato ili waweze kukidhi mahitaji yao ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninapenda kuiomba Wizara, kuna wananchi ambao wanaishi Kilwa Kisiwani kwenye magofu ya Kilwa Kisiwani ambayo yanaleta watalii kwa wingi. Wameishi pale kwa muda mrefu na wao ndio walinzi wa eneo lile lakini wananchi hao wamekuwa wakilalamika muda mrefu wakiomba na wenyewe pia wapate kipato walau kidogo ili waweze kukipa mapato kijiji lakini mpaka leo hii wananchi hawa hawajapata jibu la kueleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningeomba hawa Wananchi wafikiriwe kwa sababu yale magofu ya Kilwa Kisiwani na kipato chote ambacho kinaingia Wizarani kinasababisha na wao kulinda yale maeneo na kuyaangali kwa uangalifu, kwa hiyo hilo ni ombi ambalo ninalitoa wafikiriwe hawa Wananchi kwa kuwa ndio walinzi wa mali zile na hadi sasa hivi zinatumika kama utalii na kuongezea kipato Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sina lingine la kuongeza isipokuwa tu nina wazo lingine ambalo ninaomba Wizara pia inisaidie. Pamoja na kwamba wanyama wa msituni ndio wanaoleta utalii hapa kwetu lakini kwetu pia kumekuwa na wanyama wengi kama tembo, simba ambao imekuwa ni kero kwa wananchi. Wananchi hawawezi kuwaua hao

wanyama kwa sababu si Sheria kuua wanyama ovyo. Lakini vile vile imekuwa ni adha kwao wanapolima, robo tatu ya mazao inaliwa na wanyama hawa. Halmashauri pia hazina uwezo wa kuwa na hawa Askari wa Wanyamapori ambao wangeweza kuwasaidia ili kuepusha ile adha ili wananchi wapate mazao yao kikamilifu. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara pia iliangalie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wananchi wa Njinjo ambao wanalima lakini robo tu ya mavuno yao inaharibiwa au pengine wasivune kitu chochote, mimea yao inaliwa na wanyama. Ndio, utalii na wanyama pia ni wetu lakini naomba Wizara iwasaidie wananchi hawa ili waweze kupata mazao yao kama wanavyopata maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hapo, sina maelezo zaidi lakini naomba Muswada huo uangaliwe kama nilivyosema kiwekwe kipengele cha kuwalinda wananchi ili wasinyanyaswe kwenye maeneo yao wanapotafuta kipato chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa nitamuita Mheshimiwa Herbert J. Mntangi na Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga ajiandae na Mheshimiwa Fuya G. Kimbita pia ajiandae.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu ambao kwangu mimi nauona ni muhimu sana kwa Taifa letu.

Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya katika Wizara hii akishirikiana vizuri na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Vilevile niwapongeze sana Watendaji wote ambao kwa kweli wanafanya kazi nzuri na lazima niseme na nikiri kwamba ni moja kati ya Wizara katika sekta hii ambayo inajali sana jinsia ukianzia kwa Mheshimiwa Naibu Waziri ni Mama yaani ni jinsia hiyo. Lakini ukienda kwa Katibu Mkuu, ndugu yangu Mama Nyoni, ni mama vilevile. Ukichepuka katika sekta yenyewe ya utalii, utamkuta Mkurugenzi pale, Mama Mmari, Msaidizi wake Mama Kiangi na Watendaji katika sekta ile ya Leseni, kina mama wamesheheni. Nawapongeza sana. Lakini naomba nisimsahau ndugu yangu na Mwalimu wangu, ndugu Peter Mwenguo, ambaye naye yuko kule, yeye ni Mwalimu wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kutuelezea jambo kubwa ambalo sisi wote tunalikumbuka ametuambia kwamba utalii ni nguzo ya uchumi wa dunia, mimi nakubaliana naye sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ametueleza vilevile kwamba utalii katika nchi yetu unachangia katika pato la Taifa kutoka 13% mwaka 2000 hadi kufikia 17.2% mwaka

2005. Kwa asilimia kiasi hicho kwenye pato la Taifa siyo kiwango kidogo bali ni kiwango kikubwa lakini nasema sekta hii bado inayo nafasi ya kuweza kuongeza mchango wake katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupata ongezeko hili, yametokea mambo makubwa yafuatayo:-

Kwanza, idadi ya watalii imeongezeka lakini vilevile nyenzo za kufanyia kazi kwa mfano hoteli, magari yanayohudumia watalii, vyombo mbalimbali ambavyo vinahudumia watalii na hata wafanyakazi ambao wanahudumia watalii wameongezeka, hii imesaidia sana kuboresha uchumi wa Taifa letu. Lakini ni vizuri tukasaidia sekta hii ili iweze kuboresha maeneo ambayo tayari yamekwishaanza kufanyiwa kazi.

Jambo moja ambalo ni vema tukaliangalia ambalo pia litasaidia sekta ya utalii kuongeza mapato ni kuangalia uwezekano wa kuzi–*grade* yaani kuweka ngazi katika hoteli zetu na tuweke ngazi kwa kufuata hali halisi ya ubora wa hoteli. Ukichukulia mfano wa hoteli zinazojiita *Five Star Hotel* basi *Five Star Hotel* itakayokuwepo Tanzania aidha Dar es Salaam au Mwanza au Arusha ikipata daraja hilo la *Five Star Hotel* ifanane na *Five Star Hotel* za Kimataifa mahali pengine popote duniani. Itakuwa aibu mtalii anatoka katika hoteli ya *Five Star* kule Marekani au Amsterdam anakuja Tanzania, anaingia katika *Five Star Hotel* ya Dar es Salaam anaona ni vichekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Wizara ifanye *grading* ya hoteli hizi lakini wawekezaji wetu wa nje na hata wa ndani waeleze ni vigezo gani vinavyoweza vikafanya hoteli ikatambulika kuwa ni *Five Star Hotel* ili wanaojenga hoteli wajue vigezo hivyo na watamani hoteli zao ziwe na vigezo vinavyoweza kuwafanya kweli wakawa na hoteli zinazoitwa *Five Star*. Bila vigezo hivi kuwekwa wazi kwa wawekezaji tunaweza tukawa na utitiri wa hoteli lakini zisizofikia viwango tunavyovitaka ambavyo watalii wengi wanavitamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili utalii uweze kuendelea kuwa nguzo ya uchumi basi tunaitarajia sekta hii ya utalii iweze kuwa na mapato yatakayoiwezesha sekta yenyewe kujiendesha kwa kujitegemea lakini vilevile kuwa na pato la ziada litakaloweza kwenda kuchangia katika Mfuko wa Taifa kuboresha mahitaji mengine ya Kitaifa. Ili iweze kuwa na uwezo huo, moja ambalo nimelisema litasaidia ni kuweka ngazi mbalimbali za hoteli.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yapo mambo mengine mengi ambayo yanaweza yakasaidia kwa kuangalia upya viwango vyetu vya leseni yaani ada za leseni. Viwango tulivyokuwa navyo awali vimeboreshwa kidogo lakini bado viwango viko chini sana, ukitazama hakuna tofauti kati ya hoteli ambayo mimi naiona ni ndogo ukiilinganisha na hoteli kubwa kwa mfano hoteli ile tunayoiita Kilimanjaro Hoteli au hoteli nyingine kubwa lakini kiwango cha leseni kati ya hoteli hizi ambazo hata kwa macho zinaonekana kuwa ni tofauti sana lakini ada zake ni sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kufanya *grading* au kuweka madaraja ya hoteli vilevile tuangalie uwezekano wa kuwa na ada za leseni kwa viwango

vitakavyofanana na madaraja tutakayokuwa tunayaweka. Hii itasaidia kuboresha mapato katika sekta hii. Hoteli nyingi kubwa zina uwezo wa kulipa viwango vikubwa zaidi kuliko hoteli za kati na ndogo ambazo kwa sasa wanalipa kiwango kinachofanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo naliona ni muhimu sana, ni kuboresha ukaguzi katika vyombo vya utalii. Bado wapo *Tour Operators* ambao wanafanya kazi bila kuwa na leseni na wanafanikiwa wakati wengine wanakuwa na leseni, tatizo ni nini? Tatizo ni kwamba hatujaimarisha ukaguzi. Kwa hiyo, watu wanaweza wakafanya kazi hizo bila kuonekana lakini wanafahamika na wanaweza wakachukua watalii na wakatoa huduma bila kuwa na leseni. Nashauri tuimarishe ukaguzi wa vyombo ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo matatizo mengi ambayo yanaikabili sekta hii ya utalii na kama tunataka kuboresha mapato basi tuangalie makosa ambayo tumekwishayafanya. Kwa mfano, tumediriki kuwaruhusu watu kutoka nje ya nchi kuhamisha ndege wetu na wanyama wetu na kuwapeleka katika nchi za nje ambako huko wamekwenda kuanzisha vituo vyao vya utalii, matokeo ni nini? Kama unahitaji kumuangalia simba, sasa huhitaji kwenda Ngorongoro wala Serengeti, utamkuta simba yupo katika maeneo mapya yaliyoanzishwa katika nchi ambazo simba hawapo kabisa. Lakini ni Watanzania wenyewe, Wakenya pengine na wenzetu wengine ambao tuna maeneo yenye wanyama hao, tumeruhusu wamewachukua simba, wamekwenda kuanzisha maeneo ya utalii na wanatengeneza fedha badala watalii wale kuja kuwatafuta simba Tanzania sasa wanakwenda kuwaona simba hukohuko na wenyewe wanatengeneza fedha kwa kiwango ambacho wala hatuwezi kukikadiria. Hayo yalikuwa makosa makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumewaruhusu watalii na wawekezaji wengine wanaingia katika mbuga zetu za wanyama na kamera na vifaa vikubwa vya kisasa kabisa, wanachukua picha na wanatengeneza filamu na wanakwenda kuziweka katika maabara yao kule wanavutia watalii wengi wanatazama filamu zile wanaona wanyama wetu, wanaona sehemu zetu ambazo kwa kweli wasingeweza kuziona na wanatengeneza fedha ambazo sisi hatuna mapato yoyote. Tumekuwa wepesi sana wa kutokuwa na Sheria za kubana watu wasihamishe yale mambo ambayo tunadhani ni muhimu sana kwetu, ndiyo vivutio, sasa tunawapa nafasi watu kuja kuyachota na kwenda kuyaweka kwao kule ambako vivutio vya namna hiyo havipo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo linaboresha utalii ni usalama wa watalii wenyewe. Hivi sasa kumetokea vurugu katika nchi jirani, matokeo yake watalii wengi wamesitisha safari zao. Kwa hiyo, usalama ni muhimu sana kuwezesha watalii kuongezeka. Vita ni adui wa utalii lakini wizi na ujambazi ni adui mkubwa wa sekta ya utalii, matusi, udanganyifu na huduma mbovu ni mambo ambayo yanaathiri sana utalii na kukua kwa sekta ya utalii. Tutafanya nini katika kuboresha hali hii? Sisi kama Watanzania tupiganie sana na kuomba amani iendelee ili watalii waweze kuamini nchi hii kwamba ina usalama lakini ujambazi na wizi lazima tuvipige vita ili tusiwaache watalii wakaingiliwa na majambazi na wezi, wakaogopa kuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika siku za hivi karibuni, ametokea Dereva mmoja wa *tax* kule Dar es Salaam na maeneo mengine, mtalii alisahau vifaa vyake katika gari lake, alifanya ujasiri mkubwa sana akahakikisha amevihifadhi na kuvikabidhi na akapewa tuzo. Narudia tena, mimi nampongeza sana mtu kama yule, ni mfano mzuri sana. Sasa tunapenda na wahudumu wanaotoa huduma za utalii nao waige mfano wa mwenzetu yule alivyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji wengi wanaotoa huduma za utalii bado hawatoi takwimu zilizokuwa sahihi. Ukiwauliza kwa hiari wakwambie wamehudumia watalii wangapi watakwambia kiasi ambacho utashangaa hivi kweli mtu huyu mwenye magari kumi au ishirini anasema amehudumia watalii kumi tu ni dhahiri kwamba takwimu tunazopewa siyo sahihi. Hebu tujaribu kuweka vifungu ndani ya Sheria vitakavyowabana watakaokuwa wanatoa takwimu ambazo si sahihi ili tuweze kuboresha takwimu zetu. Nina uhakika Mheshimiwa Waziri anapozungumzia pato la Taifa limeongezeka kwa 17.2% mwaka 2005 ni kutokana na takwimu ambazo amezipata kutoka kwa *Tour Operators* hawa na wengine wote. Kama takwimu hizo anazopewa si sahihi Mheshimiwa Waziri au Wizara maana yake hapa tunazungumzia kitu ambacho kwa kweli hakina usahihi, nina uhakika kabisa kuna kasoro kubwa katika utoaji wa takwimu, tuimarishe Sheria ili tuweze kuboresha takwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo cha Utalii. Waheshimiwa Wabunge wamezungumza sana hapa kwamba tuna matatizo ya watendaji tujitahidi hicho chuo ambacho tumeshasikia kitajengwa na kwamba kitakuwa chuo kikubwa sana katika Bara la Afrika basi tujitahidi, tuchukue hatua kukiwezesha chuo hicho kujengwa haraka kwa kadri itakavyowekezana ili watu wetu waweze kupata elimu. Ninaomba katika ufundishaji hata hao wanaosimamia watu wanaopanda milima, hawa *Tour Operators* basi wafundishwe angalau lugha tatu muhimu, tuanze na tatu yaani wajue Kingereza, Kifaransa na angalau wajue pia Kijerumani na baadaye tutaangalia jinsi lugha za Mataifa mengine wanaokuja ambao hawatumii lugha hizo tatu nilizozitaja kama vile Kichina na Kijapani na baadaye nao tuwaingize yaani watu wajifunze lugha hizo. Lugha ni muhimu sana kwa sababu mimi nimeshawahi kuwasikia watu wanaowahudumia watalii, wanazungumza Kingereza ambacho hajui basi anabuni maneno ya ajabuajabu wakati mwingine wala siyo maneno mazuri, sitapenda kuyasema hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara hiyo kwa kuwa wabunifu. Leo tunazungumzia Sheria mpya ya Utalii ya mwaka 2008, ni ubunifu unaotokana na kuunganisha Sheria mbili zilizokuwepo ambazo naamini zimepitwa na wakati, Sheria ya Hoteli na Sheria ya Wakala wa Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamuita Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga na Mheshimiwa Fuya G. Kimbita ajiandae.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kwa kunipa fursa ya kuchangia.

Pili nimpongeze Waziri, Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara kwa kuleta Muswada huu muhimu kwa uchumi wetu.

Tatu niendelee kutoa mapendekezo na maoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, utalii ni njia mojawapo ambayo inaiwezesha nchi yetu kukuza uuzaji wa bidhaa zake nje ya nchi na katika suala hili tunazungumzia uuzaji wa huduma yaani *Export of Services*. Ili huduma hizi ziweze kuuzwa vizuri, hatuna budi kuitambua kwanza sekta ya utaliii haisimami peke yake, ni sekta ambayo ina maingiliano makubwa sana na sekta nyingi katika uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, nataka nisisitize kwamba kwa mfano hata kama watalii watakuja milioni moja kama ambavyo *statistics* au takwimu alizotupa Mheshimiwa Waziri zinavyoonyesha, idadi ya watalii tu kuongezeka peke yake haisaidii, kinachotakiwa hapa ni kuwa na uhakika kwamba watalii hawa milioni moja watakapokuja Tanzania, kwa kiasi gani watatumia pesa zao hapa nchini na pesa hizo zitabaki hapa nchini? Kwa hiyo, la msingi hapa ni mapato yanayotokana na hawa watalii milioni moja au lakini nane *"whatever the figure"* wanatumiaje pesa zao hapa nchini. Hapo ndipo yanapokuja maingiliano ya sekta mbalimbali ndani ya uchumi. Ikiwa watalii wetu watakaa kwenye hoteli ambazo takribani robo tatu ya vyakula na vinywaji wanavyotumia kwa maana ya vinywaji vyao vinatoka nje, vyakula vyao vinatoka nje na mambo mengine mengi yatatoka nje basi utalii huo hautusaidii kwa sababu pesa ambazo tungezipata sisi zinakwenda nje. Kuna haja ya kuhakikisha kwamba vyakula, vinywaji na bidhaa nyingine muhimu ambazo zinatumiwa na watalii zinapatikana hapahapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaliii wetu ili uweze kuwa mzuri zaidi miongoni mwa mambo yanayoweza kutusaidia ni kuwa na Shirika la Ndege linaloweza kutoa huduma ya kuwaleta na kuwarudisha wanakotoka. Ikiwa watalii wetu wataendelea kutumia *British Airways, Air France, Scandnavia Airline, Swiss Air* na kadhalika bado pato la watalii ambalo tunalitarajia lije hapa nchini litakuwa linakwenda nje. Kuna haja ya kutengeneza *air line* yetu iwe ni *air line* ambayo itasaidia kukuza utalii wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *marketing*. Tunazungumza mambo mengi hapa kuhusu utalii lakini utalii ni bidhaa na bidhaa inataka kutangazwa. Hawa watu hawawezi kuja tu kwa sababu Tanzania kuna Kilimanjaro, hapana! Kama ni Kilimanjaro tayari kuna matangazo mengine hapa duniani yanasema njoo nchi fulani utaona Mlima Kilimanjaro, kwa hiyo huna haja ya kuja Tanzania kuuona Mlima Kilimanjaro, kama vile unaweza kuupanda Mlima Kilimanjaro ukienda kwenye nchi nyingine. Kwa hiyo, suala la utangazaji yaani *marketing* ni suala la msingi sana na mimi nilitarajia Sheria hii ingetuonyesha dhahiri tumejipangaje katika *marketing* ya utalii wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tunazungumzia juu ya Balozi zetu kushughulikia E*conomic Diplomacy*. *Economic Diplomacy* ndiyo msamiati wa sasa. Ni kwa kiasi gani tunazitumia Balozi zetu kukuza utalii? Unapotembelea kwenye nchi ambazo ndiyo kwenye masoko ya utalii huoni kama hizo Balozi zetu zina wataalamu wa kutosha kuiuza Tanzania. Kwa hiyo, hili ni jambo la msingi na ni lazima tulizingatie, tuliwekee utaratibu mzuri ili tuweze kukuza utalii wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Shirika linaloitwa *TTB*. *TTB* ndiyo wamepewa mamlaka ya kuitangaza nchi. Nadhani Sheria hii ingetusaidia vizuri kama tungetengeneza kitu kinachoitwa *Tourist Marketing Facilitation Committee* ambayo itaisaidiana na *TTB* katika kuitangaza nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya *grading* ya *facilities* zetu katika Sheria tunayoizungumza katika *section 6(c)*, inampa jukumu hili *Director* wa *Tourism*. *Director* wa *Tourism* ni Mtendaji wa Serikali na shughuli zake ni za Kiserikali zaidi na urasimu wa Kiserikali tunaufahamu. Kuna haja ya kutengeneza kitu kwa jina la *Tourist Grading Council* ambayo itamsaidia utaalamu *Director* wa *Tourism* katika ku-*grade* hoteli katika misingi ambayo Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, amesisitiza sana umuhimu wa ku-*grade* hizi hoteli katika *level* s za Kimataifa siyo katika *level* za Kitanzania, hapana, iwe ni *levels* za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *section 20* ya Muswada tunaoujadili inazungumzia juu ya *appeal*. *Section* ya 51 nayo inazungumzia juu ya appeal kwa mtu ambaye atakuwa amekosewa au ameonewa chini ya Muswada huu. Ushauri wangu ni kwamba *Section* hizi mbili ziunganishwe tuwe na Appeal *Board* moja tu, hakuna haja ya kuwa na *bodies* mbili ndani ya Wizara moja zinazofanya kitu kimoja *"appeals"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Part III*, *Section 42*, ukiisoma hii pamoja na *Section* 58(2), nadhani *Section* hizi mbili zinahitaji kuunganishwa kwa sababu zote zinazungumzia ku-*reserve* maeneo ya shughuli za kitalii kwa Watanzania. Hakuna haja ya kuwa na *Section* mbili tofauti ambazo zote zinazungumzia ku-*reserve* maeneo ya shughuli za Watanzania katika *area* hii ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika maeneo haya ambayo tunasema ndiyo yawe ya Watanzania, naipongeza Serikali na ninaipongeza pia Wizara kwa kuja na pendekezo hili. Lakini nilikuwa natazama eneo kama *la car rental* ambalo nalo linasemekana au limependekezwa liwe la Watanzania peke yake, kwa uelewa wangu mdogo wa shughuli za Kimataifa za *car rental* yapo makampuni duniani ambayo yanafahamika kwa *car rental* kwa mfano HERTS na *AVIS*, hizi ni *International Firms* za *car rentals*, mtalii anayetaka kuja Tanzania anaifahamu HERTS na *AVIS*. Huyu ukimuwekea HERTS Tanzania au *AVIS* Tanzania utampata kwa urahisi sana kwa sababu anakotoka huko ndiyo makampuni ya *car rentals* anayoyaelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mimi ni kwamba turuhusu maeneo kama haya yafanywe kwa *joint ventures* na Watanzania wawemo lakini tukaribishe *foreign experience* kwenye eneo hili la *car rentals* kwa maana ya *international*

*companies* lakini Watanzania wawemo kwa sababu tuna-*deal* na *international clients,* ni vizuri basi tuka-*deal* na *international clients* kwa kutumia uzoefu wanaokuwa nao toka huko wanakotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Section* ya 59 ya Muswada inazungumzia *Tourist Development Levy*. Kwa bahati mbaya, haijaonyeshwa katika Muswada *levy* hii itakuwa ni ya kiasi gani. Angalizo ni kwamba tujitahidi *levy* hii isiwe kubwa kwa maana ya kuwa *prohibitive* kwa sababu mwisho wa siku kiwango cha *levy* hii kitajitokeza kwenye bei au gharama ambayo mtalii itabidi alipe ama katika chumba cha hoteli au katika chakula au vinywaji atakavyonunua na sisi tunafahamu kwamba vyote hivi tayari vina kodi juu yake. Kwa hiyo, tukileta *levy* maana yake tutapandisha gharama na mwisho wa siku tunaweza kujikuta tunakuwa *uncompetitive*. Kwa hiyo, ni vizuri *levy* iwepo lakini tuwe *careful* kwa kiasi ambacho tutakipendekeza kwa maana ya *magnitude* isije ikatutoa katika ushindani wa soko hili la kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliza, nataka nisisitize kwamba katika nchi ya jirani na hapa sina haja ya kutokuisema ni Kenya, utalii unachangia pato kubwa sana la fedha za kigeni katika nchi hiyo. Vivutio walivyonavyo Kenya ukilinganisha na vile vya Tanzania sisi tuna vivutio vingi zaidi kuliko Kenya, suala la msingi hapa ni kwamba kwa nini sisi hatupati fedha nyingi za kigeni katika sekta hii ya utalii kama wanavyopata Kenya?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Wizara na wataalamu wake wachukue nafasi wakajifunze Kenya wanafanya nini? Wanafanyafanyaje mpaka wenzetu wanaweza kupata fedha nyingi zaidi za kigeni katika sekta ya utalii ambayo hawana vivutio vingi kushinda sisi? Hapo ndiyo tutakapoweza kuelewa kwamba tunakosea hapa au pale ili turekebishe hivi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninapenda kuungana na wenzangu waliosisitiza juu ya hoja ya kwamba utalii wetu umejikita sana kaskazini ya Tanzania. Tunapozungumzia utalii ni kaskazini tu. Kwa nini tusifungue na maeneo mengine? Tunafahamu nchi hii ina vivutio vingi sana vya utalii, utalii uko Magharibi kule Lake Tanganyika kuna wale Sokwe ambao hawapatikani duniani isipokuwa kwa jirani yangu Ndugu Peter Serukamba. Mbuga ya Selous ni mbuga kubwa kuliko zote duniani katika masuala ya wanyamapori.

Pale Katikati ukienda Rukwa kuna Mbuga inaiyoitwa Katavi, ina wanyama ambao hawapatikani mahali pengine mpaka yupo na Twiga mweupe achilia mbali Twiga mwenye mabakamabaka, ni twiga mweupe anapatikana Katavi na kuna wanyama wengi sana, lakini tunashindwa kuufikisha utalii kule kwa sababu ya miundombinu yetu mibovu. Ndiyo maana nikasema hii ni sekta ambayo inaingiliana sana na sekta nyingine katika uchumi wetu, huwezi ukaendeleza uchumi au hatuwezi kuendeleza sekta ya utalii *in isolation from the rest of the sectors of this economy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na ninaunga mkono hoja iliyombele yetu, *subject* kwa hayo mapendekezo niliyoyatoa, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Fuya G. Kimbita.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wameshazungumzia mambo mengine ya msingi kabisa, mimi ninaomba nianzie pia kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Naibu wake na watendaji wengine wote kwa kutuletea Muswada huu ambao kwangu mimi nautafsiri ni muhimu na ukombozi wa nchi yetu kwani utalii ndiyo biashara pekee yenye kuhitaji mtaji mdogo ukilinganisha na biashara nyingine lakini na matunda yake kupatikana kwa maana ya kuwanufaisha Watanzania wote kwa maana ya wananchi wote. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wote Wizarani kwa kutuletea Muswada huu ambao ni mzuri sana na muhimu kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu utatuletea maslahi mengi sana kwa nchi yetu kutokana na kipato tutakachokuwa tunakipata kutokana na ongezeko kubwa la utalii, baadhi ya matatizo hata yale madogo madogo sana ndani ya maeneo yetu yatatatuliwa, ndivyo ninavyoamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa kazi kubwa ya utangazaji waliyoifanya. Walituletea hapa, tukapitisha bajeti yao na kweli matokeo ya ule utangazaji sasa wote tunashuhudia. Walitangaza sana kwenye magazeti, majarida mbalimbali na televisheni za nje ambapo matokeo yake tumeyaona ikiwa ni ongezeko kubwa sana la watalii, wenye mahoteli wanakiri kuongezeka kwa pato kutokana na wingi wa watalii wanaokuja hapa nchini, viwanja vyetu vya ndege mapato yameongezeka kutokana na ndege nyingi ambazo zinakuja hapa nchini. Kwa hiyo, nampongeza na naomba tuweke nguvu zaidi katika kuvitangaza vivutio vyetu na twende *strategically* kwenye maeneo ambako tunaona kuna *possibilities* za kupata watalii wanaotaka kuja hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza tuongeze nguvu kubwa katika matangazo ya vivutio vyetu. Nimwombe Mheshimiwa Waziri akakae na watu wake kuangalia uwezekano wa kuanzisha mfuko wa kutangaza utalii wetu. Huu mfuko utatusaidia sana na yale maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanayalalamikia kwamba hayajatangazwa, basi huu mfuko utafanya kazi hizo kwa ufasaha mkubwa sana. Nimtoe wasiwasi ndugu yangu Mheshimiwa Kaboyonga pamoja na wale twiga weupe na wanyama wengine ambao umewasemea, mfuko huu natumaini utasaidia katika kutangaza vivutio kama hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unajibu dukuduku langu la siku nyingi sana la kwamba, hivi haya matunda ya utalii hapa nchini kwetu anayefaidi ni nani? Jibu la siku za nyuma lilikuwa kwamba anayefaidi matunda ya utalii wetu ni watu wengine

ambao sio wa kutoka hapa nchini kwetu, sote tunawafahamu lakini kwa Muswada huu Watanzania sasa tutaanza kufaidi matunda ya utalii wetu. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na watu wake wote kwa kukidhi au kuniletea jibu la dukuduku nililokuwa nalo siku nyingi za nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nashauri, wazalendo tuhusike sana kwenye biashara yetu hii ya utalii. Haya maeneo tunayozungumza Serengeti na kwingineko tunataka kuyagawa, tuwape kipaumbele Watanzania. Watanzania sasa hivi wapo wengi sana wanaoifahamu hii biashara ya utalii na wengine wanakusudia kuingia basi tuwagawie haya maeneo ili wale wageni kutoka nje waje waingie ubia na Watanzania, sio hii ya kuwapa wageni asilimia mia moja kumiliki yale maeneo. Maeneo yale tuyagawe kwa Watanzania wazalendo ili wageni wajapo hapa nchini waweze kuingia ubia na hii itasaidia mambo mengi sana ya kiusalama, kuwepo kwenye bodi zao ili kuhakiki yale mapato kamili yanayotokana na ile biashara wanayoifanya. Mahali pengine sasa hivi ni vigumu sana kuwa na uhakika wa *data* ya kile kipato kinachopatikana kutokana na biashara ya utalii inayofanyika mahali fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine tuwe wazalendo wa kutosha, kuna baadhi ya maeneo ya utalii hapa nchini sasa hivi, baadhi ya Waafrika hatuwezi kuingia mle, zipo sababu mbalimbali zinatolewa lakini hii inakaribisha ubaguzi. Tukiweka Sheria kwamba maeneo yote ya utalii yatakuwa na wazalendo ambapo wageni wakija wataingia ubia kuyaendesha kwa pamoja, hii harufu ya ubaguzi wa rangi itapotea lakini tusipokuwa waangalifu sasa hivi Waheshimiwa wengine wameshazungumza hapa, kuna baadhi ya fukwe, mahoteli wanaweka *rates* za juu sana au saa zingine visababu vya hapa na pale kwa maana nyingine ni kwamba ngozi nyeusi pale hutakiwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba pamoja na kujaliwa vivutio vingi vya utalii, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu pamoja na Watanzania kwa ujumla wetu, hii biashara ya utalii haina ambaye amezaliwa nayo au anayeijua zaidi, ni sisi wenyewe kwa kuanzia na Waheshimiwa Wabunge tukashirikiane na Waheshimiwa Madiwani na wananchi kwa ujumla wake tuweze kuwaelimisha wananchi utalii ni nini. Kuna baadhi ya vivutio tulivyonavyo katika maeneo ya Majimbo yetu ambako mwananchi hatambui kama hiki ni kivutio cha utalii au sisi wenyewe hatutambui, lakini kwa kutembeatembea utaweza kugundua kuna vivutio vingi sana ambavyo tunavyo hatujavitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulibahatika kusafiri katika nchi mojawapo, tulisafiri karibu kilomita 670 kwenda kuona kamti kadogo tu lakini jinsi ile lugha ya kuusifia ule mti ilivyopambwa, mtu unashawishika sana kwenda kuuona. Sasa ni sisi tufanye jitihada kuanzia Waheshimiwa Wabunge hapa tulipo, maana yake niseme wazi hii ya kulalamika kwamba kuna baadhi ya maeneo yanayotangazwa zaidi na mengine hayatangazwi haitasaidia sana, tufanye jitihada sisi sote, kila mmoja kutoka kwenye Jimbo lake kwa kushirikiana na wananchi wake kuvitambua vivutio vya utalii tulivyonavyo na kuvitangaza. Tukishaanzisha na ule mfuko wa utangazaji tutaweza kupeleka hizi taarifa kwenye ule mfuko, vile vivutio vitaanza kutangazwa. Naomba hilo tulizingatie na majibu yake yatakuwa ni ya muda mfupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo utalii wa aina nyingi sana katika maeneo yetu, sote tunafahamu utalii wa wanyamapori, utalii wa wadudu, kupiga picha, hizi za kawaida, picha za filamu, utalii wa mazingira (*eco-tourism*). Utalii wa mazingira ni utalii muhimu sana na ndiyo unaibukia sana sasa hivi duniani. Watafiti wengi wanaupenda na watu wengine wanaupenda kwa *interest* zao binafsi. Upo utalii wa asili *(cultural tourism)*. Tanzania tumejaliwa, ni kisiwa cha amani, wengine wangependa kuja kutembea na kuona hivi Tanzania inavyokuwa na amani namna hii nini kinachosababisha. Kikubwa kinachosababisha ni jinsi tunavyoishi, mila zetu, desturi zetu, nako ni sehemu mojawapo pia ya utalii au kivutio cha utalii ambako wageni wangependa sana kukifahamu. Fukwe zetu, tutangaze utalii wote pamoja na wa fukwe. Fukwe zetu natumaini hatujazitumia vizuri sana. Tunazo fukwe nzuri sana hapa nchini. Wageni wengine wakifika wanashangaa, bahari, maji safi kabisa mpaka mchanga mweupe unauona, kwingine bahari imechafuka sana kwa sababu ya *pollution* mbalimbali lakini hapa nchini tunazo baadhi ya *beach* ambazo ni nzuri, namaanisha fukwe. Kwa hiyo, ninaomba tutilie mkazo maeneo yote hayo. Pia tuna mabonde na milima, Mheshimiwa Laizer hapa amezungumzia vizuri zaidi pia na wananchi baadhi ya makabila tunayo lakini nayo wafaidi pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Watanzania kwa ujumla wetu tuwe *very serious* kwenye hii biashara ya utalii. Ukitembea hata hapa nchi jirani ya Kenya ukikodisha *taxi*, yule dereva *taxi* kukuchukua ulikomkodisha mpaka unapoelekea, atakuwa ameshakuelimisha vitu vingi tu anakuzungumzia vitu mbalimbali, hata nchi nyingine, hapa Tanzania nako ni muhimu hata *taxi drivers* wetu, wangepewa somo ili wanapompakia mtu wa nje au mtu ametoka mkoa huu kwenda mkoa mwingine kumwelimisha kwenye mkoa huu kipo hiki, kipo hiki, kwenye mji huu kuna hiki na hiki, natumaini itatusaidia sana lakini hii yote itakuja kama tutakuwa *serious* kwenye hii biashara ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuanzishe vyuo vya utalii kwa wingi kwa sababu tunaona hivi vilivyopo ni vichache kutokana na sasa hivi huu utalii utakavyokua. Sasa hivi utalii una *boom*, unapaa na ili tuweze kwenda nao lazima tuanzishe vyuo vya utalii.

Pia tuwafundishe hawa *Tour Guides* ambao nampongeza Mheshimiwa Waziri na watu wake wote kwa kuwajali sana hawa ndugu zetu. Wale vijana walikuwa wanabebeshwa kama vile magari ya mizigo lakini kwa kipato kidogo lakini Muswada huu unawalinda. Natumaini kwenye kanuni hata zile *rates* watakazokuwa wanalipwa zinaweza kuwekwa pale angalau kuwalinda na kuwaendeleza zaidi. Kwa hiyo, nawapongeza kwa kuleta katika Muswada huu kipengele cha *Tour Guides* na niongezee hapo hapo, *Tour Guides* kutoka nje naomba iwe ni marufuku, *Tour Guides* wa Kitanzania wanatosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niongelee utalii mkoani kwangu Kilimanjaro. Utalii Mkoani Kilimanjaro upo wa aina nyingi. Tunayo maeneo ya tambarare kule Chemka ndani ya Wilaya yangu ya Hai, maji yanafukuta tu kutoka chini

huko, watu wangependa kuja kuyaona na sisi tumeshaanza kazi hiyo ya kutangaza na bado tunazidi kupaendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika mkoa wangu wa Kilimanjaro ipo ile dhahabu Mwenyezi Mungu aliyoiweka juu ya ardhi, Mlima Kilimanjaro. Dhahabu za wenzetu mpaka uchimbe, sisi huna haja ya kuichimba, macho yako tu ukiamka asubuhi umeiona ile dhahabu. Sasa ninaomba hii dhahabu tuitumie vizuri zaidi kwa kuona jinsi dunia sasa hivi ilivyoutambua hata ule mlima kwamba ni hifadhi ya kidunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tu, zaidi ya wageni 45,560 waliweza kupanda mlima Kilimanjaro. Hayo ni mapato makubwa sana. Sasa tunautumiaje zaidi mlima ule? Kuna haja ya kuongeza njia nyingine mpya za kuupanda ule mlima, si lazima kufika kileleni, kuna kitu wanaita *non summit tourism of Mount Kilimanjaro*, sio lazima kupanda ukafika kileleni, ndani hifadhi ya mlima wenyewe kabla hujafika kileleni kuna mambo mengi muhimu na ya ajabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilizungumza hapa wengine walicheka kidogo, kwamba kuna jani ukiligusa mvua inanyesha si uwongo, karibuni mkaone.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa ujumla, ule Mlima Kilimanjaro bado tuna nafasi kubwa ya kuutumia kwa maana ya nchi kama nchi kupata kipato zaidi lakini pia na kwa maana ya wananchi wa Kilimanjaro kuzidi kufaidika na mlima ule. Tukiongeza hizi njia nyingi mpya, mafanikio yake yapo mengi sana, kile kipato cha wananchi wa Kilimanjaro ambacho kimepungua sana kutokana na kuanguka kwa zao la kahawa basi wale wananchi wa Kilimanjaro nao watafaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie jinsi ya kuongeza njia mpya. Kuna njia mpya ya kutoka Kwasadala, Masamamula, Ng'uni kuelekea maeneo ya Nure, kule kuna vitu vya ajabu, ndiyo hayo mambo ya mimea. Yapo maeneo ambayo tungeweza kuweka vihoteli vidogo hata vya saizi ya kati, tutazidi kupata mapato kama Taifa, hata wananchi wenyewe watazidi kunufaika zaidi. Katika kuupanda huo mlima siyo kufika tu kileleni wapo wanyama wengi, mimea na hapa katika mimea kuna mimea mingine katika ule mlima ambayo pengine duniani haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri, kile kilio cha wananchi wa Kilimanjaro hususan pale Hai, mmekuja kuongeza mipaka ya hifadhi ya Mlima wa Kilimanjaro, wananchi wangu, Waheshimiwa Madiwani wangu, hawajashirikishwa vizuri. Wamekuja wameweka *beacons* zao, wananchi walikasirika kiasi cha kutaka kung'oa zile *beacons*, nikawaomba wasing'oe, tutakuja kuzungumza na ninyi ili tuweze kwenda kuwaelimisha vizuri. Lakini wale wananchi lazima walalamike yale maeneo yanavyoongezwa, Kilimanjaro tuna uhaba mkubwa sana wa ardhi, lakini gawiwo linalotokana na mlima wa Kilimanjaro hatulipati. Wenzetu wa *TANAPA* kupitia *KINAPA* lazima upige magoti sana na unapata huko kiduchu kwa kuteseka. Kwa nini

tusiwe na kiwango rasmi, *percentage* inayotokana na mapato ya Mlima Kilimanjaro kwenda kwenye Halmashauri zinazozunguka ule mlima?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri na ananisikiliza kwa makini sana, namshukuru, hilo suala lifikishwe kwenye taratibu zinazohusika. Sisi kule Halmashauri tumeshamaliza, Mkoani tumeshamaliza, ni Wizara kwa maana ya ujumla wa Serikali kuweka kiwango kamili. Wenzetu wa wanyamapori wanapata asilimia ishirini na tano. Ndugu yangu Msindai amependekeza asilimia kumi, mimi ninapendekeza asilimia kumi na tano kutokana na kuanguka sana kwa lile zao la kahawa ambalo ndilo lilikuwa linatusaidia. Zao la kahawa liliendesha uchumi wa nchi hii kwa miaka mingi, tusiwasahau wale wananchi wa Kilimanjaro, tuwasaidie kupitia huo Mlima wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, hicho kilio changu nilikuwa nikizungumza binafsi na Mheshimiwa Waziri, sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri tukimaliza tuongozane twende kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Awali ya yote, naomba ni-*quote* kidogo madhumuni ya Muswada kama alivyosema Mheshimiwa Waziri. Amesema: “Lengo letu ni kuongeza mchango wa sekta katika uchumi wa Taifa, kuongeza ushiriki wa Watanzania katika sekta hii ili kupunguza umaskini pamoja na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa katika sekta hii”.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa kama mdau katika mambo ya utalii, wengi wamechangia mambo mengi kwa aina tofauti, lakini mimi naomba nizungumzie kuhusu kero zinazowasumbua wadau wa utalii. Wizara kwa nia njema kabisa imeanzisha ulipaji wa *park fee* kwa kutumia kadi aidha Exim *Bank* au *CRDB Bank*, lakini mimi naona wameanzisha bila kuwa tayari na mpango huu. Unakuta *gate* nyingi kwenye *gates* zile za kulipia…

**NAIBU SPIKA:** Umesema mpango gani?

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mpango wa kulipa kwa kutumia *credit card* katika *National Parks*. Wameanzisha mpango huu bila kujiandaa kwa sababu sehemu nyingi katika *National Parks* unakuta hakuna umeme, miundombinu haiko tayari, unapeleka wageni katika *National Park*, mnatakiwa mlipe kwa kadi mnaambiwa *computer* ziko *down*. Kwa mfano Mlima Kilimanjaro, unakuta wageni umeshawaambia wataanza kupanda mlima saa tatu, mnafika *gate* unaambiwa *computer* ziko *down*, wageni wanaweza kukaa *gate* mpaka hata saa tano sasa wageni wanaanza kulalamika hatimaye watakuwa hawana tena moyo wa kuja Tanzania kwa sababu ya usumbufu mdogo mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuhusu malipo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisimama hapa mbele, akasema malipo yote yanaweza kufanyika kwa Tshs. Mimi sikatai kabisa malipo kufanyika kwa *dollars* lakini tukumbuke kwamba wageni wengi wakija, wengine wanakuja wanatulipa kwa *credit cards,* wanalipa kwa *travellers cheques* au *bank draft,* sasa fedha hizi zinakwenda kwa *collection,* unaweza kukuta *operator* wanazo Tshs kwa nini tusiruhusiwe kulipa kwa Tshs wakati ambapo *Tour Operator* hawana hizi dola? Sijui *National Parks* wanafuata Sheria gani, kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema tunaweza kulipa kwa Tshs kwa nini tusilipe kwa Tshs? Tusipothamini fedha zetu, nani atazithamini? Juzi juzi tu mwezi uliopita nilikuwa Uganda, Uganda hawapokei fedha yoyote ya kigeni, wanathamini fedha zao, kwa nini sisi tusithamini fedha zetu!! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu wawekezaji. Nashukuru Muswada unasema Watanzania tutamiliki sehemu nyingi kama vile kupanda mlima na *Tour Operators,* kupeleka watu kwenye *National Parks* na kadhalika lakini tusije kuonewa kwa sababu ya umaskini wetu. Anakuja *foreigner* kutoka Ulaya, anamkuta *Guide* pale Moshi anamwambia tufungue biashara ya utalii, sasa sijui ni namna gani Wizara inaweza kushirikiana na *TRA* waangalie huyu kijana anayesema anafungua *Tour Operator,* analipa kodi, mtaji kautoa wapi? Maana mara nyingi hawa *foreigners* wanawatumia hawa vijana wadogo ambao hawana fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nizungumzie hizi *special camp site* zilizopo Serengeti, Ngorongoro na Tarangire. Wawekezaji wanakuja wanatengeneza *luxury camp site*, wanalaza wageni kule, wanawachaji watu, kama sisi *Tour Operator* unakwenda unamlipa karibu 200 *dollars* kwa mtu, lakini zile *special camp site* tunatakiwa tulipe 50 *dollars*. Je, Serikali inahabari kwamba hawa watu wanatengeneza fedha nyingi na hakuna jinsi ya kuweza kuzi-*recover* hizi fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kule Serengeti kuna mwekezaji aliyepo kule Gurumenti *Game Reserve*, yeye amepewa *hunting block*, amepewa *game reserve,* ameweka *rangers* wake kule, kwa nini *TANAPA* isiweke *rangers* kule kama ilivyo Arusha *National Park*, Serengeti na kwingineko? Yeye ana-*guide* pale mwenyewe, anaweza kufanya vitu vyovyote vile anavyotaka, watu wanaingia kule, Serikali itajua ni wageni wangapi wameingia katika ile *game reserve*? Tunaomba ile sehemu isimamiwe na *TANAPA* na yeye alipe *concession fee*. Huwezi kwenda kule, Watanzania, hawaruhusiwi kuingia katika ile *game reserve* wakati ile ni maliasili yetu! Tunaomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwa nini Watanzania hawaruhusiwi kuingia kwenye hifadhi ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba mibovu haipo tu katika madini, hata kwenye utalii kuna mikataba mibovu. Huyu mtu wa Gurumeti *Game Reserve* mkataba wake ulifanywa na Mkuu wa Wilaya, huyu Mkuu wa Wilaya aliwezaje kusoma ule mkataba na kuujua kisheria, hata kutia saini mkataba wa mabilioni tunajuaje kama Tanzania inafaidika na huu mkataba?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TTB, TTB* ni kwa ajili ya kufanya *promotion* na *marketing,* lakini *TTB* iwezeshwe basi waweze kufanya *marketing* ya kutosha, waweze kuzunguka kwenye *exhibition* zote, waweze kuuza utalii wetu vizuri. Unakuta tunakwenda kwenye *exhibition* ukiangalia *Tourist Board* za nchi nyingine wanapeleka hata watu wa ngoma, sisi tuna Wamasai, basi wasimame pale waonyeshe kuna Wamasai Tanzania, kuna hizi ngoma zipo Kusini, ngoma za huko Mbeya sijui hizi wanaziitaje, ziletwe kule kwenye maonyesho ili watu waweze kuona kwamba Tanzania tuna utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile unakuta mtalii mnafanya naye *deal*, mnakubaliana kabisa mwishoni anakuuliza, *how can I get to* Tanzania? Ni aibu kusema, huthubutu kusema kwa sababu unaanza ku-*advertise* nchi nyingine, unawaambia unaweza ku-*fly* na Kenya *Airways, KLM, British Airways and so forth.* Sasa ile hatu-*promote* Tanzania, ni aibu sana kwetu. Wizara iangalie ni jinsi gani, *at least* waiwezeshe *Air Tanzania* japokuwa ipo kwenye matatizo, lakini wafanye jitihada za makusudi kabisa kuhakikisha kwamba, *Air* Tanzania inaweza kwenda hata kwenye *destination* moja kule Europe. Hata watu wakitoka kwenye sehemu tofauti wanaweza kwenda pale hata kama ni Amsterdam, wakawa *connected* wakaja Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi kuna hii *crisis* imetokea Kenya, mimi ni mdau, tumepata *bookings* nyingi sana, watu hawataki kwenda Kenya, lakini wanashindwa kuja Tanzania ndege ziko *full booked*, ni ndege chache sana zinaweza kuja Tanzania. Sasa ni lazima tuangalie jinsi gani ya kuweza kuwapata hawa wageni waje Tanzania labda *Airport* zetu wapunguze *fees* ili zije ndege nyingi kama Kenya. Ndege nyingi sana zinakwenda Kenya labda sababu *airport fees* zao sio ghali kama vile kuja Tanzania. Kwa hiyo, katika hilo, tuangalie ni jinsi gani tunaweza kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Tour Guides*, ni vizuri kabisa Muswada umewatambua, lakini kuna hawa wanaokuja na *groups* wanajiita *Tour Leaders*. Mara nyingi wanakuja hapa wakati wa *high season*, wanakaa kwa miezi mitatu, wanafanya kazi ya *Tour Guide, at the end of the day* hawa *Tour Guides* wanakuwa kama *Porters* sio *Guides* tena. Kwa hiyo, labda kwenye kanuni, Mheshimiwa Waziri aangalie ni jinsi gani anaweza kuwa-*protect* hao *Tour Guides* ili wale *Tour Leaders* wasije wakafanya kazi za *Tour Guide* wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niungane na wenzangu kusema kwamba huu ujenzi wa mahoteli huko Serengeti usitishwe mara moja. Serengeti ni *seven wonders of the world* kwa sababu mazingira ya Serengeti ni mazuri, hayana majengo mengi, huwezi ku-*compare* Serengeti na Masaimara. Masaimara ni mji sasa siyo *Game Reserve*, tuseme ni *Zoo* sio *Game Reserve* tena, kwa hiyo tusije tukaji-*compare* na Kenya halafu tukaja kuharibu mazingira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Appealing Board*, naona kuna *two authorities* za kufanya *appeal*, sasa kwa nini kuwe na *Appealing Board* mbili kwenye Sheria moja? Naomba iwe moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, tarehe 2/3 kutakuwa na Kilimanjaro *Marathon*. Naomba niwaalike Wabunge wote mje mkimbie Kilomita tano kwa ajili ya *Kilimanjaro Marathon*, wageni wanakuwa wengi sana. Huna haja ya kukimbia Kilomita tano, unaweza kutembea huku unakunywa soda yako ili ku-*support* huu utalii ambao umeanza.

Vile vile katika Mlima Kilimanjaro tumeanzisha *tour* ya watu kwenda kwa baiskeli kuzunguka Mlima Kilimanjaro kuanzia Rongai kutokea Lemosho lakini barabara ya upande ule wa Rongai ni mbaya sana. Mwaka jana tulipata watalii karibu mia mbili ambao walikuja kufanya *cycling*, kuzunguka mlima, lakini mwaka huu wamekataa kabisa kuja kwa sababu ya miundombinu tu. Wapo *ready* kuja lakini ile miundombinu ndiyo imetudondosha. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo kuona ni jinsi gani anaweza kutusaidia ili watalii waweze kuja zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kabla sijampa nafasi ya kuchangia Mheshimiwa Mbunge mwingine, Mheshimiwa Lucy Owenya aliniandikia ki-*note*, anasema zile *Five Star Hotel* labda zijengwe kwenye Miji mikubwa lakini mkipeleka huko kwenye utalii wenyewe wale watalii hawataki *Five Star* wanazo New York, Uingereza, Amsterdam. Anasema kule kwenye vivutio angalau kuwe na kitu kinachofanana na Uafrika, kisafi kuliko ma-*five stars* ndani kwa ndani. Hakusema labda alikuwa anatafuta kupunguza muda.

Pia pale *Airport* ya *KIA* kuna kiwanja kikubwa, Mheshimiwa Waziri tulishakwambia kile kiwanja kwa nini msijenge hoteli kubwa wanapokuja watu na *KLM* usiku wakakaa pale na wanapoondoka usiku wakaingia kule, kuliko watoke moja kwa moja kwenye utalii pale.

Siku moja tuliwahi kuongea, kiwanja kilikuwa chini ya *Holding Company* inaitwa *ATCO* ambayo sasa imefutwa, imeingia katika hii *Holding* nyingine, kuna kiwanja kile hebu kafuatilieni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.25 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa kumi na moja jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipofunga shughuli za Bunge saa.7.00 mchana, tulikuwa bado tuna wachangiaji wengi tu na nilisema kwamba tutaendelea saa hizi na tutamaliza kesho asubuhi. Kwa hiyo, kwa sasa hivi nitamwita Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda na Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi ajiandae. Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, endelea.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Muswada wa Maliasili na Utalii uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwanza, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kaka yetu Prof. Jumanne Maghembe, kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya katika kuhakikisha kwamba utalii unaboreka na utalii huu unaleta manufaa kwetu sisi Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naendelea kuipongeza Wizara yake kwa namna ambavyo inajitahidi japokuwa bado safari ni ndefu. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba kama kweli tukijipanga sawa, basi inawezekana tukafika mahali utalii ukawa na manufaa kama ulivyo na manufaa katika nchi zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwanza, naomba kukubaliana au kuunga mkono hoja ya Muswada huu. Mimi binafsi ninaufahamu kwa sababu ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati hiyo ya Maliasili na Mazingira. Kwa hiyo, katika maeneo mengi yale yanayohusu urekebishwaji wa Sheria tuliweza kuvutana katika Kamati na ndiyo maana ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu pale ambapo kulikuwa na tatizo tuliweza kukubaliana. Kwa hiyo, kwenye upande huo kwa kweli sitakuwa na mengi ya kuchangia katika namna ya kuuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama tulisikia vizuri wakati Mheshimiwa Waziri anawasilisha Muswada wenyewe hasa alizungumzia mambo mawili kwamba kazi kubwa ambayo imesababisha Muswada huu uje mbele yetu kwanza, ni namna ya kuboresha utalii katika nchi yetu. Kwa hiyo, nitachangia mawazo kadri nionavyo mimi kwamba ni kwa njia gani tunaweza kuboresha utalii katika nchi yetu. Lakini la pili, ni kuendelea kulinda na kutunza mazingira ya hayo maeneo yetu ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nianzie na hili la lengo kubwa tulilonalo la namna ya kukuza utalii. Unaposema tunahitaji kukuza utalii maana yake ni kwamba tunahitaji kupata faida kutokana na utalii lakini vilevile tungependa kupandisha mauzo ambayo yanatokana na utalii huo. Hali kadhalika tungependa kuwa na jina maana hadi leo zipo nchi nyingi ambazo zinajulikana kwamba uchumi wao mkubwa ni utalii. Kwa hiyo, sisi nasi tungependa kuwa na jina au ile wanaita *market share* kubwa upande huu wa utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama hayo ndiyo malengo yetu, maana yake ni kwamba siku moja tufike mahali kwa kuwa wenzetu hasa wa Kenya tunawazidi kwa vivutio vingi, ikiwezekana ndani ya muda mfupi tuwe tayari tumewaacha hali kadhalika wenzetu wa South Africa. Nadhani katika Afrika, nchi hizo mbili ndizo ambazo tunahitaji kukimbizana nazo maana unaposema unasonga mbele lazima ujue unatoka wapi! Kwa hiyo, sisi lengo letu la kwanza ni kuhakikisha kwamba kati ya hizo nchi mbili ikiwezekana tunazishika na ikiwezekana kuzipita kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hayo ndiyo malengo ambayo tumekubaliana, sasa nini kifanyike? Lazima tuwe na mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba hayo malengo ambayo tumeyaweka ya kuongeza *market share*, ya ku-*maximize profit* ili hiki kilio ambacho Waheshimiwa Wabunge wengi tunalia hapa kiweze kufika mahali kikamalizika. Kama hivyo ndivyo, mikakati pekee ni pamoja na kugawana majukumu lakini kila walio na jukumu basi watekeleza malengo yao ambayo wanapaswa kuyatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyosema kwamba tunataka tuongeze utalii, katika majukumu ambayo tunahitaji tugawane lazima tujue hivi katika nchi yetu tunavyo vivutio vingapi vya utalii? Kwa hiyo, tukiviainishe hivyo vivutio vya utalii na kufahamika na zoezi la kuviainisha maana yake ni lazima iwepo sekta fulani ambayo wao kazi yao ni kuhakikisha kwamba kila kivutio kilichopo katika nchi hii kinajulikana na hii itatusaidia hata sisi watu wa Mara kwa sababu tunavyo vivutio vingi kwa mfano tunao Mto Mara pale ambao umeanzia Ziwa Victoria mpaka kule Serengeti lakini hakuna mtu anajua habari ya Mto Mara. Ukiangalia katika nchi nyingine kwenye Mito kule ndiko watalii wanapozungushwazungushwa na boti na watu wanapata fedha lakini hicho ni kivutio ambacho wala hatukiangalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika ukiangalia Ziwa Victoria, Ziwa Victoria, Mheshimiwa Waziri, naamini atakuwa analifahamu vizuri, ukitokea hapa *gate* ya Dabaka kwenda Ziwa Victoria ni kilometa nne peke yake. Sasa ni namna gani pamoja na ukubwa wa Ziwa Victoria hao watalii watafika kule kwenye Ziwa Victoria ambapo ni umbali wa kilometa nne peke yake, haiwezekani. Haiwezekani kwa sababu hata ile barabara ya kilometa nne hatuwezi kuitengeneza! Ndiyo maana ninasema kwamba lazima iwepo sekta ambao wao kazi yao ni kuhakikisha hivyo vivutio vyote vya utalii wanaviainisha ikiwa ni pamoja na kwenda huko Tabora, Singida ambapo mambo mengi ya kale yapo huko. Siku moja nilienda Kigoma nadhani Katavi kitu kama hicho, vipo vivutio vingi sana na vizuri sana lakini vyote hivyo vinahitaji kuainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa wameainisha vivutio hivyo, ni lazima miundombinu iwepo katika maeneo yote hayo. Hii ina maanisha kwamba wataalam au wale wanaohusika na upande huo wakae na kuona ni kwa kiasi gani au ni kwa namna gani tunaweza kupeleka miundombinu katika sehemu zenye vivutio hivyo. Tunahitaji kuwa na mipango ya muda mrefu lakini na ile ya muda mfupi ambayo kama nilivyosema leo kufika pale Ziwa Victoria ni kama kilomita nne peke yake ambazo nazo bado tunashindwa kuzitengeneza ili watalii waweze kufika hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lazima tuwe na mikakati ya namna ya kuuza vivutio tulivyonavyo. Katika kuuza vivutio tulivyonavyo, hilo kwa kweli sisi Watanzania bado tuko nyuma sana na hicho ndicho wenzetu wa Kenya na South Africa wanafanya maana utasikia wanatangaza kwamba inachukua masaa mawili kuuona Mlima Kilimanjaro. Sasa mtalii anakwenda South Africa ili aweze kufika kuona Mlima Kilimanjaro wakati sisi Mlima Kilimanjaro akitua tu pale Kilimanjaro *Airport* kabla hajaenda popote tayari ameshauona Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mojawapo ya kazi kubwa tuliyonayo ni pamoja na kuwa na watu makini watakaoweza kutusaidia kuuza hivi vivutio tulivyonavyo. Namna ya kuviuza, ninakumbuka mwezi Desemba, nilienda Singapore, tulipokuwa kule tukaambiwa kuna mahali kuna kivutio cha mbuga za wanyama na watu wanaenda kukitembelea, wanaenda kule saa 5.00 usiku. Sasa mimi nikajiuliza hivi saa 5.00 usiku wanaona wanyama gani hao? Wakaanza kunisimulia wanyama mbalimbali ambao wanaonekana kule. Kweli tukalipa pale, kila mmoja akalipa shilingi za Kitanzania zisizopungua 80,000/=, muda tuliotumia kuzunguka mle hatukufikisha hata dakika 40. Tukafika pale, wakatwambia tunapanda treni kumbe si treni ni gari ndogo tu wamelikata wamewawekea humo viti mnapanda kwamba hiyo ndiyo treni, tena wale wanyama wamewawekea uzio, unatembea hivi unamwona simba yupo hapo na kwa kuwa ni usiku sasa huwezi kuona ile *fence*. Hivyo tu, shilingi 80,000/= zikaenda na kwa kweli tulipofika pale watu walikuwa wengi na wanafuatana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hiyo inaonyesha dhahiri kwamba kati ya kazi kubwa ambayo tunahitaji kuifanya, ni kuuza vivutio tulivyonavyo kwa hao watalii na kuwaambia ni kitu gani kipo Tanzania na kinapatikana wapi? Kama zoezi hilo litafanyika ipasavyo, basi ni dhahiri kabisa tutakuwa tumeupanua utalii kwa kiasi cha kutosha.

Mhesimiwa Naibu Spika, leo *at least* tunamshukuru Mheshimiwa Waziri maana nikiangalia katika ile bajeti mwaka huu *TTB* wamepata fedha za kutosha lakini bado nadhani nguvu zaidi inahitajika ili waweze kushughulikia suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hilo ni pamoja na kutambua vivutio vilivyopo na ni akinanani wanavihitaji. Kati ya watalii tulionao kuna mmoja nimemsikia akisema kwamba wapo wale watalii wanaoitwa “bishuka”, hata hao watalii wa **“**bishuka” tukiwajua**,** basi tukaangalia na maeneo ambayo wanaweza kwenda, tukawatangazia, ni imani yangu wataweza kwenda huko na katika kipindi kifupi sana utalii wetu utaweza kwenda juu na tutaweza kupata mapato ya kutosha kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la kukuza utalii linatakiwa liende sambamba na suala zima la namna ya kudhibiti mapato yanatokana na utalii. Leo yawezekana tukapigia kelele sana lakini labda mapato yanayotoka ni makubwa kuliko yanayoingia. Wakati mwingine huwa ninaona humu Bungeni tunafanya zile kazi za zimamoto tunaposema Kamati iundwe na uchunguzi ukafanywe. Leo mtu akienda kule *TANAPA* akachunguza yanawezekana kuna fedha nyingi sana zinafujwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakati mwingine katika kuboresha hayo, ni ushauri wangu kwamba hivi kuna haja gani ya hawa hawa kufanya kazi zote kwa maana hao hao wakakusanya fedha, hao hao wakazitumia fedha. Kwa hiyo, kwa wakati mwingine kama Waziri atakubaliana na mimi mwaka mmoja tu tungesema hebu tuwaombe watu wa TRA waingie pale wawe kwenye hicho kitengo cha kukusanya halafu tukaona matokeo yamekuwa namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata baadhi ya huduma zingine zinazotolewa, tunayo nafasi, kwa mfano, wale watu utakuta wanafanya kazi ya kutengeneza miundombinu, si ajabu ukakuta fedha wanazotumia wale watu katika kutengeneza ile miundombinu tukiamua kuwapa wakandarasi tofauti tofauti yawezekana wakatengeneza miundombinu ile ile lakini kwa fedha nusu ya fedha ambazo zinatumika sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hiyo ni rai yangu kwa Mheshimiwa Waziri, katika kuhakikisha kwamba tunapandisha utalii vilevile hebu tuangalie namna ya kudhibiti mapato. Mimi wakati fulani nilisikia kuna *forgery* wakati wa kukusanya mapato. Hivi kama tatizo hilo lipo na yawezekana hatujapata tu nafasi ya kupeleka kule Wakaguzi wakakagua vizuri, basi ikiwezekana mwaka mmoja tuombe *TRA* watusaidie kukusanya fedha huko yawezekana tukakusanya fedha mara mbili ya kiasi hicho cha fedha ambazo wanazikusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni suala la upungufu wa hoteli. Suala la upungufu wa hoteli katika nchi yetu wala si tatizo kwa sababu tunao Watanzania wengi wenye uwezo mkubwa wa kujenga hoteli. Tatizo kubwa lililopo ni zile *bureaucracy* ambazo zipo mpaka kuja kukubaliwa kwamba sasa hebu jenga hapa hoteli. Naamini Watanzania wengi leo wakionyeshwa, maana unafika mpaka habari ya *feasibility study*, kujua *environment impact assessment,* Watanzania wetu wengi unapowafikisha hapo ni lazima siku zote watakuwa wanaelekea kushindwa. Kwa hiyo, ni imani yangu kama watasaidiwa namna ya kuweza kuyafanya hayo, basi upungufu huu ambao unaojitokeza katika nchi yetu ndani ya miaka miwili tunaweza kuwa na hoteli nyingi na hivyo tukaweza kuwahifadhi watalii pasipokuwa na tatizo lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusisitiza sana kwamba Mheshimiwa Waziri ni vizuri akaangalia namna ya kutangaza hivi vivutio vilivyopo na namna ya kutengeneza ile miundombinu ambayo ni ya muda mfupi kutoka katika maeneo mengine kuliko pale tutakapotegemea tu watu wote kufikia katika eneo moja. Inawezekana ndiyo maana wakati mwingine inaonekana kuna tabu wakati wa kuwasafirisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hii miundombinu ni pamoja na viwanja vya ndege. Leo Musoma utashangaa kiwanja cha ndege tulichonacho ni cha udongo, ndege nyingi wala haziwezi kutua katika ule uwanja kulingana na uwanja wa ndege wenyewe ulivyo na miundombinu mibovu. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba kwanza kwa Musoma, mahali ilipo kukiwa na miundombinu mizuri kama hiyo, basi maana yake huu utalii utaboreka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia hapo, naomba kuunga mkono Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia machache kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla ya hapo, naomba niombe radhi kwa sababu mchana ilifika zamu yangu ya kuzungumza, bahati mbaya nilikuwa nimebanwa

kidogo na tatizo la kibinafsi, kwa hiyo nikashindwa kuwepo humu Bungeni kwa muda huo, naomba radhi sana kwa hilo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli kabisa katika Muswada huu mengi yamekwishazungumzwa na inakuwa ni matatizo sana wakati wenzako wameshazungumza mambo mazuri halafu wewe unakwenda unapandiapandia tu, unazungumzia lile ambalo tayari limekwishazungumzwa, huwa ninapata shida sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini labda tu nizungumzie katika upande wa dhamira ya Muswada. Kama ilivyoonyeshwa kwenye Muswada wenyewe, dhamira ya Muswada ni kuweka utaratibu mzuri katika kusimamia na kukuza biashara ya utalii nchini, hiyo ndiyo dhamira kuu ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikianza kutafsiri maana ya dhamira hii nakuja kujikuta kwamba ni ukweli kabisa ni maeneo yale tu ambayo tayari kuna shughuli za utalii zinafanyika ndiyo yatakayoweza kufaidika. Sasa nikishafikia hapo ndipo naenda katika maeneo yangu. Maeneo yangu ni baadhi ya yale maeneo ambayo kwa kweli hakuna hata dalili za kufikiria kuweka vivutio vya utalii. Kwa kweli hilo kidogo linanipeleka mahali kuanza kusikitika kwa nini inakuwa namna hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano tu, katika maeneo kwa mfano, Wilayani kwangu Chunya kuna vivutio vingi sana. Mwaka 2006 katika Bunge lako hili hili Tukufu, nilijaribu kukumbushia ili kusudi Wizara angalau iangalie maeneo ya Wilaya ya Chunya kwa vivutio ambavyo tunavyo na ilifikia mahali ikawa kama ni kichekesho kidogo, kwa sababu nilielezea baadhi ya mambo yanayopatikana kule ambayo ni mambo ya ajabu ajabu, lakini ikaonekana kana kwamba labda nilikuwa nazungumzia hadithi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia hasa zaidi katika upande wa Wilaya yangu. Nichukue mfano tu wa baadhi ya vivutio. Ukifika kule tunao Mlima Kwimba. Huo Mlima Kwimba kwanza ukiuangalia tu ile sura yake unaweza ukasema ni afadhali leo hii nianzishe shughuli za utalii katika huu Mlima. Ni mlima ambao unapendeza sana, kila upande ambapo utasimama utaona ni kama ule upande mwingine ambapo ulikuwepo, kwa kweli panavutia sana. Ukipata bahati ya kupanda pale juu mlimani ni kama mtu alitengeneza kiwanja na mahali hapo ndipo kuna wanyama wengi sana na utaona mambo mengine mengi tu ambayo yapo katika mlima huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine, katika huo mlima, kuna mapango ambayo yana historia. Kama kweli mapango hayo yanataka kuendelezwa kitalii yanaweza yakaleta kipato kikubwa sana katika eneo hilo. Kwa mfano, kuna pango ambalo wale Watemi wa zamani ilikuwa kama wewe raia ukikosea, basi yule Mtemi anakuchukua mpaka hapo kwenye pango, anakwenda akakusimamisha, mradi kama hukumu imeshatolewa, basi pale ndiyo mahali pa kutolewa hukumu, anakusukuma ndiyo unakwenda hivyo. Sasa sehemu kama hiyo kama ikiendelezwa vizuri na maelezo mazuri yakapatikana kweli haiwezi ikawa kivutio kizuri cha utalii?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sehemu nyingine katika mlima huo huo, kuna pango ambako wenyeji wa kule ndiyo wanakwenda kutambikia. Ni sehemu ambapo kuna vitu vya kale mle ndani, siyo lazima kuingia, lakini kama utaratibu unafanyika wa kuweza angalau kuangalia na kupata maelezo ya pale ni kivutio kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu kwa mfano nchi ya Korea yaani unakwenda kuona wakati ule wa mapambano yao na Wajapani, kiongozi wao alikwenda kwenye mlima na kusimama tu kwenye mlima pale akiwa anaangalia kule sehemu yake akionyeshwa kuwa hii ndiyo sehemu yangui. Wenzetu ile sehemu wameweka kama ni sehemu ya tukio muhimu, ni sehemu ya kwenda kutembelea na inaingiza fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mapango mengine. Kuna pango katika Kata yangu ya Ngwara, yapo mapango yenye historia kubwa sana. Halafu ukienda katika Ziwa Rukwa, wenzangu wa upande wa Ufipa wanaweza wakanisaidia, kuna pango na mlima unaoitwa Ryamba lya Mfipa. Sasa Lyamba lya Mfipa kuna maelezo mazuri sana katika lile eneo. Lile pango limeanzia ndani ya maji huko watu walijaribu kwenda na kuna maelezo mazuri sana. Nafikiri Mheshimiwa Waziri, labda angeweza akajaribu kuangalia maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tukio la kiasili, mawe kwa mfano, kwa sababu nazungumzia hayo kutokana na jinsi wenzetu wanavyothamini mambo ya kihistoria. Katika mapigano ya vijiji na vijiji, kuna kijiji ambacho baadhi ya wananchi wakati wakishatangaziwa kwamba kuna vita kesho walikuwa wanakwenda, sasa wakifika mahali kulikuwa na jiwe moja ambalo ndiyo walikuwa wananolea zile silaha, mikuki, mapanga na kila kitu, eneo hilo bado lipo na jiwe hilo bado lipo. Kitu kilichojitokeza wanapokuja wageni sasa wanauliza mnakwenda wapi wanawambia tunakwenda Kapalala. Kapalala ni lugha ya kule nyumbani. Kapalala ni mahali ambapo unanoa yale mapanga pamoja na mikuki, jiwe hilo bado lipo. Hivi tukilitengeneza vizuri, tukiyaweka maelezo vizuri kweli hayo maelezo hayawezi yakawa ni kivutio?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo fukwe, fukwe katika Ziwa Rukwa ni maeneo mazuri sana. Tunazo vilevile mbuga za wanyama mbili za Ngwara na Gua lakini sasa hivi zile mbuga zimegeuzwa kuwa vitalu vya kuwindia. Ni kweli tunafaidika kwa hilo lakini nafikiri kwamba ni vizuri tukaangalia jinsi gani vilevile wananchi wa maeneo yale wanavyoweza wakafaidika katika upande wa mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu baada ya hapo, niingie kwa ufupi kabisa katika upande wa mazingira. Kwa kweli sasa hivi kutokana na jinsi maeneo yetu yalivyoachiwa, basi uharibifu umekuwa mkubwa mno. Wilaya ile ina bahati mbaya kwamba lolote baya basi ndilo linalopelekwa huko, basi mifugo ndiyo imejaa kule, kiasi kwamba wakati wa kiangazi ile mifugo yote inateremka Ziwani. Inapoteremka Ziwani, matokeo yake ni kwamba hata kina cha maji ya Ziwa sasa hivi kinapungua. Nafikiri pamoja na kwamba tunajaribu kuzungumzia mambo ya maendeleo ya utalii labda vilevile si vibaya tukaangalia jinsi gani tunaweza tukahifadhi mazingira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo asubuhi nafikiri ni Mheshimiwa Siraju Kaboyonga alijaribu kusema kwamba kule Katavi kuna twiga mweupe. Kwa kumbukumbu, twiga huyo mweupe alitokea katika upande wa Mlima Kwimba, amekimbilia kule kutokana na hali ambayo sasa hivi imejitokeza. Mifugo hii tunayofuga haikai kabisa kabisa pamoja na wanyamapori. Mifugo ilipoanza kwenda katika yale maeneo ya wanyamapori wameanza kukimbia ndiyo hao ambao wamekimbilia katika upande wa Katavi. Tulikuwa na faru mweusi katika lile eneo, lakini sasa hivi ni wachache sana ambao unaweza ukawaona wote wamekimbilia upande wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kulikuwa na mawazo wakati tukilizungumzia suala hili kwamba ni jinsi gani tunaweza tukahifadhi Mlima Kwimba, likaja wazo kwamba pengine kwa nini tusiwalazimishe hao wanyama wakarudi, kwa sababu tatizo lao ni maji wakati wa kiangazi. Hivi tukifanya ubunifu wa kuwaweka hao wanyama wakati wa kiangazi wakiendelea kuwa pale itakuwa ni vibaya? Njia ni rahisi tu ni kiasi tu cha kujenga mabwawa, kiasi cha kujenga malambo kama wanyama wanayakuta maji kila wakati yapo pale hawawezi wakahama. Nafikiri labda Wizara ingejaribu kuangalia katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba tu nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba wale mamba katika Ziwa Rukwa bado wapo. Namshukuru Naibu Waziri baada ya kumweleza hivyo alijitahidi kupeleka Askari kwenda kuwawinda. Mwaka 2006 niliambiwa kwamba ile *quarter ambayo* ilikuwa inatakiwa kuwindwa haikuweza kutekelezeka. Mwaka jana wakapelekewa tena *quarter* hiyo vilevile haikuweza kumalizika. Naomba nimkumbushe tu Mheshimiwa Waziri kwamba eneo lile bado Askari hawajamaliza kazi na kwa kweli mamba wanaleta madhara makubwa sana kwa wananchi wa kule. Namwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kufikiria suala hili ili kusudi angalau aweze kutusaidia katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mara nyingi huwa nazungumzia upande wa Wilaya yangu, matatizo ambayo yako maana siwezi kuzungumzia maeneo mengine wakati kwangu kwenyewe ndio kunadorora, kwa kweli huwa sijisikii vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa nafasi hii uliyonipa ili nami nichangie kidogo kwenye Muswada huu. Kwanza, sina budi kukiri kwamba, niko kwenye Kamati ya Maliasili na Mazingira, kwa hiyo, nimeshiriki katika kuchangia hoja ambazo zitakuwa zimekwishatolewa na wenzangu au na Kamati kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami ninamshukuru Waziri, Naibu na Wizara kwa ujumla, kwa kuleta Muswada huu, kwa wakati huu ambapo ninadhani ni muafaka na hasa kwa sababu ni Muswada mzuri. Ninasema ni mzuri kwa sababu ninajua kwamba, kuna juhudi kubwa za kutangaza utalii katika nchi yetu na kuvutia wawekezaji waje kuwekeza

katika nchi yetu, kupitia utalii ili Serikali iweze kupata mapato makubwa zaidi ambayo yanawezekana. Kwa kuwa tunaamini Wizara hii au sekta hii inaweza kuzalisha, pengine hata mara kumi au ishirini kuliko inavyofanya sasa hivi, kwa hiyo, ninapenda kuzipongeza juhudi hizi ambazo ni nzuri na zina manufaa makubwa kwa Serikali yetu na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile wenzangu wengi wameshatangulia kuzungumza ili na mimi nisiirudie, ningependa kujikita kwenye masuala matatu madogo. Moja, ninataka kuzungumzia suala linaloitwa kitaalamu *carrying capacity* au *limit of acceptable use,* ambacho ni kigezo au uwezo wa eneo husika, kustahimili uwekezaji.

Katika suala hili, tunazungumzia uwekezaji kwenye masuala labda ya hoteli, namba ya vitanda vinavyotakiwa kuruhusiwa au namba ya wageni wanaoruhusiwa katika eneo fulani katika muda fulani, Kiingereza tunaita *carrying capacity,* lakini *carrying capacity* ni *technical* na namna ya kuifikia hiyo, inahitaji kujua masuala mengi ya kiikolojia au kujua mambo ya sayansi.

Inachukua muda mrefu kuweza kupata kigezo na kuweza kujua unahitaji hoteli ngapi au vitanda vingapi katika hoteli fulani, bila kuathiri mazingira ya eneo lile. Kwa hiyo, inabidi ufanywe utafiti kuweza kupata kiwango hicho, lakini kuna kitu kinaitwa *limit of acceptable use,* ambacho ni makubaliano tu kati ya wale watu wanaohusika; wanaweza kuwa ni wataalam wanakaa wanajadili kwa uzoefu wao wanasema eneo hili tunaweza tukaongeza hoteli zisizidi kiasi fulani. Hawawi na kigezo cha kisayansi cha kuweza kueleza kwa nini ninyi mnasema ni hoteli tano, sita, saba au vitanda kadhaa na sio pungufu au zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalisema hili kwa sababu kuna msukumo huu wa kutaka kuongeza wageni na kupata mapato makubwa zaidi na kwa vile tunataka kuvutia wageni kwenye maeneo ya fukwe zaidi na maeneo ya hifadhi za Taifa. Maeneo haya ni nyeti ni rahisi kuyavuruga na kuyaharibu kimazingira. Tukishayaharibu sio rahisi kuyarudishia tena na mwisho wake itakuwa ni kwamba utalii wenyewe utaporomoka utakwisha. Kwa hiyo, itakuwa ni sawa na kukaa kwenye tawi la mti halafu tunakata shina. Kwa hiyo nilitaka kuzungumzia juu ya vigezo hivyo kwa sababu tunapotaka kuongeza kwa nia nzuri tuongeze vitanda na hoteli kwenye maeneo ya Hifadhi za Taifa au ufukweni, si vizuri kwenda haraka bila ya kujua athari ya kufanya hivyo kwenye mazingira, ndiyo maana vigezo hivi vinasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hifadhi zetu, ninajua wanatumia zaidi kigezo cha *limit of acceptable use* kuliko *carrying capacity,* kama nilivyosema, ku-*determine carrying capacity* inahitaji utafiti, hiki ni kitu kigumu kidogo. *Limit of acceptable use* ni kigezo rahisi, watu wanaohusika wanakaa wanakubaliana ni kiasi hiki. Kwenye Hifadhi zetu za Taifa, wanatumia zaidi *limits of acceptable use,* kwa hiyo ni watu fulani hukaa na kujadili kwamba, hapa tunaweka vitanda kadhaa na tumejionea kuna *tendency* tayari ya kugeuza hata *general management plans,* ambazo zinaongoza uwekezaji na maendeleo katika hifadhi zetu. Watu hawapendi kufuatilia vigezo hivi na kusema hapa tubadilishe

tena *GMP* au *General Management Plan,* itupe ruhusa zaidi, kuwekeza kwenye eneo hili. Kwa maneno mengine, vigezo vinavyotumika ni vya ubabaishaji kidogo, havina msingi wowote wa kisayansi.

Kwa hiyo, tunaweza tukakuta tunavuruga maeneo yetu ya hifadhi au fukwe kwa tamaa hii ya kutaka tupate fedha zaidi, bila kuangalia au kuwa makini katika kutumia vigezo vinavyosaidia kuhakikisha kwamba, uwekezaji huo hauharibu mazingira ya hifadhi au fukwe zetu. Kwa hiyo, ningependekeza Waziri au Wizara hii, iwe makini, watumie *carrying capacity* kuliko kutumia *limits of acceptable use*, hasa katika mazingira ya sasa ambapo tunafanya *promotion* ya hali ya juu sana na kutaka kuongeza vitanda, kuongeza watalii katika maeneo yetu ambayo ni nyeti sana. Hilo lilikuwa la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, linahusiana na suala zima la kuongeza ukubwa wa viwango vya wageni kulipia ada kutegemeana na aina ya kivutio. Kwa maneno mengine, kuna maeneo mengine ambayo ni nyeti sana na ni hatari sana, kwani yanaweza kuharibiwa kirahisi sana. Tusingependa watu waende ovyo kule lakini ni vivutio vizuri sana, kwa hiyo, hata ungeweka bei gani, watu watapenda kwenda kule. Sawa sawa na Mlima wa Kilimanjaro, hata ukipandisha bei ya viingilio, watu watakuja tu kwa sababu ni kivutio muhimu sana.

Katika hifadhi zetu vilevile kuna maeneo ambayo ni vivutio maalum, hata ukienda Serengeti au Ngorongoro; kule Serengeti kuna milima kule wanasema ni visiwa, maeneo yale ndiyo makazi mazuri sana ya viumbe mbalimbali ni sehemu nyeti sana na watu hupenda kwenda ili kuona wanyama fulani fulani. Maeneo kama hayo, yalitakiwa yatengwe vizuri na ili kwenda kutembelea kule, unalipa zaidi, yaani kinawekwa kiwango kikubwa kuliko kuweka *flatrate* kwa hifadhi yote wakati unajua sehemu nyingine ni nyeti na ni vivutio vikubwa ambavyo vingeweza kupokea malipo makubwa kuliko yale yanayotolewa.

Kwa hiyo, tunaweza kuongeza mapato kwa kuongeza bei au malipo kwenye maeneo nyeti ambayo ni *sensitive,* tukapata fedha kwa watalii wachache ambao wana uwezo kwenda huko na wale wasio na uwezo, wenzangu na mimi, hawatakwenda huko kwa sababu fedha yao haitoshi. Tuwaachie wale wenye fedha walipie kule na watape fedha tunayoitaka sisi. Vilevile ili kutokuharibu maeneo nyeti kama yale, tunachotakiwa kufanya ni kuhakikisha kwamba, watu hawaendi kwa magari, kwa sababu magari yanaharibu sana maeneo yale hivyo, wanatakiwa washukie mahali waende kwa miguu. Kwa hiyo, kwanza, wanakuwa wachache halafu pili, wanatembea kwa miguu, ile *trumpling* inayofanywa na magari haiwezi kutokea. Tukifanya hivyo, bado tunaweza kuongeza mapato na kuhifadhi maeneo yetu vizuri na tukaendelea kuvuna kwa miaka mingi ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho linalohusiana na huu msukumo wa uwekezaji, nimeona kwamba, bado tunasukumia Kaskazini kwenye Hifadhi za Serengeti, Ngorongoro na kwenye fukwe za karibu ya Dar es Salaam, bado tunataka tuongeze hoteli huko utadhani Tanzania hatuna maeneo mengine wakati yapo. Ninaambiwa kwamba, kule Ngorongoro tunataka tuongeze hoteli nyingine sita, sina ubaya na hilo lakini kwa

nini Ngorongoro tu; mbona kuna maeneo mengi huko Kusini, tunazungumza kila wakati, jamani panueni uzio wa utalii pelekeni Magharibi na Kusini; kwa nini tunang'ang'ania huko huko mpaka tunafikia mahali hoteli zinaangaliana? Ngorongoro pale, umbali unaotakiwa kati ya hoteli na hoteli ni kilomita zaidi ya mbili, lakini leo unakuta kilomita hata 10, 20 hoteli zimekaa mfululizo; kwa nini tusipeleke maeneo mengine?

Hata kule kwangu Ludewa, Ukanda wa Ziwa Nyasa, kuna vivutio chungu nzima;. Milima ya Livingstone, Samaki wa Mapambo, *Skuba Diving*, ukitaka chochote unaweza na utafiti umeonyesha kwamba, kuna utalii unawezekana kati ya *Matema Beach* na Manda au Mbambabay kule chini, safi kabisa; kwa nini hatuendi huko na tafiti zimeonyesha kwamba inawezekana?

Kwa hiyo, nilipenda kwamba, wakati tukipitisha sheria hii, hebu tupanue maeneo kwa makusudi kabisa. Muswada huu unazungumzia juu ya *levy*, tunataka tukusanye fedha kutokana na utalii, ninategemea kwa ajili ya kupanua utalii maeneo mengine, basi fedha hizo zitumike kupanua utalii Kanda ya Kusini na Magharibi ili tuepukane na suala la kuharibu mazingira kwenye hifadhi zetu za Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja hii, imekuja wakati wake na ni nzuri, ila ninaomba tuzingatie hayo niliyoyazungumzia, vigezo vya kuhakikisha kwamba, *carrying capacity* haiwi-*exceeded* na kwamba, tuongeze aina ya malipo kwa vivutio mbalimbali na tusambaze utalii maeneo mengine hasa maeneo ya Kusini. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Muswada huu wa masuala ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maendeleo ya dunia sasa hivi, katika vitu ambavyo kimsingi vinategemewa sana ni pamoja na masuala ya utalii. Utafiti nilioufanya hivi karibuni, unanielekeza kwamba, mnamo mwaka 2000, takribani watu 998 milioni walikuwa watalii katika nchi mbalimbali, maana yake kama nchi ya Tanzania yenye watu milioni 36, basi hapo wanaingia mara kadhaa na watu hawa katika nchi nyingine ambazo walikuwa ni watalii, walitumia kiasi cha shilingi bilioni 478. Katika vitu ambavyo vinaingizia mapato katika Taifa lolote, kimsingi suala la utalii katika nchi zilizoendelea ni suala ambalo linaingiza kipato kikubwa sana, likifuatiwa na suala la utengenezaji wa magari, kemikali, petroli na hatimaye chakula. Katika nchi zinazoendelea, suala la utalii ni muhimu ingawa suala hili linakumbana na changamoto nyingi sana, changamoto nyingine ni pamoja na masuala ya miundombinu. Masuala ya miundombinu katika utalii, yamekuwa ni changamoto kubwa sana. Tunaposema miundombinu, maana yake ni vitu kama barabara, viwanja vya ndege na miundombinu mingine ya huduma mbalimbali, imekuwa ni changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkoa ninaotoka, tunazo mbuga za wanyama kadhaa na vivutio vingi sana, lakini pato bado limekuwa dogo kutokana na miundombinu. Tunalo eneo linaloitwa *Ruaha National Park*, lakini inakuwa ngumu kuwafikisha watalii kwa sababu kwanza, kiwanja cha ndege hakifanyi kazi, kinaitwa

Kiwanja cha Ndege cha Nduli. Barabara ya kufika huko inakuwa ni kitendawili, wanaoweza kutumia *charter flight* wanakwenda pale kuna kiwanja kidogo, lakini hili ni jambo ambalo lazima tuliangalie. Zipo Wilaya za pembezoni, ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Makete na Ludewa, hakika kule barabara hazifikiki. Kwa hiyo, tunaposema tunaleta Muswada huu ili kuboresha masuala ya utalii ni muhimu sana suala hili la miundombinu, likaenda sambamba ili kuweza kunufaika kama jinsi ambavyo inastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee pia ile barabara ya kutoka Mikumi mpaka Iringa, kuna eneo linaitwa Daraja Mbili, pale kwanza kuna mbuga ya wanyama inaitwa Mikumi, lakini vilevile kupitia barabara ile, unaweza ukaenda mpaka *Ruaha National Park* na maeneo mengine mengi ya Kanda ya Kusini. Barabara ile ya eneo la Daraja Mbili limetoboka, yaani unapita daraja la kwanza na la pili, lakini bado mpaka leo Wizara haijarekebisha takriban mwaka mzima. Ajali nyingi sana zinatokea pale na ningeomba Wizara iliangalie sana eneo la Daraja Mbili, Mikumi. Wameweka mapipa, kwa hiyo, inabidi kuiangalia barabara hiyo; Wabunge wanapita, Makatibu Wakuu juzi walikuwa Mbeya wamepita pale pale na jana wengine tumepita, lakini hatujaona uboreshaji wa aina yoyote na leo hii tumeleta Bungeni huu Muswada wa Masuala ya Utalii, kwa hiyo, nilidhani masuala haya ya miundombinu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Desemba, nilibahatika na mimi kuwa mtalii katika nchi za Mashariki ya Kati. Nilipokwenda kule, kila kituo nilichofika tulikuwa timu ya watu 80 na kila kituo walisema huduma za jamii kwamba, wanaotaka kunawa mikono, wanaotaka kupata huduma ndogo ndogo zinapatikana, yaani wale *Tour Guide* wanafahamu zinapatikana. Nikaanza kuwauliza, wenzangu hivi sasa hizi huduma, maana yake Tanzania tukiwa tunasafiri toka Dar es Salaam mpaka Iringa, tuna-*park* gari tunasema jamani tunachimba dawa, tunakwenda tunachimba dawa. Hizi *infrastructure,* tunapozungumzia utalii leo tunatarajia tupate watalii 2,000, 3,000 waje; sasa sijui huduma hizi ni jukumu la watu binafsi au nani? Jambo hili inabidi tuangalie jinsi ya kuliboresha. Kwa hiyo, mambo haya tunapozungumzia utalii, nilidhani hakika ni mambo ambayo tunapaswa tuyatazame sana, mkiweza kuwaalika sekta binafsi wajenge zile huduma muhimu itatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, ninaomba sasa niingie kwenye Muswada wenyewe. Nikianza na ile sehemu ya tafsiri, kumekuwepo na tafsiri nyingi sana na nyingine wanasema labda kitu fulani kitamaanisha, kwa mfano, tafsiri ya *Director*; imesema kwamba, *Director* wa masuala ya Utalii atakuwa ni *Director* kwa mujibu wa kifungu cha tano. Kwa hiyo, ningeshauri kwamba, Muswada huu useme atakuwa ni *Director* kwa mujibu wa maelezo ya kifungu cha tano cha Muswada huu. Maana yake, inawezekana ni kifungu cha tano cha Katiba au cha sheria nyingine. Kwa hiyo, hayo maeneo mawili pale kwenye *Director,* tuangalie kama ni kifungucha tano kwa mujibu wa Muswada huu au sheria hii, lakini kwenye *definition* ya *designated tourism facility or activity,* ieleze kwamba, ina maana ni kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kifungu cha 11; kinachoelezea juu ya masuala mazima ya *registration* na kifungu kingine kinaelezea juu ya masuala ya leseni

kwamba, huduma zote za utalii, itabidi kufanyika *registration* na leseni, hivi ni vitu muhimu sana.  Hapa nilikuwa nina ushauri kidogo kwamba, tunapozungumzia leseni kama ni hoteli au *camp site* au huduma nyingine zozote za masuala ya utalii, tuangalie maana kwa mujibu wa Muswada huu inasema kwamba, vibali vitapatikana kila mwaka na kwa uzoefu wangu mdogo ni kwamba, ili upate kibali cha ku-*operate* hiyo hoteli au *camp site,* kuna hatua; unachukua fomu unajaza, Kamati zinakaa na kujadili na kwa mujibu wa Muswada huu umesema, kibali itabidi kipatikane kila baada ya miezi 12. Mimi ninaona kama hii miezi 12 ni michache, maana inawezekana mpaka ikapatikana hiyo leseni itatumika *let us say* ndani ya mwezi mmoja taratibu zote zikafuatwa.

Sasa ningeomba kushauri, kama ingewezekana kuongeza muda basi Wizara ijaribu kulitafakari ili ile leseni ikipatikana, iweze kudumu angalau zaidi ya miezi 12, kuliko kila baada ya miezi 12 leseni ikapatikana.  Vipo vitu vingine kwa mfano, ada, ninakubaliana kabisa ada ni lazima zilipiwe kila mwaka, hii ni sahihi kabisa, lakini pia tukisema kwamba leseni italipiwa baada ya miezi 18, haimzuii afisa masuala ya utalii kwenda kukagua na kuangalia shughuli za ile hoteli kama zinafanana na jinsi ambavyo ziliombewa mwanzo, wakati wa kupata *registration* ama wakati wa kupata hiyo leseni. Nilidhani hayo ni maeneo ambayo ni ya msingi sana kuyaangalia.  Ninakumbuka, Serikali yetu kwa upande wa leseni za masuala ya biashara huko nyuma, kila biashara tulikuwa tunakata kila mwaka unakwenda unakata leseni.  Kama una duka, mashine ya kusaga au una shughuli yoyote, kila mwaka unakwenda unakata leseni, lakini Serikali baada ya kulitafakari hilo, ikaamua kwamba, leseni zile zitakuwa zinapatikana mara moja wakati mtu anaanzisha ile biashara.  Kwa hiyo, nilidhani na hili eneo pia la leseni, liangaliwe ila usikae muda mrefu lakini kuwepo na ile haki ya maafisa wa umma kuweza kwenda kukagua na kuangalia kadri taratibu zetu za nchi zinavyotuelekeza.

Katika Muswada, kifungu cha 44 pia kimeelezea juu ya masuala ya *complaint,* kwamba, endapo mtu ana *complaint,* anaweza akapeleka zile *complaints* zake kwa *Director* wa Masuala ya Utalii.  Ipo haja baadhi ya kazi zake ziweze kukasimiwa kwa maafisa wa umma wanaohusika katika hiyo sekta katika Halmashauri zetu ili masuala haya ya utalii, yazingatiwe na mambo mengine yaende kwa uharaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile niupongeze sana Muswada huu, kwa sababu kweli kabisa Muswada huu umerekebisha ule wa zamani uliokuwepo. Umezingatia sana nafasi ya Mtanzania, kifungu cha 57 kimeeleza wazi kwamba, yatakuwepo maeneo ambapo huduma hizi ya masuala ya utalii zitafanywa na Watanzania peke yake.  Kwa hiyo ni muhimu tukaangalia yale maeneo ambayo ni muhimu kama ni ufukweni au yale maeneo ambayo ni nyeti kwa ajili ya usalama na *security,* yakafanyika na Watanzania na sio kufanywa na wageni, yaani *foreigners.*  Pamoja na ile *policy* ya uwekezaji, *Tanzania Investment Centre,* wana *policy* ya masuala ya i*nvestment,* pale inapobidi tusisitize sana suala la ubia.  Suala la ubia ni la muhimu sana, isije ikawa hoteli kubwa zote zinamilikiwa na wageni.  Unakwenda kwa mfano, Zanzibar unaambiwa hii hoteli ni ya Muitaliano, hii ya Mpalestina, hii ni ya mtu kutoka Saudi Arabia, suala la sera ya *partnership* katika masuala haya nayo ni jambo la msingi sana likazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaipongeza Wizara kwa shughuli hizo za uzalendo, lakini yapo mambo mengine ambayo ningeomba tuyazingatie sana. Lipo tatizo linailotwa *leakage; leakage* ni pale ambapo kunakuwepo na Shirika la Masuala ya Utalii, ambalo linakuwa na ofisi zake ndani ya nchi, wana-*organise* watalii kuja Tanzania na hivyo, wanapokea hela kule kule nje ya nchi, kwa mfano, Marekani ama Uingereza na vilevile wanatumia ndege za huko huko Uingereza. Kwa mfano, anatumia shirika la nje, kwa hiyo, hela inayokuja Tanzania ni kidogo sana na wakati mwingine wanasema kuna kitu kinaitwa *all inclusive vocation package,* yaani kila kitu kinalipiwa kule kule. Kwa hiyo, wakija chakula cha asubuhi na usiku kimeshalipiwa, lakini mbaya zaidi kimelipiwa kwenye lile Shirika la Utalii ambalo Makao Makuu yake au *branch* yake iko nje ya nchi. Kwa hiyo, kinachopatikana Tanzania kinakuwa ni kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonyesha kwamba, katika nchi zinazoendelea, katika kila dola mia inayotumika ndani ya nchi inayoendelea katika ile nchi inabakia dola tano tu. Kwa hiyo, jambo hili ni muhimu sana tukaliangalia, maana yake wengine wanapokuja wanasema wana matatizo na hivyo inabidi kila kitu walipie nje. Wakati mwingine hata vyakula hasa vile vinavyoharibika haraka, wengine wanakuja wanakwambia sisi tuna matatizo ya *diabetic*, tunahiaji vyakula vyenye *low calories,* kwa hiyo, hawawezi kutumia vyakula vyetu na hivyo wananchi wetu hupata hasara; nyanya za Ilula hazinunuliwi, vitunguu vya Ruaha Mbuyuni havinunuliwi, viazi vya Njombe havinunuliwi, kila kitu kimeshalipiwa na vinakuja kwenye *package* kutoka nchi za nje. Hili ni jambo ambalo ni muhimu sana tukaliangalia ili kuweza kuiimarisha sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo, naipongeza tena Wizara kwa kuleta Muswada huu, lakini vilevile niwakumbushe kifungu cha 20 ambacho kimeeleza juu ya *appeals* za *authorities* kwamba, kutakuwa na wajumbe. Kuna kifungu pale kinaelezea kwamba, kutakuwepo na Mwanasheria, lakini Mwanasheria huyo atatokea *TLS*, yaani *Tanganyika Law Society*. Sasa pale ninaishauri Wizara waseme tu kwamba, kutakuwepo na Mwanasheria na vigezo wataviweka kwa ndani visiwe kwenye hii sheria, kwa sababu sasa hivi kuna Mashirika mengi sana ya Wanasheria; kuna *Tanzania Women Lawyers Association* na vyombo vingine mbalimbali vya Wanasheria. Kwa hiyo, waseme kwamba wanahitaji Mwanasheria lakini wakishasema atatoka *Tanganyika Law Society,* hapo tayari ninaona wanakuwa wameweka vigezo ambavyo vinakuwa vigumu baadaye kuvi-*reconsider* na hii ni sheria ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, ninaomba niunge mkono hoja hii na niunge mkono kwa kuomba hayo niliyoyasema yazingatiwe. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nilisema nitamwita Mheshimiwa Brg. Jenerali Hassan Ngwilizi, ninafikiri hayupo; nitamwita Mheshimiwa Bernadeta Mushashu naona hayupo. Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o halafu Mheshimiwa Manju Msambya ajiandae kama yupo, atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Galinoma.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Muswada wa Sheria ya Utalii. Ninaomba niungane na wenzangu, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kazi nzuri wanayoifanya na hasa katika kuboresha masuala ya utalii hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yameshazungumzwa na wenzangu, lakini ninapenda nizungumzie suala la kuoanisha maeneo ya utalii. Yapo maeneo mengi sana, lakini ukiangalia Waziri alipokuwa anawasilisha hoja hii, alioanisha maeneo ambayo yameshatajwa ya utalii hasa ya utamaduni ambayo yataendelezwa. Nilikuwa ninafikiri kwamba, kuna maeneo mengi, nikichukulia Mkoa wa Iringa, sikuona umetajwa hapa wakati ninaelewa kwamba, katika mkoa huu kuna maeneo kama Isimila ambayo ni ya historia ya kale na yanaweza yakaiingizia kipato kikubwa sana nchi hii; maeneo kama ya Kalenga na Lugalo ambayo yana historia kubwa sana lakini hayaendelezwi na wala hakuna anayeelewa kwamba haya maeneo ni ya muhimu. Yapo maeneo ambayo ukiangalia, kama yangeweza kuendelezwa, yangeliingizia nchi hii pato kubwa sana. Sasa nilikuwa ninafikiri kwamba, kwa vile kuna maafisa utalii huko kwenye mikoa yetu, basi waoanishe kila Wilaya ni maeneo gani yaliyopo ambayo yanaweza yakatumika kama vivutio vya watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia maeneo kama Makete, eneo la Kitulo lina ndege wanaohama kutoka dunia yote kwenda kupumzika pale hasa wakati kunapokuwa na barafu, sasa hivi ukienda utawakuta ndege wazuri sana kule. Maua ambayo hayapo hata dunia hii lakini hayajaoanisha hapa kama ni *National Park* ambayo inaweza ichukuliwe umuhimu wake na kuwa kivutio kikubwa kwa watalii hapa nchini. Hapa ukiangalia maeneo yenyewe ya Makete yalivyokaa ile milima yenyewe tu pia ni vivutio. Ukienda nchi za wenzetu kivutio cha utalii unaambiwa tu ni milima, watu wanakwenda kuangalia hakuna hata kitu kikubwa sana lakini sisi tuna milima mikubwa sana kwa mfano ukienda Makete utashangaa ile milima iliyokuwa mizuri lakini kwa sababu ni pembezoni hatuangalii kama tunaweza kuboresha, kuweka kiwanja kidogo au kuboresha kiwanja kilichopo, kiwanja kilichopo Njombe kikatumika kupeleka watalii kule na kujenga barabara ya lami kutoka Njombe hadi Makete.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia maeneo ya Ludewa, kwa mfano, Mwambao ule wa Manda, wao wanapaita *beach*, lakini sisi hatuoni kama panahitaji kuendelezwa. Mimi nilikuwa ninafikiri, kwa sababu tunakwenda kwa hatua, tungekuwa tumeyaoanisha tuyajue maeneo haya, halafu tutakapokuwa tunayaendeleza basi tunayaangalia. Maeneo ya Njombe kwa mfano, Nyumbanitu ni mahali pa historia kubwa sana, lakini hatujaweza kuangalia tutaendelezaje maeneo haya ambayo yana historia kubwa ya vizazi vilivyopita na vizazi vilivyopo ili historia hii isipotee na pia uwe utalii ambao unatuingizia fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji pia kutangaza utalii uliopo hapa nchini. Ukienda nchi za wenzetu, mgeni ukifika, kwa mfano, labda ni Wabunge wameenda kutembelea mahali, mkifika cha kwanza kabisa atakaye-*host* wale wageni ni Waziri wa Maliasili na Utalii na pale mnaonyeshwa utalii uliopo kwenye nchi ile na vivutio vyote vilivyopo. Sasa niaomba kutoa wito kwamba, Wizara itengeneze kabisa *DVD* au

chochote ambacho wageni wanapokuja basi wapewe, kikielezea maeneo ya utalii ambayo upo. Viongozi wakienda nje na kokote tunapokwenda, tuzungumzie utalii wa nchi yetu ambao tutakuwa tumetengenezewa *document*, ambayo tunaenda nayo tunaonyesha maeneo mazuri tuliyonayo, ambayo ni kivutio kikubwa na yako kila sehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nzima hii ina bahati ya kuwa na vivutio vingi sana, ambavyo tukivionyesha tunaweza vikaweza vikasaidia kuongeza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni jinsi Mungu alivyotujalia kuwa na akili ya kutumia akili na mikono yetu. Vinyago vile vinavyochongwa na ndugu zangu Wamakonde viko nchi gani hapa duniani; tumeoanishaje hawa wachonga vinyago kuwaweka mahali ikawa pia ni sanaa ambayo inaweza ikatumiwa na wanaochonga vinyago wakafaidika? Wao wanachonga kwa pesa ndogo, halafu watu wengine wanakwenda kuvinunua na kufaidika, wanaochonga wanaishia kila siku kuwa maskini, unakuta hawana hata viatu lakini wanafanya kazi kubwa sana ya kufikiria kuchonga vile vinyago. Wizara inaangaliaje hii fani ambayo Watanzania wamezaliwa nayo, vipaji walivyopewa na Mwenyezi Mungu na kuweza kuviendeleza, wakawa na sehemu ambayo ni kivutio hata watalii, wakija wakute jinsi wanavyotengeneza? Hilo ni jambo lingine ambalo tunatakiwa pia tuliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni hoteli zinazojengwa; ninaona kwa vile Wizara imesema itaangalia na wazalendo, tuanze kupewa elimu sasa hivi kabla hatujajenga hoteli sisi wazalendo, maana tutajenga hoteli ambazo hazina madaraja halafu watakuja wageni ndiyo watajenga hoteli zenye madaraja. Ninafikiri tuanze kuelimishwa, kama mtu anataka kujenga hoteli basi aelezwe kwamba, hoteli ya nyota moja inakuwa na vigezo hivi, nyota mbili hivyo hivyo mpaka nyota tano, ili anapojenga ajenge kwa vigezo, badala ya kujenga halafu baadae ndiyo inakuja kuoneka hoteli yake labda haikidhi viwango vya kuwa na nyota zile zinazostahili. Hii itasaidia sana, kwa sababu kama tutajenga hoteli basi na watalii watakuja mikoani kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyozungumza wenzangu waliotangulia, Mkoa wa Iringa una mbuga kama *Ruaha National Park*, kuna Milima ya Udzungwa na hayo mengine ambayo wenzangu wameyataja na mimi nimeshayataja lakini tatizo kubwa ni kwamba, hatuna hoteli. Endapo wananchi wangeelimishwa wakaweza kujenga hoteli, basi na sisi tungepata watalii ambao wanafurika Kaskazini halafu huku Kusini hawaendi wakati na sisi tunavyo vivutio vya kihistoria, ambavyo havipo sehemu nyingine ili tuweze kuwa na uwiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, ukiangalia kwenye huo Muswada, umezungumza tu kiujumla Bodi zitakazowekwa, lakini sikuona suala la jinsia limetajwa pale; isije ikatokea wakapangwa Wajumbe wa Bodi wote wakawa wa jinsia moja na nina uhakika wengi watakuwa ni wanaume, kama vile sisi wanawake kwenye utalii hatuhusiki. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anaangalia hizo Bodi basi suala la jinsia liangaliwe na aongeze kipengele kwamba, suala la jinsia litaangaliwa kwenye hicho kipengele cha Wajumbe watakaokuwa kwenye Bodi ambazo zitaundwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu uchangiaji wa maeneo ambayo sehemu za utalii zilipo. Kumekuwa na uchangiaji, lakini ninafikiri sasa uchangiaji huu nao ungewekwa kwa asilimia, kwa sababu unaweza kuchangia labda mtajengewa darasa moja basi mkasema wamechangia. Ninafikiri pia tuangalie uchangiaji huu kwenye hayo maeneo ambako aidha hoteli hiyo ya kitalii ipo au hizo shughuli za kitalii zipo, iwe ni kiasi gani ili kuweza kuhakikisha kwamba, jamii zinazozunguka eneo hilo pia wanafaidika na ule uwekezaji unaokuwa kwenye eneo linalohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu utalii wa ndani. Ninapenda kuiomba Wizara, iongeze pia kipengele cha kuhamasisha utalii wa ndani. Utalii wa ndani ina maana kwa sisi wananchi kuweza kutalii, kwa sababu tuna maeneo ya utalii lakini sisi wenyewe hatutembelei. Tupatiwe elimu ya utalii, labda sijui liwepo somo shuleni ambalo linazungumzia kujua vivutio vilivyoko ndani ya nchi yetu ili tuweze kuwa na tabia ya kuweza kufanya utalii. Unaweza kukuta watu tunakaa maeneo yale yale, lakini mtu haelewi hata hiyo *National Park* inafanana vipi! Sasa ninafikiri tuanze kuvutia utalii wa ndani ili tuweze kuongeza mapato. Fikiria Watanzania wote tuliopo hapa, hata robo tu tukiweza kufanya utalii kwa mwaka, mapato yataongezeka, lakini tumeachia sehemu kubwa ya nje. Wizara inajitahidi kuvutia wananchi kuweza kufanya utalii, lakini ninafikiri itafutwe mbinu nyingine ya kuweza kuhamasisha wananchi waweze kuwa watalii ndani ya nchi yao na kuelewa vitu mbalimbali ambavyo viko katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninapenda kusema kuwa, ninaelewa kwamba, Serikali inafanya juhudi ya kuhakikisha kwamba, barabara ya Dodoma Iringa inajengwa. Ninapendeza barabara hii iharakishwe kujengwa ili iweze kuwa njia fupi ya watalii kuweza kufika kwenye maeneo ya huko kwetu, kwa sababu watalii watatoka South Africa mpaka watafika Dar es Salaam, hata huko Arusha wanakokwenda watapita kwenye maeneo yetu kwanza halafu ndiyo waende huko. Kwa maana hiyo, watakuwa wameweza kutalii nchi nzima, kwa sababu barabara zitakuwa zimeboreshwa na kipato pia kitaongezeka. Barabara hizi mpya zitakapokuwa zinajengwa, kama alivyokwishaelezea Mheshimiwa Pindi Chana, zizingatie hiyo miundombinu mingine ya kupumzikia, kama za zamani zilijengwa bila kuzingatia hilo, hizi mpya zinazojengwa basi zizingatie vituo watakapokuwa wanapumzika abiria.

Kwanza, wananchi kama wananchi, wahamasishwe kabla barabara haijajengwa, wajitokeze wajenge, kwa mfano, unatoka Dodoma mpaka Iringa, kiwepo kituo kimoja pale katikati, kinatosha kabisa wananchi kupumzika badala ya kuwa na tabia hii ya kwenda porini na kufanya kama utamaduni; unaposafiri mnatawanyika; baba, mama na watoto wote kwenda porini ambapo inatupunguzia heshima, na watoto wadogo ukiwa nao kwenye gari wanasema mama tunataka kwenda kuchimba dawa. Wanafikiri labda ni msamiati wa kawaida. Kwa hiyo, ninafikiri barabara zote zinazojengwa ziwe na hivyo vituo na ambazo zimeshajengwa sasa zifanyiwe ukarabati, wananchi watangaziwe wawekeze vituo hivi. Tuna uhakika vitalipa, kwa sababu kila atakayepumzika pale, atatumia zile huduma kwa kulipia na pia biashara itakuwa nzuri kwa sababu itakuwepo mahali ambapo mtu anaweza kupata chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninapenda niishukuru na niipongeze Wizara, kwa juhudi kubwa wanazofanya na niipongeze Serikali kwa kuboresha utalii. Nina hakika kwamba, siku moja Tanzania yenye watalii wengi Barani Afrika inawezekana, kinachohitajika ni utashi kama huu tunaouona na kwa juhudi zinazofanyika, mabadiliko yatapatikana na utalii itakuwa ni mojawapo ya sekta ambayo itatuingizia kipato kikubwa, lakini pia tuangalie utalii wa mali inayozalishwa kutoka Baharini. Nchi za wenzetu hata vile vipengele vidogo, masimbi yale ni fedha, sisi tunayaachia tu. Kwa hiyo na hayo tuyaangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi kwa ufupi, niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kabla sijaendelea, kama ilivyo ada, niungane na Wabunge wenzangu, kutoa salamu za pole kwa niaba wa Wananchi wa Jimbo la Kigoma Kusini, kutokana na kifo cha Mbunge mwenzetu, Marehemu Benedict Losurutia. Pole hizi ziwafikie wanafamilia na Wananchi wote wa Jimbo la Kiteto.

Kadhalika ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare, kwa kujiunga kwenye klabu yetu hii. Ninaamini atachanganya uchungaji na siasa na atamudu tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ni naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kutuletea Muswada huu. Mimi nitakuwa na machache sana, lakini katika hayo machache sana, ninaomba nieleze moja ya vipengele nilivyosoma; ibara ya pili ya Muswada kuna mahali panazungumzia Kamati ya Ufundi ya Ushauri, ambayo itakuwa inaishauri Wizara na Waziri mwenyewe kuhusu masuala ya utalii. Ninaomba Mheshimiwa Waziri kwanza, ajihesabu kwamba ni mtu mwenye bahati; michango yote iliyotolewa na Wabunge hapa tayari ameshapata Kamati ya Ushauri wa Ufundi kutoka Bungeni. Kwa hiyo, la kwanza ningemwomba azingatie ushauri aliopewa na Waheshimiwa Wabunge ili umsaidie kufanya Muswada huu utakapokuwa Sheria, ufanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nilifuatilia asubuhi Mheshimiwa Siraju Kaboyonga alipokuwa anazungumza; katika mengi aliyoyazungumza alisema jinsi ambavyo Magharibi mwa nchi kunavyosahaulika sana katika masuala ya utalii. Nimefarijika niliposoma taarifa ya Mheshimiwa Waziri, alipokuwa anawasilisha, aliizungumzia njia maarufu iliyopitiwa na Dr. David Livingstone, ambayo inaanzia huko Bagamoyo inakwenda mpaka Ujiji Kigoma. Njia hii, ninaamini Wizara kama itatekeleza Muswada huu utakapokuwa Sheria kama ilivyokusudia, itasaidia kufanya sehemu ya Magharibi nayo ifaidike na sekta hii ya utalii. Tunafahamu yapo maeneo kongwe katika nchi hii, kwa mfano, kule Zanzibar kuna Mji Mkongwe, tunayo Mikindani, tuna Bagamoyo, lakini tunayo Ujiji na kwa taarifa ya wengi, ningependa watu waelewe kwamba, Ujiji ni Mji wa Kale na ni Mji wenye sifa zote za kuhifadhiwa.

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Mheshimiwa Joseph Simbakalia, ameonyesha azma hiyo. Ameamua tuwe na Ujiji Kongwe na Ujiji Mpya, ninadhani atakuwa anawasaidia watu wa Wazira ya Utalii kuweka vivutio. Ujiji mpya ni ile ambayo inajengwa sasa kuzunguka Mji wa Ujiji ule wa zamani na ameweza kukaa na wataalam wake kutafuta namna ya kuwashauri wenyeji wenye nyumba zao katika Ujiji ile ya zamani, wasipate tamaa ya kuzivunja na kujenga majumba mapya kwa kudhani kwamba, tunasema kipya kinyemi, japokuwa ni kidonda hapa. Yale majumba ya zamani, yakitengenezwa vizuri na kuimarishwa, yenyewe tu ni kuvutio. Kwa hili, niipongeze Wizara, yapata kama miezi mitatu iliyopita, kuna watu wamekwenda wamefanya uchunguzi wa Mji ule na wameandika taarifa ambayo ninaamini itaisaidia Wizara namna ya kuhifadhi Mji ule ili uwe ni sehemu ya Utalii.

Ninaipongeza Wizara, inajenga kituo pale kwenye sehemu ambapo Dr. David Livingstone alikutana na Martin Stanley. Kituo kile kitatusaidia sisi kuwa ni kivutio cha utalii katika sehemu ya Magharibi lakini haitoshi, tungeomba kuwe na juhudi za makusudi za kufanya eneo la Magharibi mwa nchi, liwe ni kivutio cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu alichangia asubuhi hapa akasema, wapo twiga weupe, ambao ni kivutio kama maeneo ambayo twiga hao wapo, yatawekewa miundombinu mizuri ya usafiri, lakini mtu huyo alipokuwa anazungumza, mtu mwingine akaeleza kwa utani hapa hao twiga si zeruzeru tu hao. Sasa kuwa na twiga zeruzeru ni kivutio. Sisi kule Kigoma tunazo sehemu mbili za Hifadhi; tunayo Gombe na Mahale. Mahale kuna sokwe weupe, ambao ninaamini na kwa maandiko yote niliyokwishasoma, hawajapatikana sehemu nyingine yoyote duniani ila wako Mahale tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa bahati mbaya, mtalii anayetaka kwenda kuwaona sokwe wa Mahale, atakwenda kuwaona kwa gharama kubwa kiasi kwamba, wakati mwingine anasema hakuna haja ya kwenda. Pengine katoka Ujerumani kwa ndege anafika Dar es Salaam, anapanda Precesion Air au Air Tanzania anakwenda Kigoma, kutoka pale sasa anaambiwa aingie kwenye mtumbwi ambao yeye mwenyewe hajawahi kuingia, ataamua kurudi tu. Tunashukuru, zipo juhudi zinafanywa za kutengeneza barabara Kigoma Mjini kwenda Kalya kupitia sehemu za Mahale, ambako mbuga hiyo ipo lakini ile *speed* ya barabara hiyo ni ndogo sana.

Wananchi wamefanya kile walichoweza na kwa hapa nitambue juhudi zilizofanywa na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma wakati ule Mheshimiwa Ukiwaona Ditopile Mzururi wa Ramadhan. Alisimamia vizuri ujenzi wa barabara ile lakini ninaomba Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia *TANAPA*, iunganishe nguvu pamoja na Wizara ya Miundombinu, wampe uwezo Meneja wa *TANROAD* Mkoa wa Kigoma ili asimamie ujenzi wa barabara ile na hasa kigumu sana ni madaraja. Huko nyuma kwenye vikao vyetu vya Kamati ya Maendeleo vya Mkoa, tuliwahi kuzungumza na tukawa tumeshauriana na watu wa *TANAPA* wakasema, wapo tayari kuchangia kama Wizara itapeleka kauli thabiti, kwa sababu wao watafadika zaidi na barabara ile kwenye misingi ya utalii, kwa sababu watalii wengi watakwenda kwa kuwa usafiri wa uhakika utakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema nitazungumza kwa uchache tu, nimeusoma Muswada na unazungumzia utalii wa vijijini. Bahati nzuri, tarehe 5 Januari, 2006, binafsi nikiwa ninafungua semina ya *TAKARE* pale Kigoma, nilizungumzia umuhimu wa utalii wa vijijini, ambao vilevile unawahusisha na wakazi wa maeneo hayo. Ninaomba kuwa na hamu au azma ya kupata pesa kutokana na sekta ya utalii, kisiwe kichocheo cha kutuharibia mila na utamaduni wetu. Huko nyuma nilishawahi kuwa Mjumbe wa Bodi ya Kampuni ya Simu, tulikwenda kufanya kikao kimoja kule Zanzibar, Mawimbini Hoteli; niliyoyaona kule siwezi kuyahadithia hadharani; yanachafua na yanachefua; wananchi wetu wanaiga yale. Maana ipo ndege inatoka Milan moja kwa moja mpaka Unguja na wanapokuja tangu wanaposhuka Kiwanja cha Ndege, sasa sijui kama wenzetu wa Unguja zipo sheria au hakuna au ndiyo hicho kivutio cha utalii kinasema tuachane na utamaduni wetu?

Badala ya kuwa na utamaduni mzuri, watalii wanakuja kufundisha watu wetu kutembea uchi. Sasa kweli tunahitaji pesa zinazoletwa na watalii, lakini hatuhitaji fedha hizo zije zituharibie mila na desturi zetu. Kwa hiyo, ninajua hii Sheria itaweka kanuni, maana kwenye Sheria sikuona popote pale palipozungumzia vikwazo au namna gani tutawadhibiti watu wanaokuja kutalii lakini kuja kwao kukawa kunaharibu mila na tamaduni zetu. Sasa pengine kanuni za Sheria hii zisaidie basi kuweka masharti hayo. Tunahitaji pesa, lakini tunao utu wetu ambao ni pamoja na mila na desturi zetu, visaharibiwe kwa tamaa ya pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, sikuwa na mambo mengi ya kueleza, baada ya hayo niliyoyasema ninaunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, nami niweze kujumuika na wenzangu kuchangia Muswada huu. Ninampongeza Waziri, kwa kutuletea Muswada huu kwa wakati muafaka na kwa maana hiyo, ninaunga mkono toka mwanzo mpaka mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo mfupi, ninaomba nichangie katika maeneo mawili. Kwanza, nitachangia kuhusu Muswada wenyewe na pili nitazungumzia kwa ujumla suala zima la utalii. Nikirudi kwenye suala la Muswada, pamoja na kwamba wenzangu wengi wamezungumzia mambo mengi sana na kwa kweli unapozungumza mwishoni namna hii, wenzio wamekwisha kufilisi, huna pointi za kutosha au unarudia yale yaliyozungumzwa. Wazungu wangesema; "*He who laugh last laughs best.*" Pengine hii inaeleza kwa nini nina wasiwasi kidogo. Hata hivyo, kuna swali moja ambalo ninafikiri ingawa imetajwa hapa na pale, lakini halikutiliwa mkazo wa kutosha, nalo ni la utafiti. Katika nchi nyingi zote ninazozifahamu mimi, suala la utalii haliwezi kuepuka utafiti. Utafiti kwa maana ya kujua historia ya mahali, kwa maana ya kujua utamaduni kama nyenzo ya elimu kwa kizazi kilichopo na vizazi vijavyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninashauri kwa kifupi tu kwamba, Wizara hii katika Sheria yake hiyo, ijitahidi kuhusisha suala zima la utafiti. Kwa bahati mbaya sana, nchi hii haina utamaduni huo, angalau kwa kiwango cha kutosha. Mambo mengi sana yametokea

katika nchi hii kabla na baada ya uhuru, lakini si rahisi kupata maandishi ambayo yanaelezea mambo hayo na hii ni kwa sababu hatuna utamaduni wa kuandika vitabu na vitabu haviandikwi bila utafiti. Kwa maana hiyo, ninashauri tutumie utalii kama chombo kimojawapo cha kuhakikisha tunakuwa na maandishi yatakayotusaidia mbele ya safari, sisi pamoja na vizazi vijavyo. Kwa hiyo, ninashauri suala hili lizingatiwe kwa umakini.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, katika Muswada huu ningependa nirudie waliyozungumza baadhi ya wazungumzaji waliopita, nalo ni utalii wa ndani. Utalii wa ndani tumeuacha kabisa. Sheria hii inalenga watu wanaotoka ng'ambo; Ulaya na Mashariki ya mbali, lakini sisi wenyewe hapa hatuweki mkazo wa kutosha. Vijana wetu hawajui utalii ni nini, hawajui wanyama, hata nchi hii hawaielewi sawa sawa, ninadhani tungekuwa na utaratibu wa kuwahusisha Wananchi wa Tanzania katika suala zima la utalii. Kweli hawana fedha nyingi kama watalii wa kutoka nje, lakini zile fedha ndogo ndogo walizonazo, kwa sababu ya wingi wetu pia zingeweza kusaidia, sio tu kukuza utalii lakini pia kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo mambo mawili, ninapenda nizungumzie kuhusu utalii wenyewe. Kwanza, ninafurahi kwamba kuna wasemaje ambao wanatokea Mkoa wa Iringa ambako na mimi ninatokea na wamesema vizuri sana na kwa sababu hiyo nisingependa nipoteze wakati mwingi. Ninapenda kusema kwamba, hakuna ubishi kwamba utalii wetu umeelekezwa zaidi Kaskazini, maeneo mengine kama walivyosema Wabunge wengine, kwa kweli tumeyapa kitu tunaita *lip service,* hatukuwapa umuhimu unaostahili na kwangu huko ndiyo zaidi. Hatuna kabisa suala hili japo sasa hivi tunajaribu kujipanga lakini tunafanya kama kuokotezaokoteza tu badala ya Serikali kuwa na mpango wa kutusaidia sawa saw. Mnamo miaka minne au mitano iliyopita, Wizara hii iliajili Tume moja ya wataalam kutoka nje, ikabainisha mahitaji ya utalii katika Nyanda za Juu Kusini. Ilieleza vivutio vyote kuanzia Dar es Salaam, Pwani yote ile ya Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, ikazunguka mpaka huku kwetu Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ningesisitiza kwamba, kwa mapendekezo hayo, mpango huo ungeitwa *Southern Tourism Circuit*. Nilitegema kwamba, Wizara hii ingekuwa na mipango thabiti ya kutuelekeza tufanye nini na Serikali ifanye nini ili kwa pamoja tuweze kukuza sekta hii katika maeneo yetu. Sasa kwa bahati mbaya kabisa, msukumo huo haupo. Kama nilivyosema, tunajaribu kujipanga, lakini hatuna ushauri au tuseme utaalam, tunategemea sana Wizara hii itusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, walitutumia mshauri wa utalii, ambaye tulikuwa naye mpaka juzi juzi hapa, kwa bahati mbaya Mungu amemchukua katika ajali ya gari, sijui kama tunaye mwingine badala yake. Ninataka kusema hapa kwamba, tuna vivutio vingi sana katika maeneo yetu. Ukianza vivutio vilivyoko pwani ambavyo ndiyo *Southern Tourism Circuit,* ziko *National Parks* kadhaa na pia mbuga za wanyama, labda nitaje tu; *Mikumi National Park, Selous Game Reserve, Kitulo National Park*, *Ruaha National Park*, *Katavi National Park* na *Udzungwa National Park.* Ninazitaja hizi si kwamba zote ziko Iringa, lakini hizi ndiyo zingeweza kuunganishwa pamoja ikawa ndiyo *Circuit* kama vile ilivyo ile ya Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna vivutio vingine vya historia kama alivyovitaja Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o; kuna Isimile ambako kuna Makumbusho pale ya watu ambao waliishi miaka milioni kadhaa iliyopita na ingeweza kuwa ni chombo kimojawapo cha utafiti; kuna Lugalo ambapo wengi hawajui kwa nini Lugalo pale Dar es Salaam inaitwa hivyo; inatokana na mapambano yaliyotokea kule Iringa kati ya Wahehe na Wajerumani; iko Nyumba Nitu katika Wilaya ya Njombe. Hii kama alivyosema ni sehemu ambayo ina historia yake na utamaduni wake. Hivi ni vivutio vingi sana ambavyo vingeweza kutusaidia huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningetegemea kwamba, Serikali baada ya kutambua kwamba, mpaka sasa utalii umeegemea zaidi Kaskazini, si kosa la mtu yeyote, ni tatizo la historia. Kweli huko Kusini au hata Magharibi, hatuna Kilimanjaro, lakini kuna vitu vingine badala yake, ambavyo vingeweza kukuzwa na kuwa msingi wa utalii. Sasa ninashauri kwamba, tusirudie kosa tulilofanya siku za nyuma. Tuzinduke, tuchukue hatua zinazostahili, kujenga na kuhimiza ujenzi wa miundombinu kama walivyobainisha wenzangu. Kubwa katika miundombinu ni barabara. Barabara ya kufika huko ni ngumu sana. Viwanja vya ndege; tuna kiwanja Nduli pale, hakifanyi kazi kwa miaka mingi tu na nilikuwa ninajaribu kuangalia kule Wizara inayohusika, kwa nini, hakuna sababu maalum. Kipo Kiwanja Ruaha kule, ndiyo kungeweza kuwa mahali pa kuanzia kutawanya watalii kwenda sehemu nyingine hizi ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa ambalo pengine linatukwamisha sasa hivi ni ukosefu wa malazi yanayostahili (hoteli). Hapa ningependa nipendekeze kwamba, katika matangazo ambayo ninajua yanatolewa, lakini matangazo yanayotolewa kwa heshima zote ni yale yanayohusu sehemu zilizopo sasa. Sehemu mpya hakuna, hata hawa jamaa akina *Surivan Foundation Fund* ambao ninadhani watakuja baadae mwaka huu, wanapelekwa huko ambako tayari utalii ulikwishastawi; kwa nini wasiwapeleke sehemu mpya, maana yake hawa wanataka kuwekeza katika sekta hii wanawekeza katika maeneo ambayo tayari yamekwisha wekezwa? Vilevile matangazo yetu yawe *local*, yaani yawahusishe wawekezaji *local* wa hapa hapa waweze kujenga hoteli na mambo kama hayo. Tukitegemea tu watu wa nje, itatuchukua pengine karne nyingine kabla hatujaweza kufika mahali.

Kwa hiyo, ninashauri kwa nguvu zangu zote, tujaribu kadri ya uwezo wetu, kutengeneza miundombinu na hasa sisi kule mikoani watuambie nini tunapaswa kufanya, halafu tuunganishe nguvu zetu pamoja na zile za Serikali, ninadhani tutaweza kufika mahali. Tukienda hivi hivi tu, pengine si rahisi kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye suala moja dogo lakini muhimu; nimeona katika *section 59*, Bodi au Waziri anapewa fursa au tuseme mamlaka ya kuanzisha ushuru. Ninafikiri ni vizuri, lakini ningependa kutahadharisha, hizi *levy* mara nyingi *TANAPA* wanatoa kwa vikundi au vijiji vilivyoko mpakani. Ninadhani ni vyema ieleweke kwamba, rasilimali hizi ni za wananchi wote kwa pamoja katika wilaya. Kwa maana hiyo, kama inatolewa fedha, misaada au ushuru, basi ipelekwe kwenye

Halmashauri za Wilaya. Wao waweze kuhakikisha kwamba, rasilimali zao hizo matokeo yake yanasaidia wananchi wote kwa ujumla, badala ya kubagua na kusaidia vijiji vilivyoko kwenye mipaka au vikundi vilivyojiweka katika hali ya kuweza kupata hiyo mikopo, wengine ambao hawana wanyama katika maeneo yao wasipate chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya mafupi, ninaomba nirejee tena, ninashukuru sana Muswada huu umekuja kwa wakati na nitau-*support* moja kwa moja na vilevile ninaunga mkono katika hatua zake zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Muswada huu wa Utalii jioni hii ya leo. Kwanza kabisa, ninapenda niipongeze Wizara kwa kutuletea Muswada huu ambao ni muhimu na una lengo kubwa la kuboresha shughuli za utalii katika nchi yetu na hivyo kuinua mapato ya taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni muhimu sana na hasa ukizingatia kwamba, katika miaka kadhaa iliyopita, hii Sekta ya Utalii ilikuwa ikichangia lakini kwa kiasi kidogo na ilikuwa ikichukua nafasi ya tatu ukianzia kilimo, inafuatia madini, ikawa inafuatia utalii. Baadaye pato hili limekuwa likiongezeka na kwa sasa ninadhani lipo katika nafasi ya pili baada ya kilimo. Labda nieleze kwa kifupi, mchango ambao unachangiwa na sekta hii ya utalii kwa kulinganisha, inachangia karibia asilimia 30 ya mapato ya ndani na kwa mapato ya jumla, inachangia asilimia kama 20 hivi. Kwa hiyo, Muswada huu ni muhimu na umejumuisha wadau makundi mbalimbali na hivyo tukishirikiana kwa pamoja, ninaamini kabisa kwamba, tunaweza tukavuka hata hii asilimia 20 ya mapato yote ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitapenda kupoteza muda mwingi kwa sababu ninaona ni mengi sana yamezungumzwa, ambayo yanaweza yakawa ni kama marudio nikiendelea kuyazungumza. Ningependa nizungumzie sehemu ya pili, kifungu cha sita ambacho kinahusu kazi za Idara ya Utalii; ziko nyingi hapa kuanzia (a) mpaka (q), lakini ningependa kujikita sehemu au kipengele cha (g) na (l) ukurasa wa 8 hadi wa 9. Kama msemaji aliyepita alivyosema, alijaribu kuonyesha kwamba, hakuna suala la utafiti katika sheria hii. Kipengele hiki cha (g) kinazungumzia, ninaomba nisome kama ilivyoandikwa, moja ya kazi za hii *division* ya utalii; *"to facilitate research in tourism, related subjects and to compile and publish information relevant to the tourism industry."*

Kwa hiyo, hiki ni kipengele muhimu sana, ambacho kama kweli Idara hii ya Utafiti itakitekeleza ipasavyo, kwa kweli itasaidia katika maeneo mengi na mojawapo inaweza ikasaidia sana katika sehemu ya 9, kifungu cha 56, ukurasa wa 26, ambao ni wajibu wa Mheshimiwa Waziri kupanga au kutunga kanuni.

Kwa hiyo, ninadhani hili ni suala la muhimu sana kwa sababu bila utafiti, upo uwezekano kwamba, kanuni zikatungwa, lakini kumbe ukakuta hazitekelezeki. Kwa hiyo, inatakiwa utafiti wa kina na bahati nzuri kipengele hiki kipo. Vilevile bila utafiti, katika shughuli hii ya kutunga kanuni, pengine ikatokea mabadiliko ya mara kwa mara ambapo si lazima. Ninadhani sote tunafahamu kwamba, mabadiliko ya mara kwa mara ya ghafla, yanaweza yakapelekea pia utekelezaji wa sheria usiwe mzuri, kwa sababu siyo rahisi taarifa kuwafikia wale wanaohusika haraka mara baada ya kubadilisha kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuishauri Wizara au Idara kwamba, ijitahidi sana kuwa na ubunifu katika shughuli hizi au katika kutoa taarifa zile za utafiti. Ubunifu ni kitu kimoja muhimu na kama msemaji aliyepita alivyosema, huu mkutano wa Surivan ambapo ninadhani kwa kutumia ubunifu, Idara inaweza ikapeleka taarifa mbalimbali zinazohusiana na vivutio mbalimbali katika mkutano huu ili wanaohusika au wanaoshiriki katika mkutano, waweze kufahamu ni maeneo yapi yana vivutio zaidi ya lile eneo ambalo wanakuwa wamefika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe tena Idara hii, ijitahidi kushirikiana na taasisi nyingine kwa mfano, *TAWIRI*, *TAFORI* na *TAFIRI* ili waweze kuongeza ufanisi zaidi katika shughuli hizi za utafiti au katika kutoa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuzungumzia kipengele cha (l) katika ya pili kifungu cha 6, ambayo inaelezea kuwa shughuli mojawapo ni *to identify tourist attractions and diversify tourist activities.* Hili nalo ni la muhimu, kwa sababu Idara itakapokuwa imeainisha maeneo mengi ya utalii, basi utakuwepo pia uwezekano wa kujenga hoteli katika maeneo mengine na hivyo itapelekea kupunguza ujenzi wa hoteli katika maeneo yale ambayo tunayasema ya Ngorongoro na Serengeti na hivyo kupunguza msongamano. Kwa hiyo, hili nalo ni la muhimu sana, ningeomba sasa Idara hii ikumbuke kwamba, kuna vivutio vingi kama walivyotaja wenzangu katika maeneo mengi. Kwa mfano, kwa upande wetu wa Mtwara, kuna *Makonde Plateau,* ambacho ni kivutio kizuri sana.

Ninaomba Idara ijaribu kufuatilia maeneo haya; kuna fukwe nzuri sana za mchanga mweupe, maeneo ya Msimbati na kuna maeneo ya kihistoria ya Mikindani. Idara isisahau pia kuna viboko wa maajabu sana maeneo ya Lindi, vilevile kuna maeneo mengine, Bukombe kule kuna mti mmoja wa ajabu sana na ndiyo maana nilipendekeza kwamba, Idara hii ishirikiane na taasisi nyingine za utafiti. Kwa mfano, *TAFORI* wakishirikiana nao vizuri, wanaweza wakajua ni vipi wataweza kuhusisha mti huu kama kivutio cha utalii. Hata wakishiriana na *TAWIRI* vilevile, wataweza kujua ni wanyama gani wa ajabu na kutolea taarifa ambazo zinaweza zikasaidia kuvutia watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala moja ambalo ningependa katika kipengele hiki hiki, Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake, anipatie majibu kuhusiana na uzio wa umeme ambao uko eneo la Mtwara. Ningependa kufahamu, huo uzio ni kivutio cha utalii au kuna shughuli gani ambayo inafanyika kule ndani kwa sababu eneo hili ni kubwa, hakuna anayejua kinachoendelea kule ndani na hatujui manufaa yake? Ninatambua kwamba, kama ni suala la uhifadhi, kwa kweli eneo hili limehifadhiwa vizuri sana na uoto wa asili unamea. Endapo kuna shughuli nyingine za utalii zilizopo, ningeomba nipatiwe jibu kwa sababu mwenye eneo hilo, analifuatilia mara kwa mara na hatujui anapata nini au taifa linapata nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuzungumzia katika eneo hilo hilo la kazi za Idara hii ya Utalii kuhusiana na uwezeshaji. Katika bajeti ya mwaka 2007/2008, haionyeshi kabisa kujumuisha suala la utafiti, halionekani, kwa hiyo, sijui kama kipindi

hiki Wizara itaifikiria au kama sheria hii itapitishwa kipindi hiki, watafanya vipi hizo kazi za utafiti. Kwa hiyo, ningependa kuishauri Wizara katika bajeti ijayo, ijitahidi sana kuangalia suala hili ili Idara hii isishindwe kufanya kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia nizungumzie kuhusu sehemu ya nane, kifungu cha 46(1) ambacho kiko ukurasa wa 22. Hapa panazungumziwa makosa na adhabu, lakini kiko katika kipengele cha (b).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako, ninaomba nisome, inasema kwamba; *"Without prejudice to any provisions of this Act or any other written law, any person who hinders or obstructs the Director or an authorized officer to exercise his functions under this Act, commits an offence."*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hiki kinaweza kuwa kinafikiri kwamba, pengine ni wale wadau tu au wafanyabiashara wanaoweza kuwa wamefanya hili kosa. Kwa upande wangu, ninadhani kwamba, hata Serikali yenyewe inaweza ikawa ina makosa wakati fulani. Nitoe mfano tu; *TAWIRI* ni taasisi ya utafiti ambayo iliundwa kisheria, lakini mara kwa mara Kamati inapokuwa ikiitembelea, matatizo makubwa ya kutokuwa na ufanisi katika kazi zao ni kutokana na kutokuwa na vitendea kazi na wamekuwa wakilalamikia bajeti ndogo. Sasa kwa upande wa kifungu hiki, kama ni Serikali itakayokuwa imesababisha hawa watumishi wa hii Idara kutokutenda kazi yao vizuri, sijui itakuwaje? Ningeomba Mheshimiwa Waziri, anipatie jibu wakati wa majumuisho kwamba, kama Serikali ndiyo imesababisha hivi, itakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayotaka kuzungumzia yameshasemwa, ninaomba nimalizie tu kwa kumwomba kila mdau ambaye amehusishwa katika Muswada huu, ajitahidi sana kutimiza wajibu wake kwa uaminifu mkubwa na kwa umakini na kwa kila hali ili tuweze kufikia lengo letu. Ninaamini kwamba, tutakapofanya kazi vizuri kwa ushirikiano, tunaweza tukavuka ile asilimia 30 ya mchango wa sekta hii kwa taifa na vilevile tunaweza tukatoka baada ya muda mfupi katika zile nchi maskini duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii kusema ninaunga mkono hoja. ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami pia ninapenda niungane na wasemaji waliotangulia, kwa namna ambavyo wameipongeza Wizara hii kwa kuleta Muswada huu wa Sheria hapa Bungeni ili tuweze kuridhia hatimaye Idara hii ya Utalii iweze kuboreka.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada huu kwanza ni kuboresha na kukuza biashara za utalii ndani na nje ya nchi. Ninapenda nitoe maoni yangu kama ifuatavyo: Kwanza kabisa, ingekuwa ni vyema kama vyuo vya utalii vingepewa kipaumbele kwa ajili ya vijana wetu ambao wanashughulika na shughuli hizi za kuongoza watalii na makampuni haya ya utalii. Ingekuwa ni vyema sana kuona vijana wanaopewa leseni wanapitia vyuo hivi, lakini hata madereva pia ambao wanaendesha watalii wetu wangepitia vyuo hivi. Hilo ninaomba lizingatiwe, tutaboresha shughuli hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba wenzangu wameshazungumzia mambo ya miundombinu, mimi pia ninapenda niongezee kwamba, miundombinu ambayo tunaizungumza ni pamoja na umeme na maji kwenye hoteli zetu, kwa sababu unaweza ukakuta umeme unakatika mara kwa mara, hiyo inakuwa ni adha kubwa sana kwa watalii wetu. Kwa hiyo, ninapenda pia suala hili la umeme pamoja na maji lizingatiwe, lakini pia hata magari yetu nayo yawe imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfanyabiashara yeyote anapotaka kupata faida kubwa ni lazima aweke mtaji mkubwa. Sasa umefika wakati, Wizara hii kujipanga vizuri ili kutumia pesa kwa ajili ya matangazo ambayo ni madhubuti kwa ajili ya kupata watalii wengi. Tumesema tunataka kukuza biashara yetu ni vizuri tukatumia vyombo vya habari. Vyombo vya habari, vinasambaza ujumbe kwa kasi sana. Mimi ningependa kushauri kwamba, vyombo vya habari vya kimataifa, ambavyo ni vikubwa, Wizara hii ivialike vije vitembelee vivutio vyetu ambavyo viko hapa nchini; kwa mfano, Richard Quest wa *CNN* na *BBC*, hawa ndio ambao wataweza kutangaza utalii wa nchi yetu. Ninapenda kutoa ushauri huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii umekuwa ukizingatiwa sana katika kabila moja au katika sehemu moja, lakini Tanzania hii kuna mambo mengi tofauti na mbalimbali katika mikoa mbalimbali. Kwa hiyo, ninashauri kwamba, Wizara isiangalie utamaduni wa kabila moja tu, iende na mikoa mingine; Kaskazini, Kusini, Magharibi na katikati kama Singida, kuna utamaduni mzuri sana kule na vivutio vingi ambavyo tunaweza tukaiendeleza sekta hii ya utalii *(promotion of culture, tourism and historical).* Kwa ushauri wangu, ningependa kushauri kwamba, ijengwe *tourism centre* ambayo inaweza ikakusanya mambo yote yanayohusu *historical* na *culture* ambayo tunaweza tukatumia kwa ajili ya kuweka vivutio na kuwaita watalii wakaja wakatembelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajisikia wivu sana hasa unapoenda kwenye nchi za wengine, unakuta vitu vingine wamevitoa katika nchi nyingine, wanakuja kuweka kwenye jengo moja. Unaingia pale, unalipa pesa, unaenda unaambiwa hapa sijui walikuwa wanafanya nini. Hiyo yote ningeshauri Wizara hii iweze kujenga *centre* ya utalii ambayo itakusanya mambo yote yanayohusu tamaduni zetu za kila mkoa kwa ajili ya utalii *especially* pale Dar es Salaam Makumbusho. Kituo kile kingeweza kuendelezwa ili tuweze kupata *centre* kubwa ambayo tunaweza kuwapeleka watalii wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ninazungumzia kwamba, kuwepo na siku maalum; tuna Siku ya UKIMWI na Siku ya Malaria, sawa kuna wiki ya utalii, lakini ninapendekeza ziangaliwe zile *time* ambazo watalii wengi wanakuja Tanzania *(high season).* Watalii wanapofika, basi katika tarehe hizo, kutafutwe siku moja ambayo inakuwa ni Siku ya Utalii Tanzania. Kila mkoa ushiriki kwa namna yake na kuangalia kwamba; je, mwaka huu tunazingatia kwenye jambo gani ili tusije tukazingatia jambo moja na mambo mengine tukayaacha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kampuni moja ya TATA kutoka India. Kampuni hii inataka kuja kufanya mradi wa kutengeneza magadi pale Ziwa Natron. Ninaiomba

Serikali iheshimu sana maoni ya wananchi na wakati huo huo ninataka kusema kwamba, Tanzania ilikuwa imeridhia mkataba wa kutunza maeneo *unique,* yaani maeneo yale ambayo ni ya kipekee. Katika Ziwa Natron, kuna ndege ambao wanaitwa flamingo, mazalia yao yako pale. Wanatoka pande nyingi sana za dunia wanakuja, mazalia yao yako pale.

Sasa hii kampuni itakapoenda pale kunyonya yale maji, kutoa na kuharibu mazingira yale, ninaona Serikali izingatie sana, sioni kama kuna haraka; kwa nini tuwe na haraka ya kuweza mpaka kuita wawekezaji kutoka nje? Haya mambo yanatuletea matatizo, tusubiri sisi wenyewe, tunao vijana wetu ambao wanaendelea kusoma, watakuja kufanya hiyo kazi, tusikimbilie kuwapa watu wa nje kuja kuharibu maliasili zetu. Kwa hiyo, hilo ninaomba sana lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuzungumzia suala la utamaduni; utamaduni wetu wa kitaifa umekuwa hauzingatiwi katika suala la utalii *especially,* unaweza ukakuta kwamba, labda Zanzibar kule wao wanakuwa na utamaduni wao ambao wanauendeleza, Arusha wana utamaduni wao ambao wanauendeleza, lakini bado hatuna utamaduni ambao ni wa kitaifa, tunaoweza tukasema kwamba, sisi huu ndio utamaduni wetu. Kwa hiyo, ninaomba sana tamaduni zetu ambazo zinatoka kila mkoa na *history* za kila mkoa, ziwekwe mahali pamoja na kujenga *centre* ambayo tayari nimeshaitaja ili tuweze kupata pesa na hii inaweza ikawaletea ajira wazee wetu, maana ukienda nchi nyingine unakuta *Museum* kama hizi ambazo zimekusanya tamaduni zote za taifa zima zinakaa pamoja, wale wazee wanakaa kwa kutunza zile *history,* unaingia pale, unalipa na wale wazee ndiyo wanakuwa wanapata mishahara kutokana na utalii huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo, ninaomba niunge mkono hoja hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia nichukue fursa hii, niweze kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Prof. Abdallah Maghembe, pamoja na dada yangu, Mheshimiwa Zabein M. Mhita, kwa kutuletea Muswada huu muhimu na hasa kwa wakati huu ambapo nchi yetu tunahitaji hatua nyingi za kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kimsingi Muswada huu ni sahihi kabisa, wala hakuna sababu ya kusema, kwa mfano, kuna mambo ambayo tunayaona hayako sawasawa lakini ninaamini yaliyo mengi, yamelenga masuala muhimu na yamegusa utekelezaji hasa katika Sekta hii ya Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo hayo, ninatumia fursa hii pia niweze kuelezea mambo machache tu yanayohusiana na masuala muhimu hasa yanayohusu Sekta hii ya Utalii na hasa katika kuleta pato na kuongeza tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni sahihi kabisa kwamba, utalii ni jambo muhimu sana, pamoja na umuhimu wake wa kuitangaza nchi, pia unaleta Pato kwa Taifa. Kwa mazingira jinsi yalivyo, sekta hii inaonekana sana kugusa tabaka moja tu katika jamii na

tabaka hilo hasa ukitaka kufanya biashara hii ya utalii kwa mtu mwenye hali ya chini, kwa kweli ni ngumu sana kuifanya biashara hii, ninaamini watakaoweza kufanya biashara hii ya utalii ni watu wanye pesa nyingi na ambao wanaweza kumudu labda kukopa na wakaendesha biashara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaweza nikazungumzia suala moja tu, kwa mfano, nizungumzie leseni, ukate leseni ambayo inahusiana na *Travellers Tours*, ina *Grade* A na B. Hii leseni moja mtu kama mimi nataka nikachukue leseni *Grade* A ambayo sasa nitakuwa na uwezo wa kuweza kuwachukua watalii nikawapokea na baadaye nikawapeleka hotelini, halafu baadaye nikawachukua nikawatembeza katika mbuga za wanyama. Sheria inasema kwamba kwanza, leseni yenyewe ni dola 2000 ambayo ni sawa na shilingi milioni 2.5 kwa pesa za Kitanzania, pia unaambiwa lazima uwe na magari yasiyopungua matatu kwa ajili ya kuweza kuendesha shughuli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, magari haya, mathalani *Saloon* moja kwenye *show room* zetu zilizopo Dar es Salaam, unaweza kukuta inauzwa kiasi shilingi milioni tisa na unatakiwa uwe na *saloon* tatu kwa mfano, kwa hiyo, hapa ni lazima uwe na shilingi milioni 27, mbali na hizo, zipo gharama nyingine za uendeshaji, unatakiwa uwe na ofisi na vitendea kazi kama kompyuta na hata kuweka wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi ili uweze kuanza biashara hii ya utalii, wewe ukawa ni mfanyabiashara wa *travellers tours,* lazima uwe na shilingi milioni 40. Hili ninaona kwa kweli kama tunataka tuwasaidie wananchi wa kawaida, wanaotaka kufanya biashara hii lakini wanashindwa kutokana na mazingira ya ugumu wa leseni na mambo kama hayo, ninafikiri kwamba, lazima Wizara sasa tuone tutamuwezeshaje huyu mtu wa kawaida kabisa, ambaye naye ana hamu ya kufanya biashara ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nizungumzie juu ya Wizara hii inavyochukulia hili suala la utalii, hasa namna tunavyochukulia jinsi ya kutangaza makabila, mbona tunaona kabila moja tu peke yake ndiyo linatangazwa; tunaona Wamaasai pekee ndiyo wanaotangazwa; hivi hakuna makabila mengine; kwa nini tusiwatangaze Wanyiramba, Wagogo, Wanyisanzu au Wanyaturu? Tunayo makabila mengi, kwa hiyo, tusijikite kwenye eneo moja la kutangaza kabila moja. Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anisamehe, lakini ninazungumza kwa sababu Tanzania tuna makabila mengi, nayo yana haki na tunastahili tutangazwe ili sasa hawa watalii wanapokuja, waweze kuona masuala mengi na hasa ya kitamaduni yanayohusu makabila haya.

Kadhalika, nizungumzie masuala yanayohusu maeneo ya kiutalii, maeneo haya ni ya kiasili lakini sasa yameachwa ni kama yametelekezwa; kwa mfano, Bagamoyo, siamini kama kweli tunaichukulia kama ni sehemu mojawapo ya utalii, kwa sababu ninachoona hali halisi ya Bagamoyo ni kama vile inaisha, sidhani sasa kama yale majengo yanaangaliwa vizuri. Ninaomba pamoja na kutengeneza sheria hii, lakini ni lazima sasa Mheshimiwa Waziri tuhakikishe kwamba, yale maeneo yetu ambayo tunaamini ni ya utalii, tuyape kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia niweze kuzungumzia suala moja kuhusiana na visiwa vidogo vidogo, ambavyo tunavyo kandokando mwa bahari. Tunavyo visiwa vidogo vidogo, ukiwa unatoka kigamboni kwa mfano na hasa ukienda Zanzibar, utaviona vipo Visiwa vya Sinda na ukiendelea kule mbele kuna kisiwa kingine kinaitwa Bongoyo. Niliwahi kwenda Comoro, nimeona visiwa kama hivyo vinafanyiwa kazi na vinatoa pato kwa ajili ya maslahi ya nchi, lakini sisi tunavifanyia nini, sioni kama vinafanya kazi yoyote. Tutafute watu waende pale wakawekeze ili zifanyike shughuli za kiuchumi na kuongeza Pato la Taifa. Kwa hiyo, ninaomba sana tusiziache hizi fursa wazi, mwisho wake tutangojea wajanja watakuja watazivamia hizo fursa na ninaamini kwamb, baadaye italeta mgogoro na hautakuwa na maana hasa katika kuangalia maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninataka nizungumzie tena suala lingine muhimu, ambalo linahusiana na namna hasa sisi kama Tanzania, tunavyojitangaza kuhusiana na sekta hii ya utalii. Mara nyingi watu wanasema, adui yako mwombee njaa; kwa jirani zetu kuna machafuko yametokea na yanaendelea hadi hivi sasa, ingekuwa sisi Tanzania tuna matatizo hapa, kwa jinsi ninavyowafahamu, wale watu wangepiga debe na tusingemwona hata mtu yeyote kukanyaga hapa. Sasa je, sisi tumejipanga vipi kuweza kuwaeleza watalii wakaja hapa, tukawaeleza pamoja na mazingira mengine, sehemu moja ya *East Africa* ina mgogoro lakini kuna sehemu nyingine nzuri kama Dar es Salaam na kadhalika, kwa hiyo, mnaweza mkaja kupumzika. Sisi tunajifanya ndiyo waungwana au sijui ndiyo tuna dini sana, lakini ninachosema, tunahitaji fedha kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala si la kulilazia damu na bahati nzuri tulikuwa tunazungumzia pamoja na mgogoro huu tunaouona nchini Kenya unaendelea, mfano, bandari yao bado ina uwezo wa ku-*clear* makontena yapatayo 200 kwa siku, sisi hatuna mgogoro, lakini hatuna uwezo wa kuweza kufanya hivyo. Kwa hiyo, ninafikiri hizi nafasi ni vyema tukazitumia na kujipatia pato na haitakuwa dhambi wala hakuna tatizo lolote, kwa ajili ya nchi na maslahi ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kitu kimoja, ninaona Maafisa Utalii sijui wanaishia ngazi gani, wanasema wapo mpaka ngazi ya Mkoa, lakini kwa sababu hii kazi ya utalii, watu waliozungumza mkiangalia wazungumzaji wote, kila mmoja akizungumza katika eneo lake analotoka, kuna eneo la utalii na lina vivutio vingi. Nilikuwa ninaangalia kwenye Muswada hapa, mlikuwa mmezungumzia kwamba, patakuwepo na maofisa ambao watateuliwa, ambao watakuwa wanafanya kazi badala ya Mkurugenzi; sasa hawa maofisa kwa nini wawepo hadi katika kila Wilaya? Kama mlivyofanya Maofisa wa Maliasili, maana yake akiwa pale Wilayani, kazi yake itakuwa ni ku-*identify* na kuelewa maeneo mengi ya vivutio, kwa ajili ya faida na maslahi ya nchi yetu. Kwa hiyo, ninachowaomba, pamoja na mambo mengine, muangalie na uwezekano wa kuweza kuona kwamba, hawa maofisa wasitumike wakaishia kwenye ngazi fulani, kama tunaweza tuwasogeze mpaka kwenye Wilaya ili waweze kufanya kazi ambazo ninaamini, wataharakisha hii Sekta ya Utalii. Vilevile ninaamini kwamba, vivutio vingi vya nchi hii, vinaweza vikatoa pesa na tukajiongezea pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sikuwa na mchango mkubwa sana, lakini ninaamini kwamba, haya niliyoyazungumza, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri Katibu Mkuu na Watendaji wote wananisikia. Ninaamini tunazungumza kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu, kwa hiyo, kwa yale tuliyoshauri ambayo ni mazuri, tunaomba yaingizwe ili tuweze kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Msheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii ili niweze kuchangia Muswada huu uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Waziri, pamoja na Naibu Waziri, kwa kuleta Muswada huu wa Utalii. Kwanza kabisa, ninafikiri Mkoa wa Rukwa umesahaulika sana kwa mambo mengi; sijui Waziri anafahamu kwamba, katika mkoa huu kuna maporomoko au hakuna?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa, Sumbawanga Vijijini Kata ya Kasanga, kuna maporomoko ambapo upande wa Tanzania hatuna kitu chochote ambacho tumeweka, lakini wenzetu upande wa Zambia, maana yake yale maporomoko yapo mpakani katikati ya Tanzania na Zambia, lakini upande wa Tanzania hakuna kitu chochote ambacho tumefanya. Upande wa Zambia wamejipanga vizuri na wametengeneza njia nzuri ya kushuka kule kwenye maporomoko watalii wanapokwenda, wanakula dola 50 kwa kila mtalii, lakini sisi Tanzania hakuna kitu chochote ambacho tumekifanya mpaka sasa hivi. Sasa sielewi kama Waziri anajua kuwa katika Mkoa wa Rukwa kuna maporomoko au haelewi? Nitamwomba aje Mkoani Rukwa tumpeleke kwenye maporomoko ili aweze kuyaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika Mkoa wa Rukwa tuna Mbuga nyingi sana za watalii, mojawapo ni *Katavi National Park.* Hakuna hoteli kabisa katika Mbuga hii; imesahaulika kabisa na *National Park* ni kubwa sana na ina wanyama wakubwa kuliko hata Mikumi, huwezi ukamlinganisha tembo wa Mikumi na wa Katavi, tembo wa Katavi ni mkubwa na twiga wa Katavi ni mkubwa. Tuseme sijui sisi tumekosa miundombinu; sielewi kwa nini Wizara hii imetusahau kabisa? Katavi ni mbuga moja kubwa sana lakini ina miundombinu mibovu sana, ndiyo maana watalii wengi hawaji hata kuwekeza hoteli na hatuna uwanja wa ndege.

Mbunga ya Katavi, ingeleta mapato mengi sana katika taifa letu. Katika utalii kuna magari, basi tungekuwa tunaona magari ya utalii hata mawili yanapita yanabeba watalii, lakini hakuna gari lolote. Sasa sijui mmetusahau au hamuelewi kama ile *National Park* ina faida katika nchi hii au sijui ni vipi? Hii ni mbuga ambayo ni nzuri kama ingeweza kuboreshwa, ikajengwa hoteli nzuri ya kitalii na wawekezaji wangekuja wengi kama tungeweza kuitangaza. Ninaomba Wizara waitangaze *National Park* ya Katavi ili iweze kupata huduma nzuri na bora ili watalii wanapokuja nchini Tanzania, wafike Mkoani Rukwa pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwa sababu Mkoa wa Rukwa hatuna Barabara ya lami, ndiyo maana watalii hawaji, lakini kama Serikali wangeweza kujipanga vizuri, basi wangeweza kutuboreshea tu hata kiwanja kile cha Wilaya ya Mpanda, kwa sababu Wilaya ya Mpanda ndiyo *National Park* ya Katavi iliko. Wakiboreshe Kiwanja cha Ndege cha Mpanda ili tuweze kupata watalii wengi na Mbuga za Mkoani Rukwa zingejulikana. Vilevile Mkoani wa Rukwa tuna Ziwa Tanganyika, kwa upande wa Kalema tu peke yake, kuna mambo mengi mazuri ya kale ambayo kama tungejipanga vizuri, yangekuwa utalii katika nchi yetu.

Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, ajipange vizuri ili aje autembelee Mkoa wa Rukwa, aone utalii jinsi ulivyo. Ninafikiri anaweza akatuletea watalii wengi sana au akaboresha mkoa wetu ili uwe mkoa wa kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo haya ya utalii, vilevile tunaweza tukapunguza tatizo la ajira; kama hoteli ikijengwa Mpanda au *National Park* ya Katavi, tayari tumeshatoa ajira kubwa sana kwa vijana wengi wa Mkoa wa Rukwa na Wilaya ya Mpanda. Ninawaomba Waziri, pamoja na Naibu Waziri, waje kufanya ziara waone yale mapori, siyo Katavi tu, kuna mapori makubwa ukielekea Inyonga na ninafikiri kuna vitalu vingi vikubwa, mje muangalie hivyo vitalu muone ni jinsi gani ya kujipanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, sikuwa na mengi ya kuzungumza siku hii ya leo, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ninashukuru sana. Kwa jioni hii, msemaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kukushukuru sana, kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kabla sijachangia, ninapenda kuchukua nafasi hii, kwa niaba ya Wananchi wa Serengeti, kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *AU*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais wetu, alichaguliwa wakati nikiwepo na kwa kweli wengine tulikuwa hapa, machozi yalitaka kututoka kwa furaha. Hii ni sifa sana, tukijua kwamba, amekuwa Rais kwa muda wa miaka miwili, ametuletea sifa na tuliopo alichukua kiti na alikiendesha kwa uhakika kabisa, kwa hiyo, ninapenda kumpongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa kuleta Muswada huu, ninafikiri Muswada huu ulitakiwa uwepo jana lakini tunashukuru leo umekuwepo.

Mheshimiwa Naibu spika, nilikuwa ninataka kusema kwamba, kama kuna kitu ambacho Watanzania wanaweza kukitegemea katika kukuza uchumi wetu ni utalii ambao unajumuisha hifadhi na vivutio vingine. Ili tuweze kufanikiwa, kuna kitu kimoja ambacho tunatakiwa tujue kwamba, utalii unategemea nguzo moja muhimu ambayo Tanzania inayo na inajivunia, kitu hicho ni amani. Bila amani nchini, usitegemee kama

utalii unaweza kuwepo na hivyo ninapenda kusema kwamba, amani tuliyonayo, tunatakiwa tuitumie kuhakikisha kwamba, utalii unashamiri hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nilienda Zimbabwe mwaka 2007, nilishangaa kwamba niliishi katika ile nchi kuanzia mwaka 1988 mpaka 1991, *Victoria Falls* ilikuwa huwezi kupata *booking;* watu wanaingia wanaenda *christmass* wana-*book* kwamba mimi nitarudi hapa *christmass* ijayo, leo ukienda *Falls* iko tupu na hoteli zile za *Elephant*, *The kingdom* na nyinginezo zipo lakini hazina watu kabisa na unajua kilichotokea huko. Kwa hiyo, tunapenda sana Watanzania tuhakikishe kwamba, amani inakuwepo na tunapata pesa za watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, madini haya mnayoyaona yataisha, ile si *renewable resource* ni kitu ambacho kinaisha na kuna wengine wanaanzisha miji, tuwaambie Watanzania wasianzishe miji kwenye migodi.

Nimekuta watu wanajenga miji kwenye migodi; wale wafanyakazi, yale madini yataisha lakini ukijenga karibu na hifadhi ya wanyama; wanyama hawa wataendelea kuwepo na utalii utaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sehemu fulani, ambayo tunakiwa tupeleke nguvu ya utalii, mojawapo ni *beaches*. Ukisikia watu wanakwenda Bahamas au Jamaica, wanakwenda kujianika kwenye jua, sisi tunazo fukwe ambazo ni Pwani lakini utakuta kwenye *beach*es zetu hakuna mtu, kwa sababu hazitunzwi vizuri.

Tujaribu kwenda pale *Koko Beach,* kuna watu wengi utakuta wanaogelea lakini angalia ile *structure* iliyopo pale, haifai kabisa, utaenda pale *White Sands* na hoteli zile zote utakuta watu wamekaa ndani na hakuna mtu aliyeko kwenye *beach*.

Tukizitumia zile *beach*es zinaweza kuwa ni mahali ambapo tunaweza kuziendeleza sana na tukapata watalii wengi kuliko kusema mtalii akishuka ni lazima aende kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ukienda Namibia, kitu cha kwanza unaenda kwenye kuruzi, hata mimi Mtanzania nikienda kule nikifika tu, ninaweka sanduku langu ninaenda kufanya kuruzi. Ukienda *Victoria Falls* Zimbambwe, kitu cha kwanza unafanya kuruzi, unapigwa muziki watu wanakunywa vinywaji vyao na wanalipa dola karibu 50 wanapelekwa kilomita kama kumi wanarudi, sisi hatuna kuruzi Dar es Salaam ianzie pale Kilimanjaro Hoteli iende mpaka Sea Cliff Hoteli, tutapata hela nyingi sana.

Sisi tumekazania utalii wa wanyama tu, siyo kila mtalii atapenda kuona wanyama, lazima utoe na kuruzi, wengine wanakuja kufurahia maisha yao, wengine wameoana wanataka kucheza muziki kwenye kuruzi, unapigwa na anaifurahia Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine kinachoshangaza, hivi mtalii akifika Dar es Salaam usiku anaenda wapi; kuna sehemu kweli za *high quality* ambazo wanapeleka wageni, watalii wanaenda wanakuta wamejaa, kuna sehemu wanapiga miziki ya asili? Hakuna, nenda Zimbabwe pale *Victoria Falls*, mimi nikifika kitu cha kwanza, ninajua niende Rainbow Hoteli kuangalia muziki wa kienyeji na wapo watalii pale, kwa hiyo, tusidharau miziki yetu ya kienyeji na chakula cha asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Arusha kidogo wanajitahidi, lakini nao bado, vituo vya asili hakuna, tukumbuke kuviweka. Kuhusu Hifadhi zetu za Kanda za Kusini, tuna hifadhi nzuri sana Ruaha, Mahale, Ngombe, Mikumi na Udzungwa. Hiadhi ambayo ninaiheshimu sana kuliko kule ninakotoka ni Udzungwa, kwa sababu mimi ni mwanamisitu, lakini ukweli, hatujaweka nguvu za kutosha, tunaongelea Serengeti wakati imejaa watalii mpaka mahali pa kuwaweka hakuna, unajua Kilimanjaro tunaogopa hata *environment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Ngorongoro, ukiangalia wale simba wanavyohangaika, ukifika tu na gari wanakuja kulala chini, lakini Kusini tumekusahau. Tunataka Hifadhi hizi za Kusini zipewe nguvu na kule watu waweze kupata mapato, mtu akizaliwa Arusha na mwingine Mtwara; hivi hawa watu wapo sawa?

Mtu wa Arusha, uwezekano wa kupata kazi ni mkubwa kuliko wa Mtwara, kwa sababu kuna vigezo na mahoteli yanakwenda huko, kwa hiyo, tupeleke kipato huko, tumepeleka umeme na utalii unaweza kushamiri huko.

Hoteli zetu *standard* kwa kweli zinasikitisha; bei ni kubwa, juzi nilikwenda kwenye hoteli moja, nikauliza hapa dola ngapi; wakaniambia dola 250! Hoteli kama ile ukienda South Africa ni dola 50, hoteli za hapa *standards* zake ni mbovu lakini bei kubwa, yanatumalizia utalii, halafu hatujazi-*grade* tunangojea nini?

Hivi leo ukienda Holiday Inn, Court Yard, Palm Beach pale Dar es Salaam ni star ngapi? Hivi tunangojea nini ku-*grade* hizo hoteli; inachukua mwaka, karne, tunataka hoteli zipewe *grade* ili kupandisha *standard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachosikitisha, nenda kwenye hifadhi, hoteli nyingi asilimia 90 ni za wageni, hakuna Mtanzania mwenye hisa katika hoteli hizo. Sisi Watanzania tunatunza wanyama, watu wangapi wanauawa na wanyama, mfano Serengeti, mazao yanaliwa na wanyama, halafu tunaweka mazingira ya kuwapatia wageni ndiyo waweke hoteli, Watanzania tumelala; mbona Dubai ukitaka kuanzisha biashara, lazima uwe na ubia; Malaysia ukitaka kuanzisha biashara lazima uwe na ubia; hivi sisi Watanzania tunatunza hifadhi hizo kwa nguvu zetu zote; *TANAPA* inazilinda lakini anaye-*invest* mle ni mtu kutoka nje, anachofanya ni kulipa kodi tu faida yote inaenda nje?

Watanzania lazima wapewe fursa humo, tusikumbatie wageni, hatutafika popote wala usije ukadanganyika, kitendo cha Watanzania cha kusema hatuwezi, *breweries*

hatuwezi kuimiliki mpe mgeni, Kilimanjaro mpe mgeni, hoteli za kitalii wape wageni! Watanzania tunasema hatuwezi hiyo itatuumiza, hifadhi zile Watanzania wa-*invest* mle.

Tunazo benki, unafikiri wale Wazungu wanatoa wapi pesa; wanakopa kwao na wanakuja kuiwezeza kwetu. Serikali lazima iweke utaratibu kwamba, zikopeshe Watanzania tuweze ku-*invest.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoshangaza, hoteli zinajengwa kwenye hifadhi lakini chakula kinatoka huko nje hata maji! Mheshimiwa Rais, wakati anafanya kampeni, alikwenda Serena Hoteli akapewa maji ya nje, akayakataa akasema hivi hapa Kilimanjaro hamna?

Wanasema kuku wa Tanzania hawa wa kienyeji wana minyoo, kuku wanatoka Brazil, South Africa, lakini Mtanzania yupo pale; kibaya zaidi hakuna ushuru unaopatikana kutoka kwenye hoteli hizo.

Hoteli kama Serengeti na nyinginezo, yangetoa chochote katika Halmashauri, sisi tungekuwa matajiri kuliko wote; wale watu hata laki moja hawafiki pale Mugumu, wamejiweka pale wanafaidi ndege zinakuja wanaenda Mtanzania kuingia pale huwezi hata kupata chakula.

Mtu wa Serengeti hawezi kuwa na uchumi kama huo na Serikali ina-*responsibility* ya kuhakikisha kwamba, Watanzania wanafaidi; tunataka ushuru wa kitanda, hatuwezi kuwalindia watu wanyama, watuzuie hata kuingia mle; halafu Serikali ikafanya sisi hata kupata senti moja mle hamna!

Mheshimiwa Naibu Spika, tungekuwa ni matajiri kama Zimbabwe, nenda ukaone wale wanaopakana na hoteli, wanapata chochote pale lakini sisi hatupati chochote. Tumekuwa kama watumwa, kila kitu kina mwisho, tunataka Serikali ije na tamko kwamba, Serengeti itafaidi.

Ukienda Mahale kwa Mheshimiwa Manju S. O. Msambya pale wafaidi, Udzungwa wafaidi. Waha kule niambie Mto Ruaha wanapata nini, Selous hamna kitu, wananchi wanakuwa ni watumwa wa pale, hatuwezi kuwa watumwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kusema mengi, ila sisi Watanzania ni lazima tuseme tunaweza, kinachotumaliza tunasema hatuwezi, tumewakabidhi wageni hifadhi zetu, kitendo hiki kinaniumiza sana. *Breweries* unauza, hifadhi unauza, kila kitu kinaenda kwa wageni, *we can do it,* tusijidanganye tunaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba hifadhi zetu zipewe Watanzania. Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, ameomba *site* mara ngapi, lakini hamna kitu?

Kwa hiyo, ili tutunze zile hifadhi ni lazima tu-*invest* mle ndani na mimi kama Mbunge wa Serengeti, wananisikia, lazima tupate ushuru wa kitanda, ndiyo utatupa motisha ya kulinda wale wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, ninasema ninaunga mkono hoja na ninaamini hayo niliyoyasema, Serikali ita-*take note.* *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, si kwamba, orodha yangu imeisha ipo, kesho tunaanza na Mheshimiwa Adam K. Malima, Mheshimiwa Brig. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Benadeta K. Mushashu, Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah na Mheshimiwa Samuel M. Chitalilo, hawa ndiyo watakaozungumza kesho. Tunakusudia kesho Muswada huu uishe, hasa kipindi cha asubuhi, baada ya hapo tutajiandaa na Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa sababu ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *AU*. Tutakuwa na Azimio hilo, tutaenda kujiandaa halafu ratiba nyingine zitaonekana kwenye *Order Paper* ya kesho.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa hatuna kitu kingine, ninapenda kuahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.40 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne Tarehe 5 Februari, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*